ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis - Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 14 Juni, 2016

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Spika,(Zubeir Ali Maulid) Alisoma Dua

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika. Kwanza nichukue fursa hii kumpa pole Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum Mhe. Said Soud Said kwa kukatiwa mikarafuu yote kule Pemba.

Hoja yangu ni kuhusu jana utaratibu. Serikali jana iliniahidi kwamba italeta jawabu, lakini naona mpaka leo kimya, na ukizingatia kule tarehe 17 waliyopewa ndio mwisho ng'ombe wale watapigwa mnada au watataifishwa, na hili suala linaumiza kichwa na sijapata jawabu mpaka muda huu, na ukizingatia tarehe ya mwisho ni kesho kutwa.

Mhe. Spika: Ahsante nimesikia hoja yako Mhe. Mjumbe, ndio kwanza asubuhi sasa hivi, pengine majibu utayapata, endelea kustahamili Mheshimiwa. Tuendelee Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, hii ni hotuba ya Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto Mhe. Moudline Cyrus Castico ambaye ni mimi, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2010/2017 katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kupokea, kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kwa mara nyengine kukutana hapa leo, tukiwa wazima wa afya na kunijaalia afya njema na uzima, nikaweza kuwasilisha utekelezaji wa Programu za Wizara kwa mwaka 2015/2016 na mwelekeo wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Wafanyakazi wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa tena kwa mara ya pili kuiongoza nchi hii na kwa ushindi wake wa kishindo na wa historia tokea kuanza kwa Mfumo wa Vyama vingi Zanzibar.

Ushindi huu, unadhihirisha wazi imani za wananchi kwake na ubora wa Sera za Chama Cha Mapinduzi katika kuleta Maendeleo endelevu nchini. Kwani sote ni mashahidi kuwa Uongozi wake mahiri, thabiti na makini utaendelea kuwa dira katika utendaji wa kazi zetu na mendeleo ya nchi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kumjaalia afya njema, uadilifu, maarifa na hekima katika kuiongoza nchi yetu.*(Makofi)*

Mhe. Spika, aidha, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mungu kunifanya nipate kibali cha kuteuliwa na Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein kunipa dhamana ya kuiongoza Wizara hii nyeti. Naomba mashirikiano na wadau wote ili tuweze kutoa mchango na kutekeleza majukumu yetu ipasavyo. Mungu atupe hekima upendo na busara. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kuwapongeza Mhe. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Tano na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa ni Mwanamke wa kwanza kushika nafasi kubwa ya Uongozi nchini.

Kuchaguliwa kwake kumeipa hadhi kubwa Zanzibar na Tanzania katika ulingo wa Kimataifa na inaonyesha ni kwa namna gani nchi yetu inathamini mchango wa Wanawake katika maendeleo ya Taifa. Serikali imejipanga kuhakikisha uwiano huu utaendelezwa katika ngazi zote za Uongozi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia nampongeza Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa kuchaguliwa tena kuendelea kumshauri na kumsaidia kwa karibu

Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuliongoza Baraza hili, nataraji kwamba utaliongoza Baraza kwa hekima, busara na uadilifu mkubwa kwani naamini kuwa una uzoefu na uwezo mkubwa kiutendaji. Nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza kwa kuchaguliwa na kuteuliwa kuwatumikia wananchi. Nawatakia kazi njema na ufanisi mkubwa wa kutekeleza majukumu yao. Vile vile, napenda kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa michango yao na miongozo wanayotupatia katika kuongeza ufanisi wa kiutendaji wa Wizara.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa kuwatambua Wajumbe wa kamati kama ifuatavyo;

1. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	Mwenyekiti
2. Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma	Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Abdalla Mussa	Mjumbe
4. Mhe. Maryam Thani Juma	Mjumbe
5. Mhe. Zainab Abdalla Salum	Mjumbe
6. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	Mjumbe
7. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Mjumbe
8. Mhe. Mussa Foum Mussa	Mjumbe
9. Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
10. Ndg. Latifa Saleh Suleiman	Katibu
11. Ndg. Makame Salim Ali	Katibu

Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa nawapa pole wananchi wote waliopatwa na maafa wakati wa mvua kubwa na kupata athari kwa njia moja au nyengine na nawapa pole wananchi wote walioathiriwa na kipindipindu kwa kuondokewa na ndugu zao au wapendwa wao.

Napenda kutoa wito kwa jamii tuwe na tabia ya kupenda usafi na kuweka mazingira yetu safi, KWANI ZANZIBAR BILA YA KIPINDIPINDU INAWEZEKANA.

Mhe. Spika, pia, natoa masikitiko yangu makubwa kwa vitendo vya ukatili vinavyoendelea kukithiri katika jamii yetu siku hadi siku. Naomba nitowe wito kwa vyombo vya Sheria na jamii kwa ujumla tushirikiane katika kulitokomeza tatizo hili na naviomba vyombo vya Sheria kutoa

hukumu stahiki itakayotoa funzo kwa wengine kutorejea makosa haya. Pia, nawapa pole waathirika wote waliofikwa na tatizo hili.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii nitoe maelezo ya mapato, matumizi na utekelezaji wa Programu za Wizara kwa mwaka 2015/2016 pamoja na Mwelekeo, Vipaumbele, Programu na Makadirio ya Bajeti kwa mwaka 2016/2017

MUHTASARI WA MATUMIZI NA MAPATO KWA MWAKA 2015/2016

Mhe. Spika, katika kutekeleza majukumu yake kupitia Mfumo wa Programu kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ilitengewa jumla ya Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Tano Arobaini, Laki Moja Sitini na Nne (Tshs. 7,540,164,000/=) kwa kutekeleza Programu Kuu tano (5) na Programu ndogo kumi na tatu (13). Kati ya hizo Shilingi Milioni Mia Sita Sitini na Tisa, Laki Saba na Elfu Sabini na Sita (Tshs.669,776,000/=) zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Shilingi Milioni Mia Tatu, Laki Sita na Elfu Kumi na Tisa (Tshs. 300,619,000/=) zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kukuza Usawa wa Jinsia na Kuwaendeleza Wanawake.

Shilingi Bilioni Tatu Milioni Saba, Laki Moja na Elfu Sabini na Moja (Tshs.3,007,171,000/=) zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kuimarisha Hifadhi ya Jamii na Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Thelathini na Saba, Laki Tano na Elfu Thalathini na Nne (Tshs.3,037,534,000/=) zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Uongozi na Mipango ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na Shilingi Milioni Mia Tano Ishirini na Tano na Elfu Sitini na Nne (Tshs.525,064,000/=) zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kuratibu Uzalishaji, Upatikananji wa Ajira za Staha na Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria za Kazi.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi wa Mei, 2016, fedha zote zilizotolewa ni Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Nane Sitini na Mbili, Laki Nane na Elfu Thamanini na Sita, Mia Saba na Sabini na Nne (Tsh 3,862,886,774/=) ambayo ni sawa na asilimia Hamsini na Moja (51) kwa utekelezaji wa Programu zote. Kati ya hizo Shilingi Milioni Mia Nne Hamsini na Mbili, Laki Mbili na Elfu Thalathini na Tatu, Mia Nane Arobaini (Tshs 452,233,840/=) zilitumika kwa ajili ya kutekeleza Programu ya

Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambayo ni sawa na asilimia Sitini na Saba Nukta Tano (67.5) ya fedha kwa programu hiyo.

Shilingi Milioni Mia Moja Tisini na Saba, Laki Tatu na Elfu Sitini na Nane, Mia Mbili na Nane (Tshs 197,368,208/=) zilitumika kwa kutekeleza Programu ya Kukuza Usawa wa Jinsia na Kuwandeleza Wanawake ambayo ni sawa na asilimia Sitini na Sita (66) ya fedha kwa Programu hiyo. Shilingi Milioni Mia Tisa Sitini na Sita, Laki Tano na Elfu Nne, Mia Mbili Tisini na Mbili (Tshs 966,504,292/=) zimetumika kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kuimarisha Hifadhi ya Jamii ambayo ni sawa na asilimia Thalathini na Mbili (32).

Jumla ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tatu na Nane, Laki Nne na Elfu Kumi na Sita, Mia Nane Thalathini na Nne (Tshs 2,308,416,834/=) zimetumika kwa kutekeleza Programu ya Uongozi na Mipango ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto sawa na asilimia Sabini na Sita (76) ya fedha za Programu hiyo. Jumla ya Shilingi Milioni Mia Tatu Hamsini na Tatu, Laki Tatu na Elfu Sitini na Tatu, Mia Sita (Tshs.353,363,600/=) zimetumika katika kutekeleza Programu ya Upatikanaji wa Ajira za Staha na Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria za Kazi sawa na asilimia Sitini na Saba (67) ya fedha kwa programu hiyo. (Kiambatanisho namba 1 kinahusika).

MAPATO KWA MWAKA 2015/2016

Mhe. Spika, wizara ilitarajiwa kukusanya kiasi cha Shilingi Milioni Mia Tatu Arobaini na Mbili, Laki Tisa Elfu Thamanini na Saba, Mia Sita (Tshs 342,987,600/=) kupitia Ada za Usajili na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira nje ya Nchi, Ada ya Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi na Vibali vya Kazi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara kupitia Kamisheni ya Kazi, Idara ya Ajira, Idara ya Usalama na Afya Kazini na Idara ya Ushirika ilikusanya jumla ya Shilingi Milioni Mia tatu na Kumi na Tano Elfu (Tshs.315,000,000/=) kutokana na Ada za Usajili na Ada ya Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika na Vibali vya Kazi ambayo ni sawa na asilimia Tisini na Mbili (92) ya Makadirio ya Makusanyo (Kiambatanisho namba 2 kinahusika).

VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2016/17

Mhe. Spika, wizara kwa mwaka 2016/2017 imejipangia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

1. Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Ajira kwa Vijana na kuimarisha usimamizi wa Sheria za Kazi.
2. Kupanua programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pamoja na kuimarisha mfumo wa Ushirika.
3. Kuimarisha Mfumo wa Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini wa Programu za Hifadhi ya Wazee , Vijana, Wanawake na Watoto.
4. Kuimarisha Mfumo wa Hifadhi ya Jamii.
5. Kukuza Usawa wa Kijinsia na Mapambano dhidi ya Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto; na

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA 2015/2016

Mhe. Spika, wizara kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 ilijipangia kutekeleza Programu kuu tano (5) na Programu ndogo kumi na tatu (13) kupitia Idara zake kumi na moja (11) na taasisi mbili (2) zifuatazo:

1. Kamisheni ya Kazi;
2. Idara ya Ajira;
3. Idara ya Usalama na Afya Kazini;
4. Idara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi
5. Idara ya Maendeleo ya Ushirika;
6. Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii;
7. Idara ya Maendeleo ya Vijana;
8. Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto;
9. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
10. Idara ya Utumishi na Uendeshaji na
11. Ofisi Kuu Pemba

Wizara ina taasisi zifuatazo:

1. Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; na
2. Baraza la Vijana

Mhe. Spika, Wizara kwa mwaka 2015/2016 imetekeleza Programu zifuatazo:

Programu ya Kuratibu Uzalishaji, Upatikanaji wa Ajira za Staha na Usimamizi wa Sheria za Kazi

Mhe. Spika, Programu Kuu hii ina lengo la kupunguza tatizo la ukosefu wa Ajira kwa Vijana na kuzingatia Sheria na Miongozo ya kazi ikiwemo masuala ya usalama na afya kazini. Programu Kuu hii ina Programu ndogo zifuatazo:

Programu ndogo ya Ukuzaji na Upatikanaji wa Ajira zenye Staha

Mhe. Spika, Programu hii inatekelezwa na Idara ya Ajira na inalengo la kukuza na kuongeza upatikanaji wa ajira zenye staha nchini ili kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira hasa kwa vijana kwa kutekeleza Sera ya Ajira na Mpango wa Ajira kwa Vijana. Programu hii ina jukumu la kusimamia Mfumo wa Taarifa za Soko la Ajira ambao unakusanya, unachambua, unahifadhi na unatoa taarifa za Soko la Ajira kwa watafuta kazi, waajiri na wananchi. Kwa mwaka 2015/2016, Programu hii ndogo imetekeleza yafuatayo:

Mhe. Spika, Programu hii imetoa mafunzo kwa vijana 264 Unguja na Pemba (Wanawake 165 na Wanaume 99) ya kuwawezesha kujiajiri na kuajirika. Mafunzo hayo ni pamoja na kuwajengea uwezo wa kujiamini katika kukabiliana na usaili (*Interview*) pamoja na uandikaji wa maelezo binafsi (*CV*).

Mhe. Spika, Programu kupitia Mfumo wa Taarifa za Soko la Ajira imetangaza nafasi 284 za ajira katika sekta za utalii na viwanda, zilizofuatiliwa na kukusanywa kutoka kwa Kampuni na Taasisi binafsi zilizopo Zanzibar ili kuwarahisishia vijana wanaotafuta kazi kupata taarifa za ajira kwa urahisi. Vijana wamepata fursa ya kuweza kuzungumza na waajiri na kukubaliana kuingia katika ajira rasmi. Pia, imewawezesha vijana kutambua na kufuatilia fursa za ajira zilizo katika taasisi mbali mbali za kazi kwa hapa Zanzibar, Tanzania Bara, Afrika Mashariki na nchi za nje.

Mhe. Spika, Programu kwa kushirikiana na Wakala Binafsi wa Ajira imewaunganisha na waajiri vijana 498 (wanawake 246 na wanaume 252) kwenda kufanyakazi katika nchi za Oman, U.A.E, Qatar, Kuwait na Saudi Arabia. Vijana hao wameajiriwa kwa nafasi za kazi za udereva, saluni, hoteli, upishi, kazi za nyumbani, ubaharia, taasisi za fedha, kazi za viwandani na ulinzi katika sekta binafsi. Pia, Programu ilifanya ukaguzi

kazi kwa taasisi kazi 114 na kugundua kwamba jumla ya Vijana 9,542 wapo kazini katika taasisi mbali mbali za binafsi Unguja na Pemba. (Kiambatanisho namba 3a na 3b kinahusika)

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2015/2016, programu imerusha hewani Vipindi 10 vya Redio na 4 vya TV kupitia vyombo vya habari vilivyopo Zanzibar ikiwemo vya *ZBC* ili kuelimisha jamii kufahamu umuhimu wa ajira, changamoto zinazotokana na ajira na suluhisho la changamoto hizo pamoja na athari za baadae katika sekta hii. Kupitia vipindi hivyo, Programu iliweza kuwafahamisha wananchi hasa vijana juu ya Mikataba na Miongozo ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa inayohusu ajira ili kuifahamu na kuifuata kikamilifu kwa madhumuni ya kukuza ajira zenye staha.

Mhe. Spika, Vile vile, katika kusimamia ipasavyo Sheria za Kazi, kupunguza manung'uniko na uvunjaji wa Sheria, Programu ilizikagua Kampuni saba (7) za Wakala Binafsi wa Ajira zilizosajiliwa rasmi na taasisi tatu (3) zilizoomba usajili wa kufanyakazi za Uwakala wa Ajira. Katika ukaguzi huo imeonekana kwamba bado wakala hawa wana ufahamu mdogo wa kuzitambua Sheria za Kazi na Mikataba ya Kimataifa inayohusiana na kazi za Uwakala.

Mhe. Spika, Programu ilishiriki mikutano 14 ya Kikanda na ya Kamati mbali mbali iliyoandaliwa na Washirika wa Maendeleo inayohusu masuala ya Ajira ndani na nje ya nchi. Mikutano hiyo ilikuwa na lengo la kukuza mahusiano na kuweka mikakati bora na imara ya kukuza ajira na kuhakisha utekelezaji wa Mipango iliyopo. Pia, Programu kwa kushirikiana na wadau wengine iliandaa Tamasha la Vijana na Ajira lililofanyika tarehe 30/04/2016 ambalo liliwashirikisha vijana 500 na Kampuni 24 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar na imewaunganisha Vijana hao na waajiri**.**

Mhe. Spika, Programu imezijengea uwezo Kamati 11 za Kisekta za Uzalishaji wa Ajira Unguja na Pemba zenye wajumbe 165 kuutambua Mpango wa Ajira kwa Vijana 2014 - 2018 na kuutekeleza ipasavyo kupitia Wilaya na Kamati zao ili kupunguza tatizo la ajira kwa vijana. Kupitia mafunzo hayo, Kamati hizo zimetayarisha mipango kazi ya uzalishaji ajira katika Wilaya zao. Programu ilifanya mikutano 4 ya Kamati za Kisekta za Uzalishaji Ajira kwa madhumuni ya kufahamu mafanikio na changamoto wanazokabiliana nazo na kupanga mikakati itayowashirikisha vijana katika

kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira na kiwango cha chini cha ajira.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu hii imelenga kuimarisha Mfumo wa ukusanyaji na uwekaji wa taarifa za soko la ajira; kutoa mafunzo ya kuweza kujiajiri kwa Vijana 300 kwa kushikiana na Kituo cha Kulea Wajasiriamali pamoja na taasisi mbalimbali.; kuwaunganisha watafuta kazi na waajiri; kujenga uwezo wa Vijana 120 kukabiliana na waajiri na kutangaza nafasi za ajira kupitia mfumo wa taarifa za soko la Ajira.

Mhe. Spika, Naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Ishirini na Tisa, Laki Tano na Elfu Kumi na Mbili (Tshs.29,512,000/=**)** kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii ndogo kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Maelezo kamili ya Programu hii ndogo yanapatikana katika kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu *(PBB)* kwa mwaka wa fedha 2016/17 - 2018/19 ukurasa wa Q26.

Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria za Kazi

Mhe. Spika, Programu hii inasimamiwa na Kamisheni ya Kazi na inalengo la kuhakikisha Sheria za Kazi zinatekelezwa katika taasisi zote za umma na binafsi. Kamisheni ya Kazi imetekeleza Program ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya pamoja kazini kwa lengo la kusimamia viwango vya kazi vya Kitaifa na Kimataifa, pamoja na kuhakikisha kuwa taasisi zote za kazi zinatekeleza viwango hivyo ipasavyo, kama zilivyoainishwa katika Sheria za Kazi.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2015/2016, Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria za Kazi imetekeleza yafuatayo:

Imefanya ukaguzi kazi kwa Taasisi 114 (83 Unguja na 31 Pemba) ili kuhakikisha kuwa zinafuata Sheria za Kazi ipasavyo. Kupitia ukaguzi huo, Taasisi 46 zimegundulika kuwa na kasoro katika utekelezaji wa Sheria za Kazi na zimepewa maelekezo ya kurekebisha kasoro hizo katika muda maalumu uliopangwa. Pia, hatua za ufuatiliaji juu ya utekelezaji wa maelekezo na maagizo kwa wahusika umefanywa.

Mhe. Spika, Jumuiya ya Waajiri na Vyama vinne (4) vya wafanyakazi vilikaguliwa chini ya Sheria ya Mahusiano Kazini Nambari 1 ya mwaka

2005, ambapo vimehimizwa kutekeleza Sheria za Kazi kama inavyotakiwa ili kukuza mahusiano mema baina ya Wafanyakazi na Waajiri katika sehemu za kazi. Jumla ya migogoro ya kazi 101 imesuluhishwa na kupatiwa ufumbuzi kwa wahusika kupata haki zao kwa mujibu wa Sheria. Migogoro hiyo ilihusu kusimamishwa kazi, kufukuzwa kazi, kutolipwa mshahara, kukatishwa mikataba na haki nyenginezo.

Mhe. Spika, Programu imetekeleza Mpango wa Ajira za Watoto ambapo imeweza kuhamasisha jamii juu ya tatizo la ajira kwa watoto, kuzisadia familia maskini 1,500 katika Wilaya 11 za Unguja na Pemba ambazo watoto wao wanajishughulisha na kazi na kuwarejesha Skuli watoto 5,067 (2079 wanawake na 2988 wanaume) waliotoroka ili kuendelea na masomo badala ya kufanya kazi. Familia 1,065 zimepatiwa sare za Skuli pamoja na vifaa vya kuanzishia miradi vikiwemo mafriji na mifugo.

Mhe. Spika, Programu kupitia Kamisheni ya Kazi itatekeleza Programu ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Sheria za Kazi na Majadiliano ya Pamoja ambapo itafanya Ukaguzi Kazi kwa taasisi 240, itaendelea kutekeleza Mpango wa kupambana na Ajira za Watoto, itafanya ukaguzi kazi kwa vyama vya waajiri na wafanyakazi 14 na kusuluhisha migogoro ya kazi 140.

Mhe. Spika, Naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Sitini na Mbili, Laki Tatu na Elfu Hamsini (Tsh.62, 350,000/=) kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ili Wizara kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria za Kazi. Maelezo kamili ya Programu hii ndogo yanapatikana katika Kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu *(PBB)* kwa mwaka wa fedha 2016/17 - 2018/19 ukurasa wa Q27.

Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini inasimamia utekelezaji wa Sheria Nambari 8 ya mwaka 2005 ya Usalama na Afya Kazini na inasimamiwa utekelezaji wake na Idara ya Afya na Usalama Kazini. Programu hii kwa mwaka 2015/2016 ilitekeleza yafuatayo:

Ilifanya ukaguzi katika sehemu 113 (Unguja 76 na Pemba 37) za kazi na kusimamia Sheria Nambari 8 ya mwaka 2005, Kanuni na Miongozo ya Usalama na Afya Kazini. Pia kuwapa maelekezo na kutoa miongozo kwa

waajiri na waajiriwa juu ya umuhimu wa kuweka mazingira bora ya Usalama na Afya Kazini ili kujikinga na matukio ya ajali na maradhi katika maeneo ya kazi.

Imefanya uchunguzi wa matukio ya ajali na maradhi yatokanayo na kazi katika sehemu nne (4) za kazi *(Plan Hotel Dream, Ocean Paradise, Vera Hotel Nungwi na Sayon Brother Limited)* ambazo ziliripoti kupata ajali na imeonekana kuwa sababu kubwa za matukio hayo ni uchache wa vifaa vya kujikinga na uelewa mdogo juu kujikinga na madhara yatokanayo na kazi.

Ilifanya usajili wa Sehemu za Kazi 51 (Unguja 37 na Pemba 14) kwa ajili ya Usalama na Afya Kazini kwa lengo la kuzitambua maeneo zilipo na shughuli wanazozifanya ili ziweze kufikiwa kwa urahisi kwa kufanyiwa ukaguzi wa Usalama na Afya Kazini na kufanya tathmini ya madhara yanayoweza kutokea ili kuweka mbinu za kukabiliana nayo.

Iliimarisha ushirikiano na uratibu wa masuala ya Usalama na Afya Kazini na kukuza uelewa kwa waajiri katika taasisi zinazohusiana na ulinzi, elimu na bidhaa za petroli ambapo wafanyakazi 116 walielimishwa juu ya Sheria Nambari 8 ya mwaka 2005 ya Usalama na Afya Kazini ili waweze kuelewa madhara wanayoweza kuyapata na jinsi ya kukabiliana nayo katika sehemu zao za kazi.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka 2016/2017 Wizara itaendelea kutekeleza Programu ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini yenye lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usalama na Afya Kazini Nambari 8 ya mwaka 2005 na itaimarisha mfumo wa ukaguzi wa hali ya Usalama na Afya Kazini kwa kuzikagua Sehemu za Kazi 180 pamoja na kusajili Sehemu za Kazi 120. Pia, itatoa mafunzo ya usalama na afya kazini kwa Wawakilishi wa Sehemu za Kazi 120, kununua vifaa vya Usalama na Afya kazini na kuratibu masuala ya Usalama na Afya Kazini.

Mhe. Spika, Naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Thalathini na Saba, Laki Tatu na Elfu Thalathini na Tisa (Tshs. 37,339,000/=) kwa ajili ya kutekeleza Programu ndogo ya Usimamizi wa Afya na Usalama Kazini kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Maelezo kamili kuhusu Programu hii ndogo yanapatikana katika kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu *(PBB)* kwa mwaka wa fedha 2016/17 - 2018/19 kuanzia ukurasa wa Q26 hadi Q27.

Programu Kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Mhe. Spika, Programu hii inalenga kuinua hali za Wanannchi Kiuchumi kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu, kuwajengea uwezo wa kiujasiriamali na kuwaunganisha katika Vyama vya Ushirika. Matarajio ya Programu hii ni kuona kila Mzanzibari anafanya shughuli za kiuchumi ili kukidhi mahitaji ya msingi. Programu hii ina Programu ndogo tatu (3) zifuatazo:

Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Mikopo ya Uwezeshaji

Mhe. Spika, Programu hii ndogo inasimamiwa na taasisi ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na inalenga kuwapatia Wananchi wa kipato cha chini mikopo nafuu ili waweze kujiajiri katika shughuli za kiuchumi. Kwa mwaka 2015/2016, programu hii ndogo ilitekeleza yafuatayo:-

Mhe. Spika, Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi umetoa jumla ya mikopo 337 (Unguja 261 na Pemba 76) yenye thamani ya Shilingi Milioni Mia Tano Ishirini na Tatu, Laki Nne na Elfu Ishirini na Nane (Tshs.523,428,000/=), kati ya fedha hizo Unguja zimetolewa Shilingi Milioni Mia Nne na Saba, Laki Saba na Elfu Ishirini na Nane (TShs.407,728,000/=) na Pemba zimetolewa Shilingi Milioni Mia Moja na Kumi na Tano na Laki Saba (TShs.115,700,000/=). Mikopo hiyo imewanufaisha wananchi 1,907 (wanawake 1,136 na wanaume 771) katika Shehia 161 (Unguja 118 na Pemba 43) sawa na asilimia Thamanini na Saba (87) ya kilichopangwa kutolewa. (Kiambatanisho Namb. 4 kinahusika).

Mhe. Spika**,** Asilimia Thalathini na Mbili (32) ya walionufaika na mikopo hiyo ni wafanyabiashara wa maduka ya vyakula vya jumla na reja reja, nguo, viatu, mikoba, vipodozi na wafanyabiashara wanaosafiri nchi za mbali kuleta bidhaa za aina tofauti hapa Zanzibar. Wengine ni wakulima, wavuvi na wenye viwanda vidogo vidogo. Shughuli nyengine ni ufugaji, utoaji wa huduma na kazi za mikono. Asilimia Sitini na Saba (67) ya waliopatiwa mikopo ni vijana wenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 35 wakifuatiwa na wananchi wenye umri kati ya miaka 36 hadi 55 ambao wao ni asilimia 24. Asilimia 9 ya walionufaika na mikopo ni watu wazima. (Kiambatanisho Namb. 5 kinahusika).

Mhe. Spika, Mfuko kupitia programu hii ndogo imeweka dhamana ya fedha *(Guarantee Fund)* ya Shilingi Milioni Mia Moja na Hamsini (T. Shs. 150,000,000/=) katika Benki ya *CRDB* kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vijana kupitia *SACCOS* zao Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Hadi kufikia mwezi Machi 2016, *CRDB* imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Sabini na Tano, na Laki Tatu (TShs.1,075,300,000/=) ambapo Pemba walipatiwa Shilingi Milioni Mia Tatu na Kumi na Tatu na Laki Nane (TShs. 313,800,000/=) na Unguja walipatiwa Shilingi Milioni Mia saba Sitini na Moja na Laki Tano (T.Shs 761,500,000/=). Jumla ya vijana 2,326 (Unguja 1,725 na Pemba 601) wamenufaika na utaratibu huu kupitia vikundi vyao vidogo vidogo 458 (Unguja 405, Pemba 53).

Mhe. Spika, Programu imetoa mafunzo kwa wakopaji 612 (Unguja 427 na Pemba 185) (Wanawake 390 na Wanaume 222) kuhusiana na taratibu za urejeshaji wa mikopo, uwekaji wa kumbukumbu za hesabu, faida za kutumia huduma za kibenki kwa wakopaji, umuhimu wa kujiwekea akiba na utafutaji wa masoko. Lengo ni kufanya matumizi sahihi ya mikopo na kusimamia vizuri biashara zao na hatimae waweze kurejesha mikopo waliyochukua kwa wakati.

Mhe. Spika, Programu imefanya ziara za ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo katika Wilaya zote za Unguja na Pemba. Programu pia imefanya mikutano na Uongozi wa Serikali katika ngazi za Wilaya na Shehia kuwaelewesha uwepo wa Mfuko, taratibu za kuweza kupata huduma za Mfuko, pamoja na kuhimiza urejeshwaji wa fedha walizokopa kwa wakati. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2016, jumla ya Shilingi Milioni Mia Tatu Hamsini na Nane, Laki Sita na Elfu Nne (TShs. 358,604,000/=) ya fedha za mkopo zimerejeshwa Unguja na Pemba. Kiwango hiki ni wastani wa Asilimia Tisini na Tano (95) ya makadirio ya marejesho katika kipindi cha miezi kumi (10), ambapo tulikadiria kukusanya Shilingi Milioni Mia Tatu na Sabini na Tano (TShs. 375,000,000/=).

Kati ya marejesho hayo, Unguja zilikusanywa Shilingi Milioni Mia Mbili na Sabini na Saba, Laki Tatu Hamsini na Mbili na Mia Tano (Tshs. 277,352,500/=) na Pemba Shilingi Milioni Thamanini na Moja, Laki Mbili na Elfu Hamsini na Moja na Mia Tano (Tshs 81,251,500/=) (Kiambatanisho Nam 6 kinahusika)

Mhe. Spika, Programu imetunisha fedha za Mfuko wake kutokana na kuwekeza sehemu ya fedha katika Benki ya Watu wa Zanzibar. Katika mwaka huu wa fedha uliomalizika wa 2015/2016, Mfuko ulipata faida ya Shilingi Milioni Thamanini (Tshs.80,000,000/=) baada ya kuwekeza mtaji wa Shilingi Milioni Mia Nane (800,000,000/=) katika Benki ya Watu wa Zanzibar, *PBZ Ltd.* Faida hii imeongeza kiasi cha fedha wanazokopeshwa wananchi wetu ili wananchi wengi zaidi wafaidike na Mfuko huo.

Mhe. Spika, Utekelezaji wa Muongozo mpya wa utoaji wa mikopo umewahamasisha wananchi kufungua Akaunti za vikundi vyao na Akaunti zao binafsi katika Benki za Biashara. Utaratibu huu umewafanya wajasiriamali wajenge tabia ya kujiwekea akiba ambapo Shilingi Milioni Thamanini na Mbili na Laki Tano (TShs.82,500,000/=) katika Akaunti zao na baadhi yao wameshaanza kukopeshana.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Taasisi ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi kiuchumi itaendelea kutekeleza Programu ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Mikopo ya Uwezeshaji kwa kutoa mikopo 600 yenye thamani ya Shilingi Milioni Mia Sita (600,000,000); kuangalia fursa mpya za kiuchumi; kushajiisha urejeshaji wa mikopo kwa zaidi ya asilimia Tisini na Tano (95) na kuongeza kiwango cha dhamana kufikia Shilingi Milioni Mia Mbili (200,000,000/=).

Mhe. Spika, Naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Arobaini na Moja, Laki Mbili na Elfu Thalathini (Tshs.41,230,000/=) ili Programu ya Uratibu na Usimamizi wa Mfuko wa Uwezeshaji uweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka 2016/2017. Maelezo kamili kuhusu Programu hii ndogo yanapatikana katika kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu *(PBB)* kwa mwaka wa fedha 2016/17 - 2018/19 ukurasa wa Q24.

Programu Ndogo ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Mhe. Spika, Programu hii ina lengo la kupanua na kukuza Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili kukuza kipato cha Wananchi na Kuongeza ajira. Programu hii inasimamiwa na Idara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kwa mwaka 2015/2016 ilitekeleza yafuatayo:

Mhe. Spika, Programu hii ndogo imetoa mafunzo ya ujasiriamali na mabadiliko ya mtazamo kwa vijana 140 (Wanawake 90 na Wanaume 50)

kwa awamu ya kwanza kupitia kituo cha kulea na kukuza wajasiriamali kilichopo Mbweni ambacho kwa jina jengine kinaitwa *incubator*. Jumla ya vijana 639 walipatiwa mafunzo ya ujasiriamali (572 wanawake na 67 wanaume) kwa Unguja. Baada ya mafunzo hayo vijana wapatao 98 wamejiunga katika vikundi na tayari wamejisajili na wameanza kuzalisha bidhaa mbali mbali zenye ubora. Kwa upande wa Pemba programu imetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wajasiriamali 36.

Mhe. Spika, wajasiriamali waliojiunga na kituo kupitia vikundi walivyovianzisha wamesaidiwa kuanzisha kampuni 17 za majaribio, mbili (2) kati ya kampuni hizo zimeweza kupata mafanikio na kufungua Ofisi nje ya kituo na kujiajiri. Kampuni 9 tayari zimepata mafanikio lakini bado zipo kituoni zikiwa katika hatua tofauti za usajili wa biashara na bidhaa zao kwa Kampuni 6 zimeshindwa kuendeleza na mafunzo.

Mhe. Spika, Programu imewapatia mafunzo maalumu vijana 12 (wanawake 4 na wanaume 8) juu ya uandaaji wa mipango ya biashara. Baada ya mafunzo hayo vijana watatu walifanikiwa kutayarisha mipango mizuri ya biashara na walipewa zawadi ambazo ni kompyuta na kupata fursa ya kujiunga na kituo. Mmoja kati yao amefanikiwa kuanzisha kampuni yake inayojulikana kwa jina la “Karibu Zanzibar”.

Mhe. Spika, programu imefanya mafunzo ya vitendo ya teknolojia ya kukaushia matunda na mboga mboga kwa kutumia nishati ya jua kwa vijana 201 (174 wanawake na 27 wanaume).

Vile vile, programu iliendesha mafunzo ya ukarabati wa mashine na usarifu wa mazao kwa wajasiriamali wanaolelewa kituoni hapo. Pia, Programu imehamasisha wananchi katika masuala ya ujasiriamali kwa Kikundi cha Makangale Pemba na kuwapatia mafunzo ya awali ya ujasiriamali ikiwemo maana, sifa na faida za ujasiriamali.

Mhe. Spika, Programu ilifanya Mikutano 3 ya uratibu kupitia Kamati ya Usimamizi wa Kituo cha Kulelea Wajasiriamali. Mikutano hiyo iliandaa na kujadili mipango na mikakati mbali mbali ya kukikuza na kukiendeleza kituo pamoja na kuzitatua changamoto zilizopo ikiwemo kutafuta jengo jengine kwa ajili ya kutanua huduma zinazotolewa katika kituo.

Mhe. Spika, Programu imesimamia uanzishaji wa kilimo cha ‘Green House’ katika Shehia ya Chokocho na Makombeni Wilaya ya Mkoani Pemba. Mradi huu unalengo la kuwawezesha vijana 100 wanaoishi katika

maeneo hayo kupata shughuli ya uzalishaji na kuweza kujiajiri. Pia, imefanya ziara katika Hoteli za kitalii ikiwemo *Manta Reef Resort, AIYANA Resort, Misali Beach Sun Set, Fundu Lagoon* na *Emarald Bay* kutafuta soko kwa bidhaa mbali mbali za wajasiriamali. Kikundi cha Subira Huvuta Kheri cha Kiuyu Minungwini kimepata soko la kuuza bidhaa zao katika Hoteli ya *Emarald Bay* Chokocho.

Mhe. Spika, Programu imeingia katika makubaliano na ushirikiano (MoU) na taasisi ambazo zinashughulika na masuala ya kuendeleza ujasiriamali, taasisi hizo ni kama vile, *Linking African Market and Partnership (LAMP)* kwa ajili ya kusaidia upanuzi wa uendeshaji wa kituo, na Zanzibar Milele Foundation kwa ajili ya kuanzisha mfuko maalumu wa kuwasaidia wajasiriamali wanaolelewa katika kituo ili kuongeza uwezo wao wa uzalishaji na kuwapatia mkopo wa kuendeleza biashara zao. Pia kutokana na shughulli zake kupitia kituo cha kulea wajasiriamali tumeanzisha mashirikiano na taasisi za Chuo kikuu cha kilimo Morogoro SUA, Chuo cha teknolojia Arusha, Jumuia ya Wakulima wa Matunda na Mboga Mboga Tanzania (TAHA), Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo Tanzania (*SIDO*) kwa lengo la kunyanyua uwezo wa utoaji wa huduma nzuri kwa wajasiriamali wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Programu kupitia Chuo cha Kutengeneza Vifaa vya Umeme wa Jua (*Barefoot*) imetoa mafunzo kwa awamu mbili kwa wanawake 12 wa vijijini Unguja na Pemba. Vijiji vilivyobahatika kutoa wanawake ambao wameshiriki katika mafunzo hayo ya miezi mitano ni Kinyasini, Kandwi, Makunduchi, Kisiwa Panza na Matemwe. Vijiji vyengine vitakavyokua katika programu hiyo ni Fundo, Makoongwe na Ungi Msuka kwa upande wa Pemba. Unguja ni Mbuyu-tende, Bumbwini Kiongwe na Uzi Nga'mbwa.

Mhe. Spika, kupitia mafunzo waliyoyapata wanawake wahandisi niliowataja hapo juu wameweza kuunganisha umeme wa jua kwa zaidi ya nyumba 500, katika vijiji vya Kinyasini, Kandwi, Makunduchi, Kisiwa Panza na Matemwe. Pia, jumla ya taa 70 za chaji ya kutumia jua zenye ukubwa wa aina tofauti zimetengenezwa na tayari zinauzwa. Wafanyakazi wa kituo hicho wameweza kutoa taaluma ya lishe kwa mama na watoto, na mafunzo ya ujasiriamali wa kazi za mikono kwa wanawake waliokaribu na kituo na vijiji vilivyonufaika na umeme wa jua katika Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara itaendelea kutekeleza Programu ndogo ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kutoa mafunzo ya vitendo ya uzalishaji na masoko kwa wajasiriamali 300; kuendesha mafunzo ya usarifu wa mazao ya kilimo na teknolojia kwa wajasiriamali 150 Unguja na Pemba; kufanya Kongamano la wajasiriamali 300 Unguja na Pemba kwa ajili ya kusaidia upatikanaji wa masoko ya bidhaa zao; kuwasaidia wajasiriamali 50 (Pemba 15 na Unguja 35) kushiriki Maonyesho ya wajasiriamali ya Afrika Mashariki; kutoa huduma na mafunzo kwa wajasiriamali wapatao 700 kupitia Kituo cha kulelea wajasiriamali Unguja; kuanzisha kituo cha kulelea wajasiriamali Pemba na kufanya mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa kituo hicho; Kusimamia uendeshaji wa Kituo cha Kutengeneza vifaa vya umeme wa jua; kuratibu shughuli za uwezeshaji Unguja na Pemba na kuelimisha jamii kupitia vyombo vya habari.

Mhe. Spika, naliomba Baraza lako liidhinishe Jumla ya Shilingi Milioni Mia Nne na Sitini, Laki Tisa na Elfu Kumi (460,910,000/=) kwa ajili ya kutekeleza Programu ndogo ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Maelezo kamili kuhusu Programu hii ndogo yanapatikana katika kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu (PBB) kwa mwaka wa fedha 2016/17 - 2018/19 kuanzia ukurasa wa Q24.

Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika

Mhe. Spika, Programu hii ina lengo la kuimarisha mageuzi ya Vyama vya Ushirika na kuongeza ufanisi ili viweze kuchangia katika kukuza ajira na pato la taifa. Pia, ina lengo la kuwa na Vyama vya Ushirika endelevu,vyenye ubunifu na vinavyokidhi mahitaji ya wananchama wake kiuchumi na kuchangia pato la taifa. Programu hii kwa mwaka 2015/2016 ilifanikiwa kutekeleza yafuatayo:

Mhe. Spika, Programu imesajili vyama vya Ushirika 172, (Unguja 149 na Pemba 23). Kati ya hivyo 7 ni SACCOS (Unguja: 5; na Pemba: 2), 165 ni vyama vya uzalishaji na utoaji huduma. Utekelezaji huu ni sawa na asilimia 86% ya lengo la kusajili vyama 200. Jumla ya vyama vilivyosajiliwa hadi sasa ni 2,562. Baada ya usajili vyama hivi hujengewa uwezo wa kuendesha shughuli zao kwa ufanisi.

Mhe. Spika, Programu imeimarisha uwezo wa viongozi wa Vyama vya Ushirika juu ya uendeshaji na usimamizi wa vyama vyao na imetoa mafunzo kwa viongozi 1,152 (wanawake 728 na wanaume 424) Unguja na Pemba. Hii ni sawa na asilimia Hamsini na Tisa Nukta Nane (59.8%) ya lengo la kufundisha viongozi 1,925 hadi ifikapo mwezi Juni 2016. Kati ya hao, viongozi wa SACCOS walikua ni 675 na wa vyama vya uzalishaji ni 477. (Kiambatanisho namba 7 kinahusika)

Mhe. Spika, Jumla ya vyama 275 vilipatiwa mafunzo ya utunzaji wa hesabu, mbinu za Uongozi na Utawala Bora, kuandaa Bajeti na uandishi wa kumbukumbu, kati ya hivyo SACCOS ni 216 na vyama vya uzalishaji na huduma ni 59. Zoezi hili limewawezesha viongozi wa Vyama vya Ushirika kuandika vitabu vya hesabu hadi daftari la fedha. (Kiambatanisho namba 8 kinahusika)

Mhe. Spika, Programu vile vile imetoa mafunzo juu ya mabadiliko ya mitazamo, dhana, misingi na kanuni za ushirika, uimarishaji wa uwekaji akiba, haki na wajibu wa wanachama katika kusimamia na kuendesha vyama vyao kwa wanachama 6**,**588 ambayo ni sawa na asilimia Sitini na Moja (61) ya lengo la kufundisha wanachama 10,800 ifikapo mwezi Juni 2016. Mafunzo haya yameimarisha uwezo wa wanachama na watendaji kiutendaji katika vyama vyao.

Mhe. Spika, Programu imefanya ziara za ufuatiliaji na ukaguzi wa kawaida (*inspection*) kwenye Vyama vya Ushirika katika lengo la kujiridhisha juu ya kiwango cha utekelezaji wa Sheria katika uendeshaji wa Vyama vya Ushirika. Jumla ya vyama 1,321 (Unguja 691 na Pemba 630) sawa na asilimia Sitini na Sita (66) ya lengo vimefanyiwa ukaguzi wa kawaida, kati ya vyama 2,000. Kiwango cha mitaji hasa ya SACCOS kimeongezeka, kutoka Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Mbili na Ishirini, Laki Nane Elfu Sitini na Tisa na Tisini na Sita (Tzs. 6,220,869,096/-) (mwezi Julai 2015) hadi Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Sita na Kumi na Saba, Laki Mbili Elfu Thamanini na Tisa, Mia Tisa na Arobaini (Tzs: 6,617,289,940/-) (Disemba 2015). Kiwango hiki ni ukuaji wa mtaji ni asilimia Sita Nukta Nne (6.4%). (Kiambatanisho namba 9 kinahusika)

Mhe. Spika, Programu imefanya ukaguzi wa hesabu kwa Vyama vya Ushirika 116 Unguja na Pemba. Kati ya hivyo, vyama 75 vimekaguliwa na Wizara na vyama 41 vilikaguliwa na Chama cha Ushirika cha wahitimu wa vyuo vikuu (*ZYMC*). (Kiambatanisho namba 10 kinahusika)

Mhe. Spika, Programu imefanya majaribio ya uzalishaji wa mboga mboga kupitia vyama vitatu (3) vya ushirika (Unguja 2; na Pemba 1) na kuvipatia vyama hivyo vifaa vya umwagiliaji kwa njia ya matone, pembejeo zikiwemo Mbegu, mbolea na madawa pamoja na Mtaalamu mwelekezi wa kuwafundisha mbinu za kilimo cha kisasa kwa mazao ya mboga mboga.

Mhe. Spika, Programu imeimarisha upatikanaji wa Huduma za Fedha Vijijini na imetoa mafunzo kwa viongozi na wanachama wa SACCOS zote 216 za Unguja na Pemba. Pia, Idara ya Maendeleo ya Ushirika na Chama Kikuu cha Akiba na Mikopo (*ZASCU*) kimeongezewa uwezo wa utendaji kwa kupatiwa vyombo vya usafiri vikiwemo gari mbili na vespa 20, vitendea kazi vikiwemo (kompyuta, Printa, na samani za ofisi).

Mhe. Spika, Programu imeadhimisha siku ya Ushirika Duniani ambayo ni Jumamosi ya mwanzo ya mwezi wa Julai ya kila mwaka. Kwa mwaka huu Kaulimbiu ilikuwa ni "Chagua Ushirika Kupata Usawa". Wanaushirika walishiriki shughuli za kijamii zikiwemo, kufanya usafi wa mazingira, nyumba za wazee, hospitali za Wilaya, nyumba ya kulelea watoto Mazizini na kutoa misaada kwa wazee, wagonjwa na watoto.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Programu ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika imepanga kuhamasisha na kusajili vyama vya ushirika 150; kujenga uwezo wa kiutendaji wa Vyama vya Ushirika 1,760; kufanya ukaguzi wa kumbukumbu wa Vyama vya Ushirika 1,000; kusimamia udhibiti wa ndani na usimamizi katika SACCOS 216 Unguja na Pemba pamoja na kusimamia uanzishwaji wa vyama 10 vikubwa vya uzalishaji.

Mhe. Spika, Ili programu ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka 2016/17, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Ishirini na Tano na Laki Nne (Tshs.25,400,000/=). Maelezo kamili kuhusu Programu hii ndogo yanapatikana katika kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu (*PBB*) kwa mwaka wa fedha 2016/17 - 2018/19 ukurasa wa Q24.

Programu Kuu ya Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji Wanawake

Mhe. Spika, Programu inalenga kukuza Usawa wa kijinsia, kuimarisha uwezo wa Wanawake kiuchumi, kuongeza ushiriki wa wanawake katika uongozi na vyombo vya kutoa maamuzi pamoja na kutokomeza

udhalilishaji wa kijinsia. Programu hii ina programu mbili ndogo zifuatazo:

Programu ndogo ya Uratibu wa Masuala ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Uratibu wa masuala ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake inasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto na ina lengo la kuleta usawa na uwiano wa kijinsia katika maendeleo na kumwezesha mwanamke kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka 2015/2016, Programu imetekeleza yafuatayo:

Mhe. Spika, Programu imehamasisha wanawake kuanzisha na kuimarisha vikundi vya ujasiriamali na jumla ya vikundi 62 (26 Unguja na 36 Pemba) vilifanyiwa ufuatiliaji na tathmini. (Kiambatanisho namba 11 kinahusika**)**

Mhe. Spika, Wizara imeadhimisha siku ya Wanawake Duniani tarehe 8/03/2016 ambapo Ujumbe wa mwaka huu ni **"**Mwanamke ni Mwenza katika Kukuza Uchumi, Toa Fursa Sawa Wamiliki Rasilimali". Maadhimisho hayo yalijumuisha kuandaa vipindi kumi (10) vya redio na televisheni kuelimisha jamii umuhimu wa kumwezesha mwanamke kiuchumi na kupewa haki zao za msingi, kuwafariji wazee wanaoishi katika Makao ya Wazee Sebleni, Welezo na Nyumba ya Watoto Mazizini, kufanya usafi wa mazingira Unguja na Pemba pamoja na utoaji wa zawadi katika Wodi ya Wazazi. Kilele kwa Unguja kilifanyika katika Mkoa wa Mjini Magharibi na Pemba katika Uwanja wa Gombani Mkoa wa Kusini.

Mhe. Spika, Programu iliwapatia Mafunzo Wawakilishi Wanawake (UWAWAZA) juu ya kuitambua Mikataba inayohusiana na haki za wanawake na watoto, ambayo imesainiwa na kuridhiwa na Tanzania ikiwemo Mkataba wa kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW 1979), Azimio la Haki za Binadamu (1948), Mkataba wa Haki za Mtoto (CRC 1989), Mkataba wa Kuondoa Ubaguzi Katika Ajira na Kazi (1958), Azimio la Beijing 1995, ambapo nchi wanachama zimetakiwa kukuza Usawa wa Kijinsia na Ushiriki wa Wanawake katika masuala ya kisiasa. Kwa ujumla mafunzo haya yaliwasaidia Wawakilishi Wanawake kuchangia Bajeti ya mwaka 2015/2016 kwa mtazamo wa Kijinsia.

Mhe. Spika, Programu pia iliendesha na kuratibu vikao vinne vya Kikundi Kazi cha Uzingatiaji wa Masuala ya Kijinsia. Watendaji wa kikundi kazi hicho walijengewa uwezo wa uzingatiaji na uchambuzi wa masuala ya kijinsia ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi katika sekta zao. Kikundi kazi pia kilipitia Mrithi wa MKUZA II *(MKUZA Successor Strategy)* na kuhakikisha kuwa umezingatia masuala ya kijinsia.

Mhe. Spika, Programu iliendesha Longamano la Wajasiriamli Wanawake 80 ili kubadilishana mawazo na kujifunza juu ya namna bora ya kukuza ujasiriamali, kuimarisha bidhaa zao pamoja na kutatua changamoto zinazowakabili. Kongamano hilo limepelekea wajasirimali kukubaliana kuunda Mtandao wa Wajasiriamali Wanawake Zanzibar kwa lengo la kuwaunganisha na kuwa na sauti moja ya kuzishughulikia changamoto zao kwa pamoja na kuwaunganisha na fursa mbali mbali zinazojitokeza za kibiashara. Wazo hilo limefanyiwa tathmini ya kina na Wizara na hatua ya uundaji wa Mtandao huo imeanza.

Mhe. Spika, Programu imefanya tathmini ya MKUZA II kuangalia ni namna gani utekelezaji wake umezingatia jinsi ya kutoa mapendekezo ya namna gani MKUZA unaofuata unaweza kuzingatia jinsia kwa kuleta maendeleo yenye uwiano baina ya mwanamke na mwanamme. Tathmini pamoja na mambo mengine wamegunduwa kuwa hakuna uwiano katika umiliki wa rasilimali hasa ardhi, kuimarisha ushiriki wa wanawake katika ngazi zote za maamuzi, ufinyu wa upatikanaji wa ajira kwa wanawake na uhaba wa mnyambuliko wa takwimu kijinsia. Pia, timu ya wajumbe wa kuandaa Mpango wa Kitaifa wa MKUZA (*MKUZA Drafting Team*) imejengewa uwezo katika hatua zote ili kuhakikisha kuwa masuala ya kijinsia yanazingatiwa ipasavyo katika mpango huo mpya.

Mhe. Spika, Programu imefanya mikutano na waratibu wa wanawake na watoto wa Shehia za Wilaya ya Mjini, Magharibi “A”, Magharibi “B” na Kusini Unguja kujadili namna bora ya utendaji wa kazi za waratibu hao pamoja na kutoa taarifa kwa wizara juu ya maendeleo ya utekelezaji wa haki za wanawake na watoto katika shehia zao.

Mhe. Spika, Programu ya Uratibu wa Masuala ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake kwa mwaka 2016/2017 inatarajia kuhamasisha wanawake 38 kuanzisha na kuimarisha vikundi vya wajasiriamali; kuratibu shughuli za wanawake; kuwajengea uwezo wanawake 75 kushika nafasi za uongozi kwenye ngazi za Wilaya na Shehia; kuzijengea uwezo Kamati 45 za Malezi za Shehia na Kuadhimisha siku ya Wanawake Duniani.

Mhe. Spika, ili Programu ya Uratibu wa Masuala ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake iweze kutekeleza shughuli zake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya shilingi milioni Mia Moja Sabini na Nane, Laki Tisa na Elfu Tisini (178,990,000/=). Maelezo kamili kuhusu Programu hii ndogo yanapatikana katika kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu (*PBB*) kwa mwaka wa fedha 2016/17 - 2018/19 kuanzia ukurasa wa Q24 hadi Q25.

Programu Ndogo ya Mapambano Dhidi Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto

Mhe. Spika, Programu hii ina lengo la kukuza mwitiko na kuratibu mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto nchini. Programu hii inasimamiwa na Idara ya Wanawake na Watoto na kwa mwaka 2015/2016 ilitekeleza yafuatayo:-

Mhe. Spika, Programu imechukua juhudi kubwa ya kupunguza vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto katika ngazi mbali mbali, lakini bado kumekuwa na idadi kubwa ya malalamiko ambayo yanapokelewa wizarani. Jumla ya malalamiko 100 (46 Unguja na 54 Pemba) yamepokelewa. Malalamiko hayo yalihusu zaidi kutelekezwa kwa mama na watoto kulikosababishwa na kuvunjika kwa ndoa, mgawanyo wa mali walizochuma wanandoa, mimba za nje ya ndoa na kupigwa. Baada ya kupokea malalamiko, wizara inachukua jitihada ya kutoa ushauri nasaha pamoja na kuwapa rufaa walalamikaji kwa mujibu wa mahitaji yao. (Kiambatanisho Namba 12 kinahusika)

Mhe. Spika, programu imeanzisha kituo maalum cha huduma za simu kwa waathirika wa matukio ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto inayotumia namba 116. Jumla ya simu 475 zimepokelewa kwa lengo la kutoa ushauri nasaha pamoja na maelekezo kwa waathirika, kati ya hizo simu 18 zilipatiwa rufaa kunakohusika.

Mhe. Spika, programu ilifanya mkutano na wadau wa kupinga vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa wanawake na watoto katika Wilaya ya Kati Unguja ambao ulijumuisha jumla ya washiriki 80 (wanawake 52 na wanaume 28) kutoka katika Shehia 20 za Wilaya hiyo. Wadau hawa hivi sasa wanaitumia taaluma hiyo kuelimisha jamii inayowazunguka.

Mhe. Spika, programu kwa kushirikiana na Vyombo vya Habari imetoa Elimu kupitia *ZBC, Coconut, Zenji FM,* Bomba, *Hits* na Chuchu FM juu ya athari na ukatili wa udhalilishaji wa wanawake na watoto pamoja na kuhamasisha wanawake waweze kujiinua kielimu na kuunda vikundi vya kufanya shughuli za kiuchumi ikiwemo ujasiriamali. Jumla ya vipindi 180 vilirushwa hewani na jumla ya sehemu 100 "*episodes*" za mchezo wa kuigiza wa redio Mshike Mshike zimetayarishwa na kurushwa hewani kwa ajili ya kuielimisha jamii kuhusu masuala ya kupinga vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia, mimba za umri mdogo na ndoa za mapema. Pia, programu ilifanya mikutano miwili na waandishi wa habari kuwajengea uwezo juu ya kuripoti matukio ya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Mhe. Spika, programu imeandaa kutano na wadau wa kutathmini utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Kupinga Vitendo vya Udhalilishaji na Ukatili wa wanawake na watoto ili kutambua mafanikio na changamoto zinazokabili katika utekelezaji wa kampeni hiyo.

Tathmini imeonesha kuna mwamko mkubwa wa jamii wa kutoa taarifa za matukio hayo, Kamati za shehia zinafuatilia kesi na kuwashajiisha wananchi kukubali kutoa ushahidi.

Hata hivyo, harakati hizi bado zimekabiliwa na changamoto ya ucheleweshwaji wa kupata hukumu kwa kesi hizo. Takwimu za Mahakama zinaonyesha kati ya kesi 49 zilizofunguliwa kwa kipindi cha Januari hadi Oktoba, 2015 ni kesi 2 tu zilizopatiwa hukumu. Hali hii huwavunja moyo wananchi na wanaharakati wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia nchini.

Mhe. Spika, programu imetoa mafunzo ya ukufunzi kwa viongozi 39 wa dini (24 Kiislamu na 15 Kikristo) Unguja na Pemba kwa kutumia miongozo ya dini ya kupinga ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto. Viongozi hao tayari wanaifikisha taaluma hiyo kwa waumini wao kupitia mihadhara, mahubiri, madrasa na "*Sunday Schools*" pamoja na sehemu mbali mbali za mikusanyiko. Waumini wa dini ya Kikristo wameunda mtandao wa mapambano hayo Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, programu imetoa mafunzo kwa Kamati 70 za kupambana na vitendo vya Udhalilishaji na Ukatili wa Kijinsia za Wilaya na Shehia kwa Unguja na Pemba. Mafunzo haya yalitolewa kwa Kamati 10 za Wilaya, Kamati 36 za Shehia za Unguja, na Kamati 24 za Shehia za Pemba. Kwa

kupitia mafunzo haya wanakamati waliandaa mipango kazi ya mwaka na Kamati hizo zimechangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa muamko wa jamii juu ya udhibiti wa ongezeko la vitendo hivyo na kuripoti matukio.

Mhe. Spika, programu imetoa mafunzo kwa watendaji wa vyombo vya kusimamia sheria wakiwemo Mahakimu, Waendesha Mashitaka, Wapelelezi, Madawati ya Polisi ya Kijinsia na Watendaji kutoka wizara inayosimamia masuala ya wanawake na watoto ambao wanashughulikia masuala ya kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto. Jumla ya washiriki 30 walifaidika na mafunzo hayo kutoka Unguja na Pemba. Kupitia mafunzo hayo washiriki waliweza kujifunza mbinu zaidi za kuyafanyia kazi matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, sheria na miongozo iliyopo ili waweze kuielewe na kuitumia katika kazi zao hasa wakati wa kuchunguza matukio ya udhalilishaji ili ushahidi usiweze kupotea.

Mhe. Spika, programu imeadhimisha siku 16 za wanaharakati za kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto kwa kufanya kongamano la wadau 60 wa Unguja na Pemba na kutathmini utekelezaji wa masuala ya ukatili na udhalilishaji wa wanawake. Washiriki walitoa maazimio ya kiutendaji kwa kila sekta husika ambapo Tume ya Makerebisho ya Sheria imetakiwa kuharakisha mchakato wa marekebisho ya Sheria zinazosimamia kesi za Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Mahakama kuweka muda maalum wa kumalizika kwa kesi hizo ili kuwapunguzia usumbufu mashahidi.

Mhe. Spika, programu imefanya mikutano miwili ya Kamati ya Mawaziri ya kurahisisha uendeshaji wa kesi za ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto. Mikutano hiyo ilijadili mafanikio na changamoto zinazokabili uendeshaji wa kesi hizo. Imeonekana kwamba Mahakama zinachelewesha hukumu na hazitolewi hukumu stahiki kwa baadhi ya kesi zinazohukumiwa na imeshauriwa kuimarisha mashirikiano baina ya Mahkama, Polisi na Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mhe. Spika, programu ipo katika hatua ya kutayarisha mpango wa miaka 5 wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Mhe. Spika, programu hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017 itazijengea uwezo kamati 20 za kupinga vitendo vya udhalilishaji za shehia; Itaratibu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa kupambana na vitendo vya ukatili na

udhalilishaji kwa wanawake na watoto; itajenga uwezo wa wadau wanaopambana na vitendo hivi ikiwemo vyombo vya sheria; itaelimisha jamii kupitia vyombo vya habari na itafanya ufuatiliaji na tathmini.

Mhe. Spika, ili Programu ya Mapambano dhidi ya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto iweze kutekeleza shughuli zake kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya shilingi Milioni Mia Tatu Kumi na Moja na Laki Moja (311,100,000/=). Maelezo kamili kuhusu programu hii ndogo yanapatikana katika kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu (*PBB*) kwa mwaka wa fedha 2016/17 - 2018/19 ukurasa wa Q25.

Programu Kuu ya Kuimarisha Huduma za Kiustawi.

Mhe. Spika, programu hii inalenga kuimarisha mifumo ya hifadhi ya jamii, hifadhi ya mtoto na huduma kwa wananchi wanaoishi katika mazingira magumu zaidi na kuimarisha ustawi na maendeleo ya vijana nchini. Programu hii ina programu ndogo mbili kama zifuatazo:

Programu Ndogo ya Uratibu wa Huduma za Uhifadhi wa Jamii.

Mhe. Spika, programu hii ndogo ina lengo la kuimarisha mifumo ya hifadhi ya jamii na huduma kwa wazee na watoto wakiwemo watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi. Programu hii inasimamiwa na Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii. Kwa mwaka 2015/2016, programu hii imetekeleza yafuatayo:

Mhe. Spika, programu imepokea na kufanya tathmini ya maombi 26 (17 Unguja na 9 Pemba). Katika kipindi hiki, imelipa fidia ya maombi 28 yenye thamani ya Shilingi Milioni Kumi na Tisa, Laki Tisa Elfu Arobaini na Moja, Mia Tisa na Sitini na Sita (TShs.19,941,966/=) (13 Unguja yenye thamani ya 14,950,199/= na 15 Pemba yenye thamani ya 4,991,767/=). Jumla hii inajumuisha maombi 11 (Unguja 2 na Pemba 9) yenye thamani ya Shilingi Milioni Kumi na Saba, Laki Tatu Elfu Sabini na Tatu, Mia Tatu na Arubaini na Nne (Tsh.17,373,344/=) yaliyokuwa hayajalipwa katika mwaka wa fedha uliopita. Hadi kufikia mwezi Aprili mwaka 2016 kuna deni la fidia za wafanyakazi 6 kwa Unguja na 20 kwa Pemba lenye thamani ya shilingi Milioni Arobaini na Nne, Elfu Thalathini na Nne, Mia Tatu Hamsini na Tano (TShs.44,034,355/=) ambapo Unguja ni Shilingi Milioni Kumi na Saba, Laki Tisa Elfu Kumi na Nne (Tshs.17,914,410/=)

na Pemba ni Shilingi Milioni Ishirini na Sita, Laki Moja Elfu Kumi na Tisa, Mia Tisa Arobaini na Tano (Tshs.26,119,945).

Mhe. Spika, programu inaendelea kuwapatia chakula (milo mitatu) kwa siku wazee 71; (Unguja 63 na Pemba 8) wa nyumba za Wazee Welezo, Sebleni na Limbani. Wazee 57 (Wanaume 32 na Wanawake 25) wanaoishi Makundeni Pemba wanaendelea kupatiwa posho kwa ajili ya matumizi madogo madogo ya kila mwezi.

Mhe. Spika, watoto 37 wanaolelewa katika nyumba ya kulelea watoto Mazizini (Wanaume 21 na Wanawake 16) wanaendelea kupatiwa mahitaji ya chakula, mavazi, malazi, malezi, elimu na huduma za afya. Pia, watoto hupatiwa posho la Tshs. 7,000/- kila mwezi.

Mhe. Spika, programu inaendelea kuzisaidia jumla ya familia 151 (Unguja 97 na Pemba 54) zinazoishi katika mazingira magumu kwa kuwapatia posho ya Tshs 20,000/- kila mwezi kwa lengo la kuwasaidia kimaisha.

Vile vile, imeendelea kuwapatia msaada wa posho la maziwa shilingi 20,000/- kila mwezi kwa muda wa miaka 2 familia 8 (Unguja 2 na Pemba 6) zenye watoto mapacha zaidi ya wawili. Pia, programu imezika maiti 6 (3 Pemba na 3 Unguja) zisizo na jamaa.

Mhe. Spika, jumla ya malalamiko 170 (Unguja 114 na Pemba 56) yameripotiwa katika Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii. Kwa upande wa Unguja malalamiko 75 yalihusu kudai huduma za matunzo na 39 mvutano wa malezi na kwa Upande wa Pemba, matukio 34 yalihusu kudai huduma za matunzo na 22 mvutano wa malezi. Jumla ya watoto 326 (Unguja 206 na Pemba 120) wameathirika na matukio hayo kati ya hao wanaume 113 Unguja na Pemba 74 na wanawake 95 Unguja na Pemba 46.

Mhe. Spika, programu imepokea jumla ya matukio ya udhalilishaji wa watoto Elfu Moja na Kumi na Nne (1,014) kutoka Vituo vya Mkono kwa Mkono Unguja na Pemba. Pemba 139 kutoka Chake Chake, Wete na Mkoani na 875 yameripotiwa kutoka Vituo vya Mkono kwa Mkono vya Mnazi Mmoja, Kivunge na Makunduchi ambayo yaliyohusisha, kukashifiwa 355, kubakwa 497 kulawitiwa 35 na kupewa Ujauzito 127. (Kiambatanisho Namba 13 kinahusika)

Mhe. Spika, jumla ya kesi 10 zimefuatiliwa katika Mahakama ya Watoto Vuga kwa Watoto waliotenda makosa ya kulawiti, kutorosha na kubaka.

Kati ya kesi hizo, kesi 3 zimetolewa maamuzi; 1 kulipa fidia ya Tshs. 100,000/=, 2 zimefutwa kutokana na upande wa mashtaka kushindwa kukamilisha ushahidi, kesi 1 jalada limeondolewa kutokana na mshtakiwa kutohudhuria Mahakamani na 7 zinaendelea katika hatua za kusikilizwa mashahidi.

Mhe. Spika, programu ipo katika hatua ya kuandaa mfumo wa kutunza taarifa za watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi, pamoja na kuandaa makubaliano ya mashirikiano na Wizara ya Afya katika maandalizi ya mfumo huo.

Mhe. Spika, programu katika kurahisisha utekelezaji wa Sheria ya Mtoto Nam.6 ya mwaka 2011 imeandaa Kanuni za Ulinzi na Hifadhi ya Mtoto, Kanuni za Malezi ya Kambo na Kanuni za Uanzishwaji na uratibu wa nyumba za kulelea watoto na vituo vya kutwa. Hatua inayofuata ni kuziwasilisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kuhakikiwa.

Mhe. Spika, katika kuimarisha hifadhi ya mtoto katika ngazi ya Wilaya, programu imewajengea uwezo Maafisa Ustawi wa Wilaya za Kaskazini "A", Kaskazini "B" na Magharibi kwa kuwapatia mafunzo ya vitendo juu ya usimamizi wa kesi za udhalilishwaji wa watoto kwa kuzingatia Sheria ya Watoto. Jumla ya Maofisa 6 wa Ustawi wa Wilaya wameajiriwa katika Wilaya 6, (4 Unguja na 2 Pemba). Vile vile, mpango kazi wa miaka mitano wa utekelezaji wa majukumu ya hifadhi ya mtoto kwa Wilaya ya Mkoani umeandaliwa.

Mhe. Spika, programu imefanya matengenezo makubwa ya Kitengo cha Hifadhi ya Mtoto pamoja na kuwapatia Maofisa nyenzo za kufanyia kazi ili kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi wa kitengo hicho. Programu pia imetoa mafunzo ya msaada wa kisaikolojia kwa Maofisa Ustawi wa Jamii na Watendaji wa Kitengo cha Hifadhi ya Mtoto Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, programu imefanya tathmini ya Vituo vya Kulelea Watoto kwa lengo la kuangalia hali halisi ya utoaji wa huduma ya malezi katika vituo hivyo. Tathmini imebaini kuwepo kwa vituo 11 vya makaazi ya watoto vyenye jumla ya watoto 520 (423 wanaume na 97 wanawake) (Kiambatanisho Namba 14 kinahusika).

Kasoro kadhaa zimebainika zikiwemo kuingizwa kwa watoto bila ya kufuata utaratibu, mazingira ya majengo na taratibu za malezi kutoridhisha.

Katika kukabiliana na changamoto hizo programu imesitisha uingizaji wa watoto waliopo katika vituo vyote vya Zanzibar, imefanya uhakiki wa familia za watoto waliopo katika vituo hivyo na ikibainika kutokuwepo kwa sababu za msingi za watoto kuwepo katika vituo hivyo watarudishwa katika familia zao. Pia, uandaaji wa kanuni za uanzishaji wa vituo vya Makaazi unaoendelea utatoa suluhu ya changamoto hizo.

Mhe. Spika, Programu inatekeleza Mpango wa Majaribio wa Marekebisho ya Tabia kwa Watoto wanaokinzana na Sheria na walio katika hatari ya kukinzana na Sheria katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Hadi kufikia mwezi Mei, jumla ya watoto 26 wamepokelewa (Wanawake 4 na Wanaume 22). Watoto hao hupatiwa huduma mbali mbali za marekebisho ya tabia pamoja na mafunzo ya kompyuta, lugha ya kingereza, Ujasiriamali, Ufundi wa *welding*, maigizo na ushauri nasaha. Watoto hao wameonesha mabadiliko mazuri ya kitabia.

Mhe. Spika, Katika kuongeza uratibu wa shughuli za hifadhi ya jamii nchini, Programu imeendelea kufanya mikutano ya kila robo mwaka na wadau wa hifadhi ya Jamii Unguja na Pemba. Jumla ya mikutano mitatu (2 Unguja na 1 Pemba) ilifanyika. Mikutano hiyo imesaidia kuimarisha mashirikiano baina ya Wizara na wadau wa Hifadhi ya Jamii ambao ndio watekelezaji wakubwa wa Sera hiyo ya Hifadhi ya Jamii ya Zanzibar.

Mhe. Spika, Programu imeendelea na shughuli ya uundaji wa Mabaraza mapya ya Watoto ya Shehia, jumla ya Mabaraza manne (4) ya Shehia yameundwa katika Wilaya ya Mkoani na Mabaraza manne (4) yametembelewa na kupatiwa mafunzo pamoja na ushauri katika Shehia za Wara, Kichungwani, Pujini na Kangani Pemba.

Mhe. Spika, Pia, programu imeadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wazee tarehe 1 Oktoba 2015. Kilele cha Maadhimisho hayo kimefanyika Wilaya ya Kaskazini A" katika Viwanja vya Chuo cha Amali Mkokotoni. Maadhimisho hayo yaliambatana na matukio mbali mbali yaliyowashirikisha wadau na wazee wenyewe ikiwemo kufanya Mkutano na Waandishi wa Habari, Usafi wa Mazingira, kutembelea wazee na wagonjwa na matembezi ya wazee katika fukwe. Ujumbe wa mwaka huu katika maadhimisho hayo ulikuwa ni "Ushirikishwaji wa Wazee kwa Maendeleo Endelevu"

Mhe. Spika, Programu imeanza kulipa Pensheni jamii kwa Wazee wote waliosajiliwa wenye umri wa miaka 70 na kuendelea kuanzia mwezi wa

Aprili 2016. Jumla ya Wazee 21,263 (Unguja12,722 na Pemba 8,541) walitarajiwa kulipwa katika Mpango huo ambapo jumla ya Wazee 18,371 (11,019 Unguja na 7,352 Pemba) waliweza kulipwa. Kwa Mwezi wa Mei, jumla ya Wazee 22,206 walitarajiwa kulipwa, Kati ya hao Wazee 19,333 (Unguja 11,892 na Pemba 7,441) tayari wamelipwa. Mpango wa Pensheni Jamii unamlipa kila mzee aliyesajiliwa Shilingi 20,000/- kila mwezi. Kwa kuanzia malipo yamefanywa kwa njia ya fedha taslim kwa kutumia Vituo maalum.

Mhe. Spika, Mwitiko wa Wazee kwenda kupokea Mafao yao kwa mara ya kwanza ulikuwa ni asilimia 86 ya Wazee wote waliosajiliwa ambapo kwa Mwezi wa Mei ni asilimia 87 ya wazee wote. Kwa mara ya kwanza hali hii ilisababishwa na ukosefu wa taarifa, umbali wa vituo na baadhi ya wazee kufariki. Changamoto kubwa ni kuwepo kwa idadi kubwa ya wazee wenye sifa ambao bado hawajasajiliwa, hata hivyo Programu inaendelea kushirikiana na Ofisi za Wilaya kupitia Masheha kuhakikisha Wazee wote wenye sifa wanaingizwa katika Mpango huo (Kiambatanisho Namba 15a na 15b kinahusika).

Mhe. Spika, Programu ya Uratibu wa Huduma za Hifadhi ya Jamii kwa mwaka 2016/2017 italipa fidia kwa watu 14 waliopata ajali kazini; itaratibu shughuli za Malezi na Makuzi ya Mtoto; itatoa misaada ya kiustawi; itashughulikia Malalamiko ya Watoto yatayoripotiwa Wizarani; itaimarisha Mabaraza ya Watoto ya Shehia; italipa Pensheni kwa Wazee 22,000; itahudumia Wazee 120 wanaokaa katika Makao ya Wazee Unguja na Pemba; itaandaa na kutoa vitambulisho 22,000 vya Wazee wanaopokea Pensheni, itaratibu shughuli za Hifadhi ya Mtoto na Hifadhi ya Jamii; itahudumia Watoto 40 wa nyumba ya Mazizini na itaratibu uendeshaji wa Vituo 11 vya Kulea Watoto Yatima na kukamilisha uandaaji wa Kanuni za Sheria ya Watoto.

Mhe. Spika, Programu hii ndogo ya Uratibu wa Huduma za Hifadhi ya Jamii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi naliomba Baraza lako kuidhinisha kiasi cha Shilingi Bilioni Tano, Milioni Sabini na Mbili, Laki Tisa na Elfu Sitini (Tshs.5,072,960,000/-). Maelezo kamili kuhusu Programu hii ndogo yanapatikana katika kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu (PBB) kwa mwaka wa fedha 2016/17 - 2018/19 kuanzia ukurasa wa Q25 hadi Q26.

Programu ndogo ya Uratibu wa Maendeleo ya Vijana

Mhe. Spika, Programu hii ina lengo la kuratibu shughuli za Vijana ikiwemo kuimarisha ushiriki wao katika masuala ya kiuchumi na kijamii. Programu inasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Vijana na kwa mwaka 2015/2016 imetekeleza yafuatayo:

Mhe. Spika, Programu imekamilisha maandalizi ya uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2016 mnamo tarehe 18/04/2016 Mkoani Morogoro ambapo Mgeni Rasmi katika uzinduzi huo alikuwa ni Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

Mhe. Spika, Mwenge wa Uhuru kila mwaka hubeba ujumbe maalum kulingana na mahitaji ya taifa letu na dunia kwa ujumla. Ujumbe wa mwaka huu ni ‘Vijana ni Nguvu Kazi ya Taifa, Washirikishwe na Kuwezeshwa’. Pamoja na ujumbe huo wananchi wanaelimishwa na kuhamasishwa kuendelea na mapambano dhidi ya UKIMWI, Malaria, dawa za kulevya na Rushwa.

Mhe. Spika, Wizara iliadhimisha Siku ya Vijana Duniani 12/08/2015 kwa kuandaa Kongamano la Kitaifa lililowakutanisha Wawakilishi wa Vijana kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba. Kongamano hilo lilitoa fursa kwa Vijana hao kubadilishana mawazo juu ya namna ya kutumia fursa zilizopo, kukabiliana na changamoto zinazowakabili zikiwemo tatizo la ajira kwa Vijana, mimba za umri mdogo, dawa za kulevya na UKIMWI. Vijana hao waliazimia kuharakisha hatua ya kujiunga na Mabaraza ya Vijana ili kukuza ushiriki na ushirikishwaji wao katika mambo yanayowahusu.

Mhe. Spika, Mwaka 2015 ulikuwa ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu nchini kote, kwa kutambua umuhimu wa vijana katika Uchaguzi programu iliandaa maandamano, mabango na vipeperushi vilivyobeba ujumbe usemao ‘Kijana Maamuzi yako ni Muhimu Kuimarisha Amani na Maendeleo yako’ vilivyohamasisha vijana kushiriki katika hatua zote za uchaguzi kwa amani, sambamba na kuhamasisha vijana wenye sifa kujitokeza kugombea nafasi mbali mbali katika Uchaguzi Mkuu.

Mhe. Spika, Programu imeandaa Mwongozo sanifu wa Stadi za Maisha kwa Vijana walio nje ya skuli. Mwongozo huu utatumika kuwapatia mafunzo na kujenga tabia njema ili kuwaandaa kukabiliana na chanagamoto za kimaisha. Mwongozo huo umeshakamilika na tayari umeshafanyiwa majaribio. Pia, jumla ya Vijana 5,000 (3,000 Unguja na 2,000 Pemba) wamepatiwa mafunzo ya Stadi za Maisha.

Mhe. Spika, Wizara imekamilisha utayarishaji wa Kanuni za Sheria ya kuanzisha Baraza la Vijana na zimetangazwa katika Gazeti rasmi la Serikali namba 6566 la tarehe 16 Juni, 2015 na inaendelea na uhamasishaji wa vijana kujiunga kwa hiari katika Baraza hilo. Vijana waliokubali kujiunga na Baraza huorodheshwa katika Shehia zote za Unguja na Pemba. Hatua za kufanya Uchaguzi wa Viongozi wa Baraza la Vijana katika ngazi ya Shehia zinaendelea. Uchaguzi kwa Shehia zote za Wilaya ya Kati na Wete umekamilika; Wilaya zilizobakia ziko katika hatua za kukamilisha Uchaguzi katika Shehia zao. Jumla ya Shehia 166 zimekamilisha Uchaguzi wa Viongozi wao kwa Unguja na Shehia 111 zimekamilisha Pemba. Shehia 107 zilizobaki kwa Unguja na Pemba zinaendelea na hatua ya kukamilisha Uchaguzi. (Kiambatanisho Namba 16 kinahusika)

Mhe. Spika, Jumla ya vikundi 25 (Unguja 10 na 15 Pemba) vya Vijana vya kiuchumi vilifanyiwa ufuatiliaji kwa lengo la kufahamu mafanikio na changamoto zinazowakabili katika shughuli zao za uzalishaji za kila siku. Vikundi hivi viliweza kupewa ushauri wa namna ya kuimarisha shughuli zao ili zilete tija na kuzalisha kwa faida na hatimae kuongeza pato lao na la taifa.

Mhe. Spika, Programu ilifanya Kongamano la Vijana kutoka Jumuiya 18 za Vijana Pemba, kwa lengo la kubadilishana mawazo juu ya namna bora ya kuwasaidia Vijana kutatua changamoto zinazowakabili.

Mhe. Spika**,** Programu ya Uratibu wa Maendeleo ya Vijana kwa mwaka 2016/2017 itatoa mafunzo ya Stadi za Maisha kwa Vijana 330; itahamasisha na kuimarisha vikundi vya Vijana 80; itatoa mafunzo ya kuimarisha vikundi vya Vijana 20; itaratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru; itaratibu shughuli za Maendelo ya Vijana; itasimamia shughuli za kilimo cha Mboga Mboga kwa Vijana 100 Unguja na Pemba na itasimamia uanzishwaji na uendelezaji wa Baraza la Vijana.

Mhe. Spika**,** ili Programu ya Uratibu wa Maendeleo ya Vijana iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi naliomba Baraza lako kuidhinisha kiasi cha Shilingi Milioni Mia Tatu thalathini na Saba, Laki Nne na elfu Thamanini (Tshs.337,480,000/-). Maelezo kamili kuhusu Programu hii ndogo yanapatikana katika kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu (PBB) kwa mwaka wa fedha 2016/17 - 2018/19 ukurasa wa Q26.

Programu Kuu ya Uongozi na Mipango ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto

Mhe. Spika, Programu hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mipango, Sera na Programu za Wizara, kuimarisha Mashirikiano ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa pamoja na shughuli za Utafiti. Pia, inasimamia maslahi ya wafanyakazi na kuimarisha mazingira ya utendaji wa kazi. Programu hii ina programu ndogo zifuatazo:-

Programu ndogo ya Kusimamia Mipango, Sera na Tafiti za Wizara

Mhe. Spika, Programu hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia utayarishaji na utekelezaji wa Sera, Mipango, Tafiti, Programu na miradi ya Maendeleo ya Wizara, pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Wizara. Inaimarisha mashirikiano ya kisekta, kitaifa, kikanda na kimataifa pamoja na kuratibu na kusimamia utekelezaji wa masuala mtambuka ikiwemo jinsia. Programu hii kwa mwaka 2015/2016 imetekeleza yafuatayo:

Mhe. Spika, Programu imekamilisha utayarishaji wa rasimu ya Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Rasimu hiyo imejadiliwa na wadau mbali mbali wa masuala ya Uwezeshaji na kupitishwa na vikao vya kamati tendaji na Kamati ya Uongozi ya Wizara. Rasimu hiyo iko katika hatua ya kupitiwa na Kikao cha Kamati ya Makatibu Wakuu na hatimae kujadiliwa katika Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, Programu inaendelea na hatua ya kufanya mapitio ya Sera ya Mtoto ya mwaka 2001 ambapo tayari timu ya wataalamu imekusanya maoni kwa wadau mbali mbali wakiwemo watoto wenyewe Unguja na Pemba. Uandaaji wa rasimu ya Sera utakwenda sambamba na utayarishaji wa Mpango kazi wa rasimu hiyo pamoja na mpango wa ufuatiliaji na tathmini.

Mhe. Spika, Programu imeandaa Mpango wa utekelezaji wa rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar. Mpango huu unaeleza kwa kina majukumu ya kila mdau katika kutekeleza mikakati iliyomo katika rasimu hiyo na hatua za kuchukua ili malengo na matamko yaliyomo yaweze kufikiwa.

Mhe. Spika, Programu imekamilisha uandaaji wa Mpango wa utekelezaji wa Sera ya Hifadhi ya Jamii ambapo majukumu ya kila mdau

yameainishwa. Programu ipo katika hatua za mwisho za kuchapisha nakala 849 za Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2014 kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

Mhe. Spika, Programu imeendelea kuratibu miradi ya Wizara ambapo jumla ya Miradi minne ya Maendeleo na Miradi minne ya washirika wa maendeleo iliratibiwa utekelezaji wake. Miradi hiyo ni; Mradi wa Kulea na Kukuza Wajasirimali, Mradi wa Kituo cha kutengeneza vifaa vya Umeme wa Jua, Mradi wa Hifadhi ya Jamii na Mradi wa Ajira kwa vijana. Kwa upande wa Mashirika ya Maendeleo ni Mradi wa Uratibu wa Juhudi za kupinga vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Mradi wa Uimarishaji wa Mfumo wa Hifadhi ya Mtoto, Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wawanake na Mradi wa Huduma za Fedha Vijijini.

Mhe. Spika**,** Programu iliratibu uandaaji wa taarifa ya utekelezaji wa Mkutano wa 60 wa Hadhi na Haki ya Wanawake ambayo iliwasilishwa katika Tume ya kusimamia na kuratibu utekelezaji wa haki na hadhi ya wanawake nchini Marekani. Viongozi Wakuu na Watendaji walishiriki katika Mkutano huo uliofanyika mwezi Machi 2016. Mkutano ulijadili namna nchi wanachama watakavyotekeleza Malengo Endelevu ya Maendeleo (*Sustainable Development Goals*) kwa kuleta maendeleo yenye uwiano baina ya mwanamke na mwanamme. Mkutano huu ulileta chachu kwa Wizara kusimamia uingizwaji wa masuala ya jinsia katika uandaaji wa Mrithi wa MKUZA II (MKUZA *Successor Strategy*).

Mhe. Spika, Programu imewajengea uwezo Maofisa 60 (30 Unguja na 30 Pemba) wa Wizara wakiwemo Wakurugenzi katika masuala ya Ufuatiliaji na Tathmini, uandishi wa ripoti na uwekaji wa takwimu na kumbukumbu. Mafunzo ambayo yamewawezesha watendaji kutengeneza Mipango ya ufuatiliaji wa kazi zao za kila siku na za Miradi pamoja na kuandaa viashiria vya ufuatiliaji kwa mujibu wa kazi zao. Programu imefanya ziara za ufuatiliaji katika baadhi ya shughuli za Wizara Unguja na Pemba ikiwemo kituo cha kulea na kukuza wajasiriamali, Nyumba ya Wazee Sebleni na Welezo, ujenzi wa jengo la Idara ya Ushirika, Nyumba ya Watoto Mazizini na vikundi vya uzalishaji Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Programu imeratibu zoezi la kufanya tathmini ya matokeo ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kuzingatia zaidi namna gani Mfuko huo umeweza na utaendelea kuwanufaisha wanawake. Tathmini hiyo ilivishirikisha kwa asilimia 50 vikundi vyote vya wanawake

vilivyopewa Mkopo wa Mfuko wa Uwezeshaji Unguja na Pemba ambapo matokeo yameonesha kuwa asilimia 44 ya mikopo iliyotolewa kwa wanawake imetumika zaidi katika shughuli za biashara zikiwemo maduka ya jumla, biashara ndogo ndogo na biashara za kutembeza bidhaa. Vile vile, matokeo yameonyesha kuwa asilimia 35 ya wakopaji wanatumia fedha hizo kwa ufugaji wa kuku, kilimo cha mwani na mboga mboga.

Mhe. Spika, Programu imeratibu zoezi la kutathmini namna ya kuunda Mtandao wa Wajasiriamali Wanawake Zanzibar na kutoa ushauri wa namna ya kuunda mtandao huo. Kazi hiyo iko katika hatua za mwisho za kukamilika ambapo itaweka bayana namna mtandao huo utavyofanya kazi na kuleta tija. Mapendekezo ya rasimu ya Katiba ya Mtandao huo yataainisha Muundo, Uanachama na Uongozi wa Mtandao.

Mhe. Spika**,** Programu ndogo ya kusimamia Mipango, Sera na Tafiti za Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 itamalizia hatua za uandaaji wa Sera ya Uwezeshaji; Sera ya Usalama na Afya kazini na Sera ya Mtoto pamoja na mipango kazi yake; itakamilisha Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Ushirika; kumalizia Sera ya mafunzo kazini; itaratibu ufanyaji wa Tafiti za kuzitambua fursa za ajira zilizopo kwa vijana katika Sekta ya uvuvi wa bahari kuu na kilimo cha alizeti pamoja na Utafiti wa Hali halisi ya Vijana, itaimarisha mashirikiano, itaandaa Mfumo wa Ufuatiliaji na tatmini wa Wizara, itafanya ziara za ufuatiliaji na tathmini ya Shughuli za Wizara na itaratibu utekelezaji wa Programu na miradi ya Wizara.

Mhe. Spika, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Sabiini na Tano (Tshs.75,000,000/=) kwa kutekeleza Programu ndogo ya Kusimamia Mipango, Sera na Tafiti za Wizara kwa Mwaka 2016/2017. Maelezo kamili kuhusu Programu hii ndogo yanapatikana katika kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu ya (*PBB*) kwa mwaka wa fedha 2016/17 - 2018/19 ukurasa wa Q26.

Programu Ndogo ya Usimamizi wa Huduma za Utawala na Utumishi

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Usimamizi wa huduma za Utawala na Utumishi inasimamiwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji na ina lengo la kujenga mazingira mazuri ya kazi kwa kuhakikisha upatikanaji wa maslahi ya wafanyakazi, vifaa na huduma muhimu. Kwa mwaka 2015/2016 Programu ilitekeleza yafuatayo:

Mhe. Spika, Programu imehakikisha upatikanaji wa vifaa vya ofisi na huduma muhimu za kuendeshea ofisi. Imefanya matengenezo ya gari tano (5), mashine za fotokopi, kompyuta, viyoyozi na vespa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Programu imejenga uwezo wa kiutendaji kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 6 (Unguja 4 na Pemba 2), nje na ndani ya nchi. Wafanyakazi 30 (4 nje na 26 ndani ya nchi) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika fani za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Maendeleo ya Jamii, Biashara, Uchumi, Miradi, Ukatibu Muhtasi na Utunzaji kumbukumbu.

Mhe. Spika, jumla ya wafanyakazi wapya 7 (Unguja 5 na Pemba 2) wameajiriwa katika mwaka 2015/2016, kati ya hao 5 ni Wanawake na 2 ni Wanaume katika fani ya Maendeleo ya Jamii na Usarifu wa Mazao ya Chakula, Wafanyakazi sita (6) ni wa Hifadhi ya Mtoto na (1) ni kwa ajili ya Kituo cha Kulea na Kukuza Wajasiriamali (*incubation Center*) Mbweni.

Mhe. Spika, programu imerusha hewani vipindi vya redio 40 kupitia redio za *ZBC, Zenj FM, Hits FM* na *Coconut FM* na vipindi 6 kupitia *ZBC TV*, Makala 7 yalitolewa kupitia Gazeti la Zanzibar Leo na vipindi 40 vimerushwa hewani vya matukio yanayohusu programu masuala yanayosimamiwa na wizara.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi wa Mei, 2016 programu ilitakiwa kuwapatia posho la likizo la kawaida wafanyakazi 170 Unguja na Pemba ambapo wafanyakazi 100 walishapatiwa posho na 70 bado hawajalipwa. Pia, wafanyakazi (5) walistaafu kazi baada ya kufikia umri wa kufanya kazi hiyo kisheria na mfanyakazi (1) amefariki dunia.

Mhe. Spika, programu imefanya ukarabati wa jengo la Ofisi ya Idara ya Ushirika Migombani, Nyumba za Wazee Limbani Pemba pamoja na kujenga ukuta katika eneo la Nyumba za Wazee Welezo.

Mhe. Spika, programu imefanya kikao (1) cha Kamati ya Uongozi na vikao 5 vya Bodi ya Zabuni; ajenda zilijadiliwa na kuidhinishwa ikiwemo ukarabati wa Jengo la Idara ya Ushirika Migombani, jengo la wazee Limbani, Zabuni ya Ununuzi wa Vifaa vya kuendeshea ofisi; Vespa 20, Gari 2 na samani za ofisi pamoja na Zabuni ya Ujenzi wa Uzio wa Nyumba za Wazee Welezo, Unguja.

Mhe. Spika, programu imefanya ukaguzi wa ndani na ripoti ya ukaguzi wa ndani na nje zilitayarishwa. Pia, mafunzo ya kuwajengea uwezo Viongozi, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo vya Uhasibu, Ghala, Manunuzi na Maofisa wanaosimamia miradi yalifanyika ili kuweza kutekeleza kazi zao kwa ufanisi na kwa kufuata sheria za manunuzi. Vile vile, ziara za kuhakiki miradi inayosimamiwa na wizara imefanyika Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/17, programu imepanga kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 9 na ya muda mfupi kwa wafanyakazi 10 Unguja na Pemba; kutoa mafunzo ya ndani kwa wafanyakzi 13; kuandaa mpango mkakati wa rasilimali watu; kuboresha kitengo cha habari na mawasiliano cha wizara; kukamilisha Mfumo wa Serikali Mtandao wa Wizara (*E Government*); kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu kwa njia za kieletroniki; kuandaa vipindi 80 vya kuelimisha jamii, kuimarisha kitengo cha ukaguzi wa ndani; kulipa posho ya likizo kwa wafanyakazi 170 Unguja na Pemba na kununua vifaa vya ofisi.

Mhe. Spika, ili Programu ya Usimamizi wa Huduma za Utawala na Utumishi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Moja Arobaini na Tisa na Laki Tatu (Tshs.2,149,300,000/=) kwa ajili ya matumizi ya Programu na Mishahara Unguja na Pemba. Maelezo kamili kuhusu programu hii ndogo yanapatikana katika kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu ya (*PBB*) kwa mwaka wa fedha 2016/17 - 2018/19 ukurasa wa Q26.

Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba

Mhe. Spika, Programu ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba inasimamiwa na Ofisi Kuu Pemba na inaratibu utekelezaji wa programu zote za Wizara kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika, ili Programu ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Tatu Ishirini na Mbili, Laki Nane na Thamanini na Tisa Elfu (Tshs.3,322,889,000/=) kwa ajili ya matumizi ya Programu na Mishahara kwa Pemba.

Mhe. Spika, kwa maelezo kamili kuhusu Programu za Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto tafadhali angalia kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu (*PBB*) kwa mwaka wa fedha 2016/2017– 2018/2019 kuanzia ukurasa wa Q1 hadi Q32.

MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Spika, ili Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto iweze kutekeleza programu zake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2016/2017, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Moja na Nne, Laki Nne na Elfu Sitini (Tshs. 12,104,460,000/=). Kati ya hizo, Shilingi Milioni Mia Moja, Ishirini na Tisa, Laki Mbili na Elfu Moja (Tshs. 129,201,000/=) ni kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Uratibu wa Uzalishaji, Upatikanaji wa Ajira za Staha na Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria za Kazi. Shilingi Milioni Mia Tano Ishirini na Saba, Laki Tano na Elfu Arobaini (Tshs. 527,540,000/=) ni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Shilingi Milioni Mia Nne Tisini na Elfu Tisini (Tshs. 490,090,000/=) kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kukuza Usawa wa Jinsia na Uendelezaji wa Wanawake. Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Nne na Kumi, Laki Nne na Elfu Arobaini (Tshs. 5,410,440,000/=) kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kuimarisha Hifadhi ya Jamii na Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tano Arobaini na Saba, Laki Moja Elfu Thamanini na Tisa (Tshs. 5,547,189,000/-) kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uongozi na Mipango ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, wizara katika kipindi cha mwaka 2016/2017 inatarajiwa kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi Milioni Mia Nne Thamanini na Saba na Laki Nne (Tshs. 487,400,000/-) kutokana ada za usajili na ukaguzi wa vyama vya ushirika, ada ya ukaguzi wa mikataba ya ajira nje ya nchi, ada ya ukaguzi wa maeneo ya kazi na vibali vya kazi (Kiambatisho Namba 17a na 17b kinahusika).

HITIMISHO

Mhe. Spika, tunatambua na kuthamini sana michango ya Washirika wa Maendeleo katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na Programu za Wizara. Napenda nichukue nafasi hii kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi

ya Zanzibar, kuwashukuru sana washirika wetu wote wa maendeleo kwa mashirikiano waliyotupa katika utekelezaji wa majukumu yetu ikiwemo kuongeza ajira, kusimamia sheria za kazi, kupanua Programu za Uwezeshaji na Kuimarisha Ustawi, Hifadhi na Maendeleo ya Wazee, Vijana, Wanawake, Watoto na Wananchi kwa ujumla. Washirika hao ni pamoja na nchi wahisani, ikiwemo Umoja wa Ulaya, India na Jamhuri ya Watu wa China. Mashirika ya Kimataifa, ikiwemo *UNFPA, UNICEF, UN WOMEN, UNDP, UNIDO, ILO, SAVE THE CHILDREN, FHI, MIVARF, HELP AGE INTERNATIONAL, CSEMA, Measure Evaluation, VSO, REPSSI, Shell*, Tunajali Program, Benki ya Maendeleo ya Afrika pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, katika kutekeleza majukumu yake, wizara ilishirikiana na wizara na taasisi nyengine za serikali pamoja na zisizo za serikali. Napenda kuchukua fursa hii kuzishukuru taasisi hizo zote kwa mashirikiano makubwa waliyotupa na naziomba tuendelee kushirikiana kwa pamoja ili tuweze kufikia malengo tuliyopanga kwa maslahi ya wananchi na taifa letu kwa jumla.

Mhe. Spika, Natoa shukrani kwa Ofisi za Mikoa, Wilaya na Shehia, Taasisi za Dini, Vyama vya Siasa vinavyounga mkono Sera na Ilani ya CCM kwa mchango wao katika usimamizi na ufuatiliaji wa masuala yanayohusu wizara kwenye maeneo yao, ikiwa pamoja na masuala ya kupiga vita vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto, uandaaji wa Baraza la Vijana pamoja na kusaidia kufanikisha zoezi la ulipaji wa Pensheni Jamii. Pia, natoa shukrani kwa taasisi za kiraia ambazo zimechangia katika juhudi za serikali za kuimarisha Ustawi na Maendeleo ya Wazee, Wanawake, Vijana, Watoto na wanaoishi katika mazingira magumu zaidi. Taasisi hizo ni pamoja na *ZAYEDESA, COSTECH, ZAFELA, ZAWCO, ZAMWASO, ZLSC, COWPZ, PIRO, UVIKIUTA, UWAWAZA, UWT, ACTION AID, TAMWA, TMC, CUZA, ZYMC, ZAPROCO, Madrasa Resource Centre, JUMAZA, Male Network, ZIADA, SUZA, Pathfinder, Ikhlas,* na *Milele Foundation*. Shukurani zangu pia ziende kwa taasisi za kifedha, ikiwemo *PBZ* na *CRDB* kwa mashirikiano yao mazuri kwa wizara.

Mhe. Spika, vyombo vya habari vimetoa mchango mkubwa katika utekelezaji wa shughuli zetu, ikiwemo kutangaza matukio yaliyohusu wizara, pamoja na kuelimisha jamii juu ya masuala ambayo wizara inayafanyia kazi. Hivyo, nachukuwa fursa hii kuwapongeza viongozi na

watendaji wa vyombo hivyo vya habari, vikiwemo redio za serikali na za kijamii, televisheni na magazeti kwa mashirikiano yao kwa wizara.

Mhe. Spika, yote ambayo nimeyaeleza katika hotuba yangu hii yametekelezwa kwa mashirikiano makubwa baina ya Watendaji Wakuu wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto akiwemo Katibu Mkuu; Ndugu Fatma Gharib Bilal, Naibu Katibu Mkuu; Ndugu Maua Makame Rajab, Katibu Mtendaji Baraza la Vijana, Wakurugenzi, Kaimu Afisa Mdhamini Pemba na Wafanyakazi wa ngazi zote. Hivyo, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati kwa kufanya kazi kwa mashirikiano, umakini na juhudi kubwa. Mashirikiano haya yamepelekea kutekeleza malengo na majukumu yetu kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia, nawashukuru wafanyakazi wangu kwa kuonesha kubadilika katika utendaji na kuacha kufanya kazi kwa mazoea. Inawezekana nawapa mchaka mchaka, lakini nao wako sambamba na Msemo wa "HAPA KAZI TU" na ukisema tuache kufanya kazi kwa mazoea. Naamini watakuwa mfano bora kwa wenzao katika kufika mapema na kuyajali mazingira ya kazi.

Vile vile, nawaomba waendeleze umoja, mashirikiano, mshikamano, upendo na nidhamu ili tuweze kufanikisha vyema malengo yetu kwa mwaka wa fedha unaokuja na itakayofuata. **AMIN**. Bwana apewe sifa, Assalamu Alaykum, Ramadhani Kariim.

Mhe. Spika, ahsanteni sana kwa kunisikiliza, kwa kuniheshimu mimi. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho Namba 1

MCHANGANUAO WA FEDHA ZA MATUMIZI KWA MUJIBU WA PROGRAMU KUU NA PROGRAMU NDOGO 2015/2016

	PROGRAMU	KILICHOTENGWA 2015/2016	MATUMIZIHALISI JULAI 2015 – MEI 2016	ASILIMIA
1.	Q0101: Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi	669,776,000	452,233,840	67.5%
	Q010101: Uratibu na Usimamizi wa Mikopo ya Uwezeshaji	72,509,000	15,899,840	
	Q010102: Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika	41,520,000	12,761,000	
	Q010103: Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi	555,747,000	423,573,000	
2.	Q0102: Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji	300,619,000	197,368,208	66%

	wa Wanawake			
	Q010201: Uratibu wa Masuala ya Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji Wanawake	276,374,000	195,868,208	
	Q010201: Mapambano dhidi ya Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto	24,245,000	1,500,000	
3.	Q0103: Kuimarisha Huduma za Ustawi	3,007,171,000	966,504,292	32%
	Q010301: Uratibu wa Huduma za Uhifadhi wa Jamii	2,624,505,000	931,679,142	
	Q010302: Maendeleo ya Vijana	382,666,000	34,825,150	
4.	Q0104: Uongozi na Mipango ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto	3,037,534,000	2,308,416,834	76%
	Q010401: Kusimamia Mipango, Sera na	85,970,000	12,099,430	

	Utafiti za Wizara			
	Q010402: Usimamizi wa Huduma za Utawala na Utumishi	2,182,700,000	1,638,772,604	
	Q010403: Uratibu na shughuli za Wizara Pemba	768,864,000	657,544,800	
5.	Q0105: Kuratibu Uzalishaji, Upatikanaji wa Ajira za Staha na Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria za Kazi	525,064,000	353,363,600	67%
	Q010501: Ukuzaji na Upatikanaji wa Ajira za Staha	117,232,000	70,120,000	
	Q010502: Usimamizi wa Afya na Usalama Kazini	128,002,000	92,074,500	
	Q010503: Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini	279,830,000	191,169,100	

	JUMLA KWA PROGRAMU KUU	7,540,164,000	3,862,886,774	51%

Kiambatanisho Namba 2

MCHANGANUO WA MAPATO YA WIZARA 2015/2016

SN	AINA YA HUDUMA	MAPATO YALIYOKADIRIWA	MAPATO YALIYOPATIKANA	ASILIMIA
1.	ADA ZA USAJILI NA UKAGUZI WA VYAMA VYA USHIRIKA	17,600,600	7,263,000	41%
2.	ADA YA VIBALI VYA KAZI KWA WATAALAM WA KIGENI	264,387,000	254,997,000	96%
3.	ADA YA UKAGUZI WA MIKATABA YA AJIRA NJE YA NCHI	26,000,000	23,050,000	89%
4.	ADA YA UKAGUZI WA MAENEO YA KAZI	35,000,000	29,690,000	85%
	JUMLA	342,987,600	315,000,000	92%

Kiambatanisho Namba 3a

NCHI WALIZOKWENDA KUFANYA KAZI 2015/2016

JINSI	KUWAIT	OMAN	QATAR	SAUDI ARABIA	U.A.E	JUMLA
WANAUME	10	26	165	3	48	252
WANAWAKE	0	228	0	1	17	246
JUMLA	10	254	165	4	65	498

Kiambatisho Namba 3b

IDADI YA VIJANA WALIOAJIRIWA NA TAASISI BINAFSI KATKA MIKOA

MKOA	JINSIA		
	WANAWAKE	WANAUME	JUMLA
KASKAZINI UNGUJA	2,089	2,943	5,032
KUSINI UNGUJA	249	1,639	1,888
MJINI MAGHARIBI	903	1,102	2,005
KASKAZINI PEMBA	36	228	264
KUSINI PEMBA	84	269	353
JUMLA	3,361	6,181	9,542

Kiambatanisho Naamba 4

UTOAJI WA MIKOPO YA MFUKO WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI JULAI 2015 HADI APRILI 2016

WILAYA	IDADI YA MIKOPO	MIKOPO YA VIKUNDI	MIKOPO BINAFSI	SHEHIA ZILIZONUFAIKA	FEDHA ZILIZOTOLEWA	WALIONUFAIKA		JUMLA YA WALIONUFAIKA
						KE	ME	
CHAKE CHAKE	23	9	14	14	36,600,000	104	44	148
MKOANI	17	8	9	9	26,900,000	90	67	157
WETE	22	11	11	13	31,500,000	102	64	166
MICHEWENI	14	7	7	7	20,700,000	56	23	79
JUMLA NDOGO	76	35	41	43	115,700,000	352	198	550
MJINI	50	21	32	25	82,100,000	163	120	283
MAGHARIBI	50	10	45	20	99,750,000	175	107	282
KASK “A”	36	15	21	18	65,030,000	128	110	238
KAS ‘B’	50	16	34	22	62,595,000	130	95	225
KATI	25	5	20	11	48,903,000	56	50	106
KUSINI	50	13	37	22	49,350,000	132	91	223
JUMLA NDOGO	261	80	181	118	407,728,000	784	573	1,357
JUMLA KUU	337	115	222	161	523,428,000	1,136	771	1,907

Kiambatanisho Namba 5

WALIONUFAIKA NA MIKOPO YA MFUKO WA UWEZESHAJI KIUMRI NA KISEKTA

WILAYA	IDADI YA MIKOPO ILIYOTOLEWA	SHEHIA ZILIZOFIKIWA	JUMLA YA FEDHA ZILOTOLEWA	WALIONUFAIKA		JUMLA	UMRI WA WALIONUFAIKA			SEKTA ZILIZONUFAIKA						
				KE	ME		15-35	36-55	56-70	KILIMO	UVUVI	BIASHARA	VIWANDA VIDOGO	K/MIKONO	UFUGAJI	HUDUMA
CHAKE CHAKE	23	14	36,600,000	104	44	148	112	32	4	19	27	56	34	6	5	1
MKOANI	17	9	26,900,000	90	67	157	103	42	12	10	52	62	13	7	9	4
WETE	22	13	31,500,000	102	64	166	138	24	4	26	34	71	14	9	5	7

MICHEWENI	14	7	20,700,000	56	23	79	43	27	9	22	23	15	3	3	4	9
JUMLA NDOGO	76	43	115,700,000	352	198	550	396	125	29	77	136	204	64	52	23	21
MJINI	50	25	82,100,000	163	120	283	187	84	12	27	32	107	62	8	15	32
MAGHARIBI	50	20	99,750,000	175	107	282	132	49	101	35	21	104	59	13	18	32
KAS ‘A’	36	18	65,030,000	128	110	238	174	51	13	50	38	71	14	23	39	3
KAS’B’	50	22	62,595,000	130	95	225	154	64	7	31	36	67	23	17	42	9
KATI	25	11	48,903,000	56	50	106	65	38	3	35	9	18	13	8	17	6
KUSINI	50	22	49,350,000	132	91	223	169	46	8	85	31	52	8	12	31	4
JUMLA NDOGO	261	118	407,728,000	784	573	1,357	881	332	144	263	167	419	179	81	162	86
JUMLA KUU	337	161	523,428,000	1,136	771	1,907	1,277	457	173	340	303	623	243	106	185	107

Kiambatanisho Namba 6

MAREJESHO YA MIKOPO MFUKO WA UWEZESHAJI KUANZIA JULAI 2015 HADI APRILI 2016

WILAYA	Julai 2015	Agosti 2015	Sept. 2015	Oktoba 2015	Novemba 2015	Disemba 2015	Januari 2016	Februari 2016	Machi 2016	Aprili 2016	JUMLA
CHAKE	2,256,500	2,478,000	2,014,000	2,404,500	1,953,000	1,709,000	2,258,000	2,628,000	3,790,500	2,551,00	24,042,500
MKOANI	1,492,000	2,107,000	2,406,000	872,000	1,807,000	4,257,000	1,566,000	1,880,000	1,027,500	1,660,000	19,074,500
WETE	2,406,000	2,937,000	2,435,000	1,240,000	1,775,000	1,734,000	1,284,000	2,736,000	2,623,500	1,737,000	20,907,500
M/WENI	1,711,000	1,607,000	3,352,000	967,000	1,903,500	1,600,500	1,655,000	1,570,000	1,366,000	1,495,000	17,227,000
JUMLANDOGO	7,865,500	9,129,000	10,207,000	5,483,500	7,438,500	9,300,500	6,763,000	8,814,000	8,807,500	7,443,000	81,251,500
MJINI	9,167,000	6,554,000	9,190,000	3,599,000	5,855,000	9,805,000	8,164,000	6,247,000	5,672,500	4,664,000	68,917,500
MAGHARIBI	9,209,000	9,542,000	7,847,000	5,986,000	13,781,000	10,831,000	5,163,000	10,027,000	6,384,000	10,478,000	89,248,000
KASKI ''A''	4,211,000	4,617,000	2,892,000	1,689,000	3,314,000	3,684,000	3,530,000	4,108,500	3,692,500	1,710,000	33,448,000
KASKI ''B''	4,100,000	4,371,000	3,153,000	1,786,000	4,942,000	2,084,000	3,317,500	3,520,000	2,442,000	2,282,000	31,996,500
KATI	2,180,000	2,140,000	3,382,000	1,410,000	4,144,000	1,754,000	3,367,000	3,460,000	2,981,000	4,629,000	29,447,000
KUSINI	952,000	2,321,000	1,861,500	1,681,000	2,540,000	1,521,000	2,672,000	5,006,000	1,750,000	3,991,000	24,285,500
JUMLANDOGO	29,819,000	29,545,000	28,325,500	16,151,000	34,576,000	29,679,000	26,213,500	32,368,500	22,921,000	27,754,000	277,352,500
JUMLAKUU	37,684,500	38,674,000	38,532,500	21,634,500	42,014,500	38,979,500	32,976,500	41,182,500	31,728,500	35,197,000	358,604,000

Kiambatanisho Namba 7

VIONGOZI WA VYAMA VYA USHIRIKA WALIOPATIWA MAFUNZO JULAI-MACHI 2016

S N		Washiriki		Jumla
		W'ke	W'me	
1	Uzalishaji na Huduma	324	153	477
2	SACCOS	404	271	675
	Jumla	728	424	1,152

Kiambatanisho Namba 8

VYAMA VILIVYOPATIWA MAFUNZO KI-WILAYA

SN	Wilaya	SACCOS	Uzalishaji & Huduma	Jumla
1	Mjini	41	6	47
2	Magharibi A	9	5	14
3	Magharibi B	16	7	23
4	Kaskazini A	21	9	30
5	Kaskazini B	17	4	21
6	Kati	15	7	22
7	Kusini	6	3	9
8	Chake Chake	36	6	42
9	Mkoani	19	5	24
10	Wete	25	4	29
11	Micheweni	11	3	14
	Jumla	216	59	275

Kiambatanisho Namba 9

UKUAJI WA MITAJI YA SACCOS JULAI-DISEMBA 2015

MWEZI	UNGUJA	PEMBA	JUMLA	Ukuaji mtaji
Julai 2015	4,751,871,300	1,468,997,796	6,220,869,096	6.4%
Disemba 2015	5,032,519,245	1,584,779,695	6617,298,940	

Kiambatanisho Namba 10

UKAGUZI WA HESABU 2015/2016

SN	UNGUJA	PEMBA	ZYMC	Jumla
	42	33	41	116

Kiambatanisho Namba 11

VIKUNDI VYA UJASIRIAMALI VYA WANAWAKE VILIVYOFANYIWA UFUATILIAJI UNGUJA NA PEMBA

S/N	JINA LA KIKUNDI	SHUGHULI	SHEHIA
1.	Tupendane	Kilimo cha migomba	Wesha
2.	Bidii na maarifa	Kilimo cha mboga mboga	Ndagoni
3.	Juhudi huleta maendeleo	Ufumaji	Wara
4.	Inshalla Salama	Kilimo cha mboga mboga	Ndagoni
5.	Vumilia	Kazi za mikono	Wara
6.	Penye nia	Kazi za mkono	Mvumoni
7.	Nia safi	Ushoni	Madungu
8.	Baada ya dhiki	Ufugaji wa kuku	Wesha
9.	Kipapo Liquid Soap	Utengenezaji wa sabuni	Kipapo
10.	Tuwenao	Kazi za mikono	Chanjaani

MKOANI

S/N	JINA LA KIKUNDI	SHUGHULI	SHEHIA
11.	Umoja wetu	Kilimo cha tangazawizi	Mtambile
12.	Nguvu mali	Kilimo cha mboga mboga	Mjimbini
13.	Faragani	Saccos	Mbuguani
14.	Uwama	Utengenezaji sabuni	N'gombeni
15.	Maendeleo	Kilimo cha mihogo na migomba	Kiwani
16.	Tutumie Wakati	Kilimo cha mpunga na kazi za mikono	Makombeni
17.	Nia njema	Kilimo cha mchicha	Mbuyuni
18.	Jitegemee	Uuzaji wa mafuta ya chikichi	Ukutini
19.	Jumbamwe	Ushonaji	Mapinduzi
20.	Maendeleo	Kilimo cha mchicha	Jondeni

WETE

S/N	JINA LA KIKUNDI	SHUGHULI	SHEHIA
21.	Mshike mshike	Vitalu	Kizimbani
22.	Fahari	Vipodozi	Selemu
23.	Tuvumiliane	Dawa asili	Kipangani
24.	Pemba Clove Honeny	Asali	Mtemani
25.	Mkipimiliki	Utengenezaji sabuni	Machengwe
26.	Juhudi ni nguvu	Kilimo cha miti na ufugaji wa kuku wa kisasa	Kisiwani
27.	Mwanzo mgumu	SACCOS	Kinyikani
28.	Subira yavuta heri	Kushona mikoba	Kiuyu

MICHEWENI

S/N	JINA LA KIKUNDI	SHUGHULI	SHEHIA
29.	Tubadilike Kiuchumi	Tea Masala	Kinyasini
30.	Tudumishe Amani	Kilimo cha njugu na halizeti	Makangale
31.	Nia njema Hairogwi	Kilimo cha mboga mboga	Majenzi
32.	Tupendane	Utengenezaji wa viatu	Kiungoni
34.	Sibahatishi	Kilimo cha mboga mboga na Utengenezaji sabuni.	Mjini Wingwi
35.	Tujaaliye	Kilimo cha miti	Konde
36.	Zao nia	SACCOS	Maziwa Ng'ombe

MJINI

S/N	JINA LA KIKUNDI	SHUGHULI	SHEHIA
1.	UWAMI	Ufugaji kuku na Kufuma	Migombani
2.	Tujinasue	Biashara ndogo ndogo	Sebleni
3.	Tujiwezeshe	Kukopeshana bidhaa	Sebleni
4.	Tusifarakiane Kinamama	Kutengeneza maua kwa kutumia Karatasi ngumu	Muembe Shauri
5.	Kwahani Cooperation	Kukopeshana bidhaa	Kwahani
6.	Amani na Utulivu	Kutengeneza achari	Chumbuni
7.	Hamtuwezi kwa kazi zetu	Kutengeneza bidhaa kwa kutumia ukindu	Urusi
8.	Tushikamane	Kulima Mboga Mboga	Migombani

MAGHARIBI

S/N	JINA LA KIKUNDI	SHUGHULI	SHEHIA
9.	Mwenye kusubiri hachoki	Ufumaji na Ushoni	Mtopepo
10.	Busara	Kutengeneza mapambo ya Ofisini na nyumbani	Mtofaani
11.	Tuamkeni	Kilimo cha Mboga Mboga	Kianga
12.	Kitunze kidumu	Mafuta ya Nazi ya Viungo, Ushoni, ufumaji na upishi wa vyakula vikavu	Pangawe
13.	Umoja ni Nguvu	Biashara Ndogo Ndogo	Mwanakwerekwe
14.	Busara	Upikaji Sabuni na Kutengeneza Madomet	Mtofaani

KATI

S/N	JINA LA KIKUNDI	SHUGHULI	SHEHIA
15.	Saccos ya wadi ya uzini	Kilimo	Tunduni
16.	Mtarazaki hana haya	Kilimo(pilipili boga na vitunguu maji)	U/Ukuu Kaebona
17.	Tunamuomba Mungu	Kilimo cha tungule	Umbuji
18.	Nia njema hairogwi	Kilimo cha mboga mboga	Mpapa

KUSINI

S/N	JINA LA KIKUNDI	SHUGHULI	SHEHIA
19.	Mzozo mwiko	Kilimo na Ufumaji madomet	Makunduchi
20.	Hatusumbuani	Ufinyanzi	Kitogani

KASKAZINI “A”

S/N	JINA LA KIKUNDI	SHUGHULI	SHEHIA
21.	Vijana Group	Ushoni wa nguo	Moga
22.	Tupendane	Ufugaji wa kuku	Mcheza shauri
23.	Ugalipo	Ufugaji wa ngombe wa maziwa na kuku	Mcheza shauri

KASKAZINI “B”

S/N	JINA LA KIKUNDI	SHUGHULI	SHEHIA
24.	Ukulima wa muhogo	Kilimo cha muhogo	Kiombamvua
25	Mkorofi si mwenzetu	Kilimo cha migomba	Upenja
26.	Ususi endelevu	Kilimo cha halizeti, muhogo, mpunga na utengenezaji wa sabuni	Pangeni

Kiambatanisho Namba 12

MALALAMIKO YA UDHALILISHAJI WA WANAWAKE YALIYORIPOTIWA WIZARANI 2015/2016

UNGUJA

SN	AINA YA LALAMIKO	WILAYA							JUMLA	HATUA ZILIZOFIKIWA
		MJINI	MAGH ‘A’	MAGH ‘B’	KASK ‘A’	KASK ‘B’	KATI	KUSINI		
1.	Madai ya mahari	1	1						2	Zipo Mahkama ya Kadhi
2.	Talaka				28				28	Wameshauriwa kwenda

										ZAFELA
3.	Kutelekezwa na Mume			1			1		2	1. Ameshauriwa kwenda Idara ya Ustawi Wilaya ya Kinondoni. 2. Mahkama ya Kadhi
4.	Matunzo ya Ujauzito	1						1	2	Imepatiwa Suluhu
5.	Kupigwa	1	1	5					7	Zimepelekwa dawati la Jinsia
6.	Madai ya Mirathi		1						1	Ameshauriwa kwenda Ofisi ya waqfu na mali ya Amana
7.	Madai ya Mali baada ya kuachana		1	3					4	Wameshauriwa kwenda ZAFELA
	JUMLA	3	4	9	28		1	1	46	

PEMBA

WILAYA	KUPIGWA	KUTELEKEZWA	MGOGORO WA NDOA	MADAI YA MIRATHI	KUTISHIA AMANI	KUIBIWA KARAFUU	MADAI YA MAHARI	MIMBA	SHAMBULIOLA AIBU	MADAI BAADA YA KUACHWA
CHAKE CHAKE	1	6	9	3	-		2			1
MKOANI	-		3	-	-		3			
WETE	-		7	-	1		2			1
MICHEWENI	1		1	-	-		1			
JUMLA	2		20	3	1		8			2

Kiambatanisho Namba 13

MATUKIO YA UDHALILISHAJI WATOTO YALIYORIPOTIWA KATIKA VITUO VYA MKONO KWA MKONO UNGUJA NA PEMBA; JULAI 2015 - APRILI, 2016

UNGUJA

KITUO	KUKASHIFIWA	KUBAKWA	KULAWITIWA	UJAUZITO	JUMLA
HOSPITALI YA M/MOJA	284	369	15	90	758
KIVUNGE	17	51	11	12	91
MAKUNDUCHI	6	13	3	4	26
JUMLA	307	433	29	106	875

PEMBA

KITUO	KUKASHIFIWA	KUBAKWA	KULAWITIWA	UJAUZITO	JUMLA
CHAKE CHAKE	23	25	1	7	56
MICHEWENI	8	17	3	5	33
WETE	17	22	2	9	50
JUMLA	48	64	6	21	139

Kiambatanisho Nambari 14

MUHTASARI WA WATOTO WANAOLELEWA KATIKA VITUO VYA KULELEA WATOTO ZANZIBAR - 2016

JINA LA KITUO	ME	KE	JUMLA	ME 0-1	ME 2-5	ME 6-7	ME 8-12	ME 13+	KE 0-1	KE 2-5	KE 6-7	KE 8-12	KE 13+	%	NDUGU	% NDUGU
Alfa Nurania Pemba	15	2	17			1	4	10			2			3.27	2	1.92
African Muslim Pemba	118	0	118			6	97	15						22.69	10	9.62
Fysabilillah Markaz - U	9	12	21			1	3	5		1	1	7	3	4.04		0.00
Islah	12	5	17			2	3	7			1	3	1	3.27	8	7.69
Istiqama	8	0	8				8							1.54	2	1.92
Markaz Lyakin	35	0	35				14	21						6.73	15	14.4

																2
Mazizini IUJ	11	15	26	1	1		6	3	2			7	6	5.00	12	11.54
Montesory	18	17	35		3	7	4	4		5	8	2	2	6.73	8	7.69
Omar Bin Khatwab	44	0	44	0	0	0	7	37	0	0	0	0	0	8.46		0.00
SOS Children's Village	103	46	149	1	2	7	16	77	0	9	1	8	37	28.65	39	37.50
African Muslim - Unguja	50	0	50		0	9	23	18						9.62	8	7.69
Jumla	423	97	520	2	6	33	185	197	2	6	13	27	49	100	104	100
Asilimia Kiumri	81.35	18.65	100	0.38	1.15	6.35	35.58	37.88	0.38	1.15	2.50	5.19	9.42		20	

Kiambatanisho Namba 15a

MUHTASARI WA IDADI YA WAZEE WALIOLIPWA PENSHENI JAMII KWA MWEZI WA APRILI 2016

WILAYA	WALIOTAKIWA KULIPWA	WALIOLIPWA	WASIOLIPWA	ASILIMIA YA WALIOLIPWA
MAGHARIBI A	891	676	215	75.87%
MAGHARIBI B	1,021	780	241	76.40%
MJINI	2,696	2,012	684	74.63%
KATI	1,607	1,475	132	91.79%
KUSINI	1,276	1,211	65	94.91%
KASKAZINI A	3,577	3,287	290	91.89%
KASKAZINI B	1,654	1,578	76	95.41%
JUMLA UNGUJA	12,722	11,019	1,703	86.61%

MKOANI	2,323	2,010	313	86.53%
CHAK CHAKE	2,333	2,005	328	85.94%
WETE	2,403	2,066	337	85.98%
MICHEW ENI	1,482	1,271	211	85.76%
JUMLA PEMBA	8,541	7,352	1,189	86.08%
JUMLA KUU	21,263	18,371	2,892	86.40%

Kiambatanisho Namba 15b

MUHTASARI WA IDADI YA WAZEE WALIOLIPWA PENSHENI JAMII KWA MWEZI WA MEI 2016

WILAYA	IDADI YA WAZEE	IDADI YA WALIOLIPWA	WASIOLIPWA	% YA WALIOLIPWA
MAGHARIBI "A"	1,044	734	310	70.31%
MAGHARIBI "B"	1,090	823	267	75.50%
MJINI	3,035	2,261	774	74.50%
KUSINI	1,320	1,265	55	95.83%
KATI	1,730	1,591	139	91.97%
KASKAZIINI "A"	3,620	3,452	168	95.36%
KASKAZINI "B"	1,890	1,766	124	93.44%
JUMLA UNGUJA	13,729	11,892	1,837	86.62%
MKOANI	2302	2138	164	92.88%
CHAKE CHAKE	2314	2071	243	89.50%
WETE	2390	2014	376	84.27%
MICHEWENI	1471	1218	253	82.80%
JUMLA PEMBA	8477	7441	1036	87.78%
JUMLA KUU	22,206	19,333	2873	87.06%

Kiambatanisho Namba 16

IDADI YA MABARAZA YA VIJANA YA SHEHIA KIWILAYA ZANZIBAR

UNGUJA

SN	WILAYA	IDADI YA SHEHIA	SHEHIA ZILIZOFANYA UCHAGUZI	SHEHIA ZISIZOFANYA UCHAGUZI
1.	KATI	42	42	0
2.	MAGHARIBI ‘A’	31	27	4
3.	MAGHARIBI ‘B’	34	25	9
4.	KUSINI	22	0	22
5.	KASKAZINI ‘A’	44	40	4
6.	KASKAZINI ‘B’	31	0	31
7.	MJINI	49	32	17
	JUMLA	253	166	97

PEMBA

SN	WILAYA	IDADI YA SHEHIA	SHEHIA ZILIZOFANYA UCHAGUZI	SHEHIA ZISIZOFANYA UCHAGUZI
1.	CHAKE CHAKE	31	29	2
2.	MICHEWENI	22	18	4
3.	WETE	36	36	0
4.	MKOANI	32	28	4
	JUMLA	121	111	10

Kiambatanisho Namba 17a

MUHTASARI WA MAKADIRIO YA FEDHA KWA PROGRAMU KUU NA NDOGO KWA MWAKA 2016/2017

	PROGRAMU	MAKADIRIO 2016/2016
1.	Q0101: Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi	527,504,000
	Q010101: Uratibu na Usimamizi wa Mikopo ya Uwezeshaji	41,230,000
	Q010102: Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika	25,400,000
	Q010103: Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi	460,910,000
2.	Q0102: Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji wa Wanawake	490,090,000
	Q010201: Uratibu wa Masuala ya Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji Wanawake	178,990,000
	Q010201: Mapambano dhidi ya Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto	311,100,000
3.	Q0103: Kuimarisha Huduma za Ustawi	5,410,440,000
	Q010301: Uratibu wa Huduma za Uhifadhi wa Jamii	5,072,960,000
	Q010302: Maendeleo ya Vijana	337,480,000
4.	Q0104: Uongozi na Mipango ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto	5,547,189,000
	Q010401: Kusimamia Mipango, Sera na Utafiti za Wizara	75,000,000
	Q010402: Usimamizi wa Huduma za Utawala na Utumishi	2,149,300,000
	Q010403: Uratibu na shughuli za Wizara Pemba	3,322,889,000
5.	Q0105: Kuratibu Uzalishaji, Upatikanaji wa Ajira za Staha na Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria za Kazi	129,201,000
	Q010501: Ukuzaji na Upatikanaji wa Ajira za Staha	29,512,000
	Q010502: Usimamizi wa Afya na Usalama Kazini	37,339,000
	Q010503: Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini	62,350,000
	JUMLA KWA PROGRAMU KUU	12,104,460,000

Kiambatanisho Namba 17b

MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO YA WIZARA KWA MWAKA 2016/2017

SN	AINA YA HUDUMA	MAPATO YALIYOKADIRIWA
1.	ADA YA MAFUNZO	11,975,000
2.	ADA ZA USAJILI WA VYAMA VYA USHIRIKA	14,370,000
3.	ADA YA UKAGUZI WA VYAMA VYA USHIRIKA	17,963,000
4.	ADA YA UKODISHAJI WA UKUMBI	9,580,000
5.	ADA YA UKAGUZI WA MIKATABA YA AJIRA NJE YA NCHI	41,913,000
2.	ADA YA VIBALI VYA KAZI KWA WATAALAM WA KIGENI	323,340,000
3.	MALIPO YA UKAGUZI KATIKA SEHEMU ZA KAZI	20,358,000
4.	ADA YA UKAGUZI WA MAENEO YA KAZI	47,901,000
	JUMLA	487,400,000

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wako. Waheshimiwa Wajumbe kinachofuata nitamuita Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ili aje awasilishe hotuba yake. Baada ya hapo itaanza kuchangiwa hiyo hotuba. *(Makofi)*

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)(Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Spika, ahsante sana. awali ya yote kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake kubwa ambayo kaisoma karibu masaa mawili. Kwa hivyo, nampongeza kwa hatua hiyo na *In sha Allah* na mimi niko nyuma yake nitasoma kwa muda mfupi ufuatao.

Mhe. Spika, hii ni Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa ukarimu wake wa kutupa uhai, afya njema na nguvu, tukaweza kukutana tena katika chombo hichi muhimu katika nchi yetu kwa lengo la kuwawakilisha wananchi wa Zanzibar. Kutokana na kuelewa umuhimu wa vitu hivi nasema *ALHAMDULILLAH*.

Mhe. Spika, baada ya shukurani na pongezi, sasa naomba kwa ruhusa yako niingie katika maudhui. Samahani Mheshimiwa.

Vile vile, napenda kuendeleza ukarimu wa kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyengine katika kufanikisha kazi hii, ambayo natarajia kuiwasilisha kwenu katika muda mfupi ujao. Lakini kabla sijafanya kazi hiyo kwa niaba ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari, naomba niwatambue kwa majina.

Kwanza kabisa nawashukuru na kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Kijitoupele kwa kuniamini na kunipa ridhaa ya kuwatumikia nikiwa kama Mwakilishi wao katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Nawaahidi nitawapatia utumishi uliotukuka na nitawatumikia kwa nguvu zangu zote. Lakini pia, kwa heshima kubwa nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kuniteua mimi kuwa Mjumbe wa Kamati hii na hatimaye kupata nafasi ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii.

Mhe. Spika, baada ya shukrani na pongezi, sasa naomba kwa ruhusa yako niingie katika maudhui ya taarifa hii, kwa kuwa kazi ya Kamati ya kufanya Mapitio ya Makadirio ya Wizara kabla hayajapitishwa na Baraza zima la Wawakilishi, ni kazi ya kikanuni, hivyo kuna haja ya msingi ya kuhakikisha kwamba inafanywa kwa kufuata taratibu zote zilizowekwa na Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Naomba nilihakikishie Baraza hili tukufu kwamba kazi tumeifanya kwa umakini mkubwa na kwa uadilifu wa hali ya juu, ingawa Mhe. Spika, kulikuwa na changamoto kubwa ya muda ulikuwa mdogo.

Mhe. Spika, katika suala la muda ambalo limekwenda sambamba na upya wa Kamati, kwa kuwa sote tunaelewa kwamba, mambo yamekwenda kwa haraka sana, hivyo Kamati hazikupata fursa ya kuzikagua wizara na taasisi zake ili kuweza kujiridhisha na utendaji wao wa kazi kabla ya kuidhinisha matumizi mapya ya mwaka unaokuja.

Vile vile, Kamati hazikupata muda wa kujiridhisha ni kwa kiasi gani Bajeti ya Mwaka unaomalizika (2015/2016), ilifanyiwa kazi ipasavyo, hali iliyopelekea Kamati kudhani kwamba mambo yalikwenda sawa kama yalivyopangwa lakini ukweli utabakia kwa watendaji wa wizara hizo.

Mhe. Spika, nia na madhumuni ya kutaja changamoto hii ni kutaka kuwafanya Wajumbe wa Baraza hili waelewe kwamba, Kamati pamoja na upya wake na muda kuwa mdogo, lakini imefanya kazi yake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ni miongoni mwa wizara muhimu katika nchi yetu, kwa kuwa ndio wizara inayoisimamia jamii nzima, kuanzia kwa mama zetu, watoto wetu, vijana wetu na wazee wetu. Kwa lugha nzuri tunaweza kusema hii ndio "**WIZARA MLEZI au ULEZI KAZI**".

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti, kumradhi naomba nimpishe Mwenyekiti wa Baraza ili aendelee na hiki kikao ili nami niweze kuendelea na shughuli nyengine ofisini. Mhe. Mwenyekiti karibu sana.

Hapa Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alikalia kiti

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)(Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii na Uwezeshaji): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti,

Vile vile, Wizara hii ndiyo inayosimamia maswala muhimu ya ajira zetu nchini, pamoja na kuwawezesha wananchi kuishi katika maisha bora na yenye hadhi.

Hata hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kutoa masikitiko ya Kamati kwa Serikali. Licha ya ukweli kwamba Wizara hii ndiyo inayosimamia jamii nzima, nikiwemo mimi na wewe

Mhe. Mwenyekiti, lakini bajeti inayotengwa kwa wizara hii ni ndogo sana. Hali inayopelekea kuwa na changamoto zisizokwisha. Zaidi ya hilo, pia uingizwaji wa fedha zilizotengwa kwa mwaka, nao pia hauridhishi hata kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kulifafanua suala hili, katika Mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ilipangiwa kutumia Shilingi 7,015,100,000 kati ya hizo 5,351,700,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na 1,663,400,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo hadi kufikia mwezi Mei, 2016 wakati Kamati inakutana na Wizara kujadili Makadirio ya mwaka 2016/2017 ni jumla ya shilingi 3,223,401,120 sawa na asilimia 46% tu ya makadirio yote ndizo zilizopatikana.

Mhe. Mwenyekiti, katika hali kama hii, Kamati inajiuliza suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi litawezekana vipi? Maswala kama ya mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, gharama za kuwalipa wazee, gharama za kuwasaidia watoto na wanawake dhidi ya vitendo vya udhalilishaji, ikiwemo kufuatilia kesi hizo sehemu mbali mbali za nchi yetu, uwezeshaji wa vijana ili waweze kupata nguvu za kujiendeleza kiuchumi kwa kuwapatia vitendea kazi vitakavyowawezesha kujiajiri wenyewe, na mengineyo, yote yanahitaji kuwa na fedha za kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo basi, naomba nitoe ombi maalum kwa Serikali, kuitazama wizara hii, kwa jicho la huruma na kuipa kipaumbele wakati wa kutenga fedha kwa ajili ya uendeshaji wa Wizara za Serikali, kwa kuwa hapa ndipo wananchi hasa walipo. Sisi sote tunao watoto, vijana na wanawake katika majumba yetu, na wote wanahitaji kuendelezwa, lakini pia, sisi sote itafika wakati tutakuwa Wazee na tutahitaji Wizara hii itusaidie kuendesha maisha yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa tathmini ya Wizara hii, sasa nijielekeze katika kujadili mambo mbali mbali yaliyojitokeza wakati wa majadiliano ya mapendekezo ya Makadirio ya Matumizi na makusanyo ya Mwaka 2016/2017, yaliyofanyika baina ya Kamati na Wizara hii. Baadhi ya mambo hayo ni kama ifuatavyo:

VIPAUMBELE VYA WIZARA

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu ya Wizara ili kufikia malengo iliyojiwekea kwa mwaka, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto imejiwekea vipaumbele vyake, ambavyo ndivyo vitakavyoiwezesha kuweza kutumia rasilimali zake kwa mipango itakayokuwa imara na yenye kufikia malengo. Vipaumbele hivyo vitaiwezesha Wizara kuweza kuzigawa rasilimali walizonazo, katika kutekeleza mambo muhimu kwanza kabla ya mengine ambayo yatakuwa na umuhimu mdogo kwa wakati husika.

Mhe. Mwenyekiti, wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017, imejiwekea vipaumbele kumi (10), kwa ruhusa yako. Mhe. Mwenyekiti, naomba nivitaje baadhi ya hivyo; Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Ajira kwa Vijana, Kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Mipango inayohusu wazee, vijana, wanawake na Watoto, kupanua programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi, kuimarisha mfumo wa uratibu na usimamizi wa programu za hifadhi ya wazee, kusimamia mageuzi ya mfumo wa ushirika na kuimarisha uwezo wa vyama vya ushirika katika uzalishaji na utoaji wa huduma n.k.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inapongeza suala zima la kuwa na vipaumbele vya Wizara, kwa kuwa ni njia pekee ya kuiwezesha kufikia malengo kwa urahisi na kuwa na ufanisi wa kuendesha mambo yao. Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo, maoni ya Kamati ni kuwa vipaumbele kumi ni vingi sana, na tunaishauri Wizara ijiwekee vipaumbele kidogo ambavyo itakuwa rahisi kuvifanyia kazi kwa kutumia rasilimali ndogo iliyopo.

Katika kutekeleza hili, Kamati inaishauri Wizara kuchagua mambo ya msingi ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi kwa haraka, ili kuyawekea kipaumbele. Kwa mfano suala zima la udhalilishaji wa Wanawake na watoto, kwa kujiwekea mkakati wa makusudi wa kutafuta suluhisho la matatizo hayo, kwa kuwa na sheria ya Kuzuia udhalilishaji, kupendekeza marekebisho ya Sheria za sasa n.k

SUALA LA AJIRA

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo liliibua Mjadala wakati wa Kikao cha Kamati na Wizara ni suala la Ajira nchini. Kwa kuwa ajira ni jambo la msingi

na ni haki ya kila mwananchi kwa mujibu wa Katiba ya nchi, Kamati ilitaka kujua hali ikoje kwa sasa. Ni dhahiri kwamba, hii ni changamoto kubwa inayoikabili Serikali yetu, hasa ukizingatia kwamba idadi ya vijana wanaomaliza masomo katika vyuo mbali mbali nchini inaongezeka siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, kuna haja ya lazima kwa Serikali kufanya utaratibu wa makusudi wa kuandaa programu maalum ambazo zitawawezesha vijana kuweza kujiajiri wenyewe. Kwa mfano, Serikali, inaweza kuandaa programu zinazohusiana na maswala ya uvuvi, kilimo, uzalishaji wa bidhaa za viwandani n.k. Hata hivyo, hili halitaweza kufanikiwa ikiwa Serikali haitoweka utaratibu maalum wa kuwapatia vijana mafunzo maalum, vitendea kazi, mashine na mitaji ya kuendesha shughuli hizo. Suala hili linaweza kufanyika hata kwa njia ya mikopo yenye masharti nafuu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, Kamati iliutaka uongozi wa Wizara kupitia Idara ya Kazi, kulisimamia kwa umakini na kwa karibu suala zima la ajira za Mahoteli ya Kitalii. Ni dhahiri kwamba, sote tunaelewa kwamba kumekuwa na malalamiko mengi na yasiyokwisha katika Hoteli mbali mbali kuhusiana na ajira wanazopatiwa vijana wetu. Suala la Mikataba ya Ajira limekuwa ni tatizo sugu ambalo linahitaji kufuatiliwa kwa karibu. Katika kulitatua suala hili Kamati imeitaka Wizara kuandaa vipindi vya Redio, TV na kutoa matangazo katika Magazeti, kwa lengo la kuwaelimisha wananchi suala la Mikataba mbali mbali ya ajira, ili kuepusha mivutano isiyokuwa ya lazima katika sehemu za kazi.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Usalama katika sehemu za kazi pia ni suala muhimu katika kuhakikisha usalama wa wafanyakazi wakati wote wanapokuwa kazini. Hata hivyo, inaonekana muamko na uelewa wa wafanyakazi walio wengi kuhusu suala hili ni mdogo sana. Kamati inaiomba Wizara katika kukuza uelewa wa wananchi waandae utaratibu maalum wa kupita katika maeneo mbali mbali ya kazi, ili kuwapatia elimu wafanyakazi, lakini pia vipindi vya Redio na TV vinaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kwa yale maeneo ambayo vinaweza kusikika.

Kamati pia, inaiomba Serikali kuharakisha taratibu za kuandaa sera ya maswala ya usalama kazini, ambayo kwa sasa ipo katika ngazi ya Makatibu Wakuu. Tunaamini kwamba, sera hii itaweka mikakati madhubuti ya kuwalinda wafanyakazi wetu kwa lengo la kuweza kuongeza uzalishaji. Hata hivyo, Ili kuwa na Sera iliyokusanya maoni ya makundi mbali mbali ya Wananchi, tunaiomba Serikali kuwashirikisha wahusika wa kila sekta, ikiwemo na

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika hatua mbali mbali za uandaaji wa Sera hiyo, kwa ajili ya kupata maoni yao.

Mhe. Mwenyekiti, kamati pia inaiomba Serikali kuanzisha utaratibu wa kuwawekea bima maalum ya kazi wafanyakazi wake, ili kuweza kuwasaidia wakati wanapopatwa na majanga sehemu za kazi.

KUKUA KWA VITENDO VYA UDHALILISHAJI NA CHANGAMOTO YA KISHERIA

Mhe. Mwenyekiti, vitendo vya udhalilishaji wa watoto na wanawake vinavyofanywa na watu mbali mbali vimekuwa vikiongezeka kwa kasi sana. Jamii imekuwa ikishuhudia kukua kwa vitendo hivi siku hadi siku. Kutokana na ukweli huo, lawama nyingi zimekuwa zikielekezwa kwa Serikali kwamba inashindwa kusimamia ipasavyo suala hili lakini pia lawama zinaelekezwa kwa muhimili wa Mahakama kwamba kesi zinazowasilishwa Mahakamani hazitolewi hukumu ipasavyo.

Kamati kwa kuliona hili, imeona ipo haja ya kujadiliana kwa kina na Wizara husika, ambapo iligundulika kwamba changamoto zinazolikabili tatizo hili ni nyingi, zikiwemo uelewa wa jamii kuhusu maswala ya kisheria na uendeshaji wa kesi, changamoto ya kuwapata mashahidi, lakini kubwa zaidi ni Changamoto ya uwepo wa Sheria inayohusiana moja kwa moja na maswala ya Udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyema ikafahamika kwamba, kwa sasa, maswala ya udhalilishaji yanapojitokeza yanasimamiwa na Sheria mbali mbali zikiwemo; Sheria ya Makosa ya Jinai - Penal Act Namba 6, 2004, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai *Criminal Procedure Act* Namba 7, 2004, Sheria ya Ushahidi Sura ya 5 *Evidence Act CAP 5* n.k.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ikiwa kama msimamizi mkuu wa maswala ya udhalilishaji wa wanawake na watoto haina mamlaka juu ya utekelezaji wa Sheria zote hizi tatu, na badala yake usimamizi wa Sheria hizi uko katika Taasisi tofauti zikiwemo Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, ambayo ipo chini ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma, Jeshi la Polisi ambalo lipo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani, hali inayopelekea kuleta ugumu kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto katika kusimamia utekelezaji wa sheria hizi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pamoja na Wizara imeona ni vyema, ikatungwa Sheria mpya ambayo itakusanya kwa pamoja utaratibu mzima wa kushughulikia maswala ya udhalilishaji ambayo utekelezaji wake utakuwa chini ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Kamati imeshauri Wizara kwa kufuata taratibu zilizopo Serikalini, kuandaa Rasimu ya Sheria hiyo ili iweze kujadiliwa na hatimaye kupitishwa na Baraza la Wawakilishi.

Hata hivyo, Kamati pia inaishauri Wizara kufanya utafiti wa kina utakaowezesha kukusanya kwa pamoja, maeneo yote ya kisheria ambayo yanaonekana yanaleta ugumu katika kushughulikia suala zima la kupunguza vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na kusababisha ucheleweshaji wa kesi hizo. Maeneo hayo kwa pamoja yawasilishwe kwa Tume ya Kurekebisha Sheria kwa lengo la kufanyiwa kufanyiwa mapitio upya ya Sheria husika.
Sheria ya Ushahidi Sura ya 5 *Evidence Act CAP 5*

Mhe. Mwenyekiti, kwa umuhimu wa pekee naomba nizungumzie suala hili. Mhe. Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba, Sheria hii ina nafasi kubwa sana katika utaratibu mzima wa kuendesha kesi za jinai. Hata hivyo, kutokana na ukweli kwamba Sheria hii ni ya muda mrefu, bila ya shaka itakuwa imepitwa na wakati. Mhe. Mwenyekiti, Baraza lako tukufu litakumbuka kwamba siku ya tarehe 27/05/2016 Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, alikiri ndani ya Baraza hili wakati alipokuwa akitoa majibu ya nyongeza kwa swali lililoulizwa kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwamba sheria hii imepitwa na wakati. Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba ninukuu maneno ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kama ifuatavyo:

> "…ni vyema kwanza Waheshimiwa Wajumbe wakatambua Sheria ya Ushahidi ambayo inaongoza sasa hivi ni ya mwaka 1917, mwakani inatimia umri wa miaka mia moja. Kwa hiyo, kuna mambo mengi ambayo yametokea katikati hapa ambayo inabidi sheria ile sasa ifanyiwe mabadiliko…."

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyojuwa"hakuna hukumu bila ya ushahidi", hivyo, tujiulize Mahakama zetu zinawezaje kufikia hatua ya kutenda haki ikiwa Sheria inayotumiwa imepitwa na wakati kiasi hiki? Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaamini kwamba wakati umefika wakati kuwa na Sheria ya Ushahidi inayoendana na mazingira ya nchi yetu na maendeleo ya teknolojia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali inalijuwa suala hili na tayari Sheria hii imeanza kufanyiwa mapitio muda mrefu sasa, Kamati inaitaka Serikali

kuwasilisha Mswada wa Marekebisho ya Sheria hii katika Mkutano wa tatu wa Baraza la Tisa la Wawakilishi kwa ajili ya kusomwa kwa mara ya kwanza.

Kwa kufanya hivi, tunaweza kusaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa matatizo ya udhalilishaji nchini.

MAJENGO YA WIZARA

Afisi Kuu Unguja

Mhe. Mwenyekiti, wizara inakabiliwa na Changamoto ya maeneo ya kufanyia kazi, ambapo jengo la Wizara ni finyu sana. Vyumba vya Ofisi ni kidogo, hali inayopelekea watendaji kutumia ofisi za jumla na kupata usumbufu wakati wa kutekeleza majukumu yao.

Afi kuu Pemba

Mhe. Mwenyekiti, changamoto ya Jengo la Ofisi kwa upande wa Pemba ni kubwa, ambapo zaidi ya miaka mitano sasa Wizara inatumia jengo la kukodi. Jengo linalotumika ni jengo la Benki ya *NMB* ya zamani ambalo Wizara imekodi kwa gharama ya 22,200,000 kwa mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, fedha hizi ni nyingi sana, ambapo kwa miaka mitano Wizara inatumia zaidi ya milioni 100 kwa ajili ya kodi ya jengo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa tayari Wizara imeshapatiwa kiwanja cha ujenzi wa Ofisi katika maeneo ya Gombani Pemba, na tayari tenda ya kumtafuta mkandarasi ilishatoka, Kamati inaiomba Wizara ya Fedha na Mipango ambayo ndiyo inayosimamia ujenzi huo, kufanya jitihada za makusudi kuanza ujenzi haraka iwezekanavyo, ili kupunguza gharama za kukodi majengo kwa fedha nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, sote tunaelewa kwamba miradi karibu yote ya Serikali inasimamiwa na Wizara ya fedha jambo ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa kucheleweshe miradi ya maendeleo. Kamati yangu inajiuliza hii Wizara ya Fedha na Mipango ina watumishi kiasi gani kuweza kusimamia kila mradi ukiachilia ile miradi mikubwa ya kitaifa, mpaka hii miradi ya ujenzi inayosimamiwa na wizara husika.

Kutokana na hali hiyo, Kamati yangu inaishauri serikali kwa hii miradi midogo iliyomo kwenye Wizara moja moja ni vyema ikasimamiwa na taasisi husika ili kuifanya iende kwa haraka na iweze kumalizwa kwa wakati. Kinyume na hivyo

ikiwa tabia hii ya miradi yote kuwa inasimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango maana yake tunachagua kwenda kwa mwendo wa pole kitu ambacho kwa sasa kimepitwa na wakati.

Jengo la Wazee - Limbani

Mhe. Mwenyekiti, hili ni jengo la wazee wanaohudumikiwa na Serikali, lililopo Limbani - Pemba, ambapo kwa sasa linafanyiwa ukarabati na wazee hao wamehamishiwa sehemu nyengine kutokana na ubovu iliyokuwa nao. Kwa taarifa ilizozipata Kamati kutoka kwa uongozi wa wizara kwamba, jengo limeshafanyiwa ukarabati kwa asilimia kubwa, limeshawekwa plasta, limeezekwa upya, limeshawekwa milango na madirisha, bado choo na banda la kupikia. Hivyo basi, Kamati inaitaka wizara kuhakikisha kwamba ujenzi huo unamalizika haraka iwezekanavyo na kuwarejesha wazee kuendelea kuishi katika maeneo yaliyo salama kwa afya zao.

Mahakama ya Watoto - PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, kama inavyoeleweka kwamba katika kuhakikisha kwamba haki na usalama wa watoto unalindwa katika ngazi zote za kitaifa na kimataifa, kumekuwa na haja ya makusudi ya kuanzisha Mahakama za Watoto ambazo zitawawezesha watoto kupata haki zao kiurahisi na kujihisi wapo katika mikono salama.

Kwa upande wa Unguja, Mahakama ya watoto imeshaanzishwa na inaendelea na kazi zake, hata hivyo, kwa upande wa Pemba, jengo ambalo lilitarajiwa kuwa ni sehemu ya Mahakama kama hiyo, bado linafanyiwa matengenezo, halijakamilika. Kwa kuwa, vifaa vya kuanzisha Mahakama hiyo vipo, Maafisa wameshapatiwa mafunzo husika, tunaiomba Serikali kupitia uongozi wa Mahakama Pemba, kufanya haraka ya kulikamilisha jengo hilo, ili shughuli za kuendesha kesi za watoto ziendelee kama ilivyo kwa Upande wa Unguja.

Kwa kuwa, kukosekana kwa jengo hilo, kunapelekea kesi za watoto kusikilizwa katika Mahakama za kawaida, jambo ambalo linaonekana kuongeza hofu ya watoto wakati wa kuendesha kesi hizo hali inayopelekea kukosekana kwa haki za watoto wengi.

PENCHENI YA JAMII

Mhe. Mwenyekiti, Hii ni aina ya mafao ambayo anatakiwa kupata kila mtu kama ni haki ya msingi pindi anapofikia umri wa miaka 70 na kuendelea.

Wazee ambao watakuwa na sifa hiyo, wanatakiwa kupata malipo ambayo yatawasidia kujikimu na maisha yao ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, imeamua kuanzisha utaratibu wa kutoa aina hii ya pencheni kwa wananchi wake. Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Serikali, pamoja na kutoa tahadhari ifuatayo;

Mhe. Mwenyekiti, Utaratibu wa sasa wa kuwatambua wazee waliofikia umri uliotajwa hapo juu, ni kwa kutumia vielelezo mbali mbali kama vyeti vya kuzaliwa, vitambulisho vya kusafiria, kwa kutaja matukio mbali mbali yaliyotokea hapo zamani n.k, Kamati inaishauri Wizara kuwa na usimamizi mzuri katika suala hili, ili kuhakikisha kwamba hakuna mtu anayestahiki kupata pensheni hii ambaye ataachwa bila ya kuorodheshwa. Na vile vile, usajili wa wazee hawa uwe unafanyiwa mapitio angalau kila baada ya miezi sita ili kuepusha kuja kuwa na Wazee hewa, hasa ukizingatia kwamba utaratibu wa kupokea fedha kwa sasa unaweza kufanywa kwa kupitia wadhamini wa wazee husika. Hivyo basi, kuna uwezekano mkubwa Mzee akawa ameshafariki, lakini mdhamini wake akawa anaendelea kupokea fedha hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia inapenda kutoa tahadhari kuhusu suala la ugawaji fedha, kwamba uendelee kufanywa na Maafisa wa Wizara ili kuepusha udanganyifu. Suala la vituo vya ugawaji wa fedha ambavyo kwa sasa vipo 47 kwa Unguja na Pemba, Kamati inashauri idadi hiyo iongezeke, kulingana na ongezeko la usajili wa Wazee.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia, inaitaka Wizara kutoa elimu kwa Wananchi kuhusiana na suala hili la pencheni ya jamii, ambalo linaonekana ni jipya na ambalo limezua maswali mengi sana miongoni mwa jamii yetu. Kupitia elimu hiyo wananchi watapata uelewa na pia itapunguza malalamiko ya wananchi.

SUALA LA KUWAWEZESHA WANANCHI

Mhe. Mwenyekiti, Katika suala hili, Serikali kupitia Wizara hii, imejiwekea mikakati mbali mbali ikiwemo kuwapatia wananchi mikopo nafuu, kuanzisha vituo vya kuwalea wajasiriamali (ambapo wajasiriamali husajiliwa na kupatiwa mafunzo mbali mbali kama ya usarifu wa matunda, maziwa, jinsi ya kutengeneza bidhaa kama sabuni n.k), pia kuwapatia vifaa vya kazi mfano mashine za kazi. Vile vile, Wizara imeanzisha Kituo cha *Barefoot*, ambapo mafunzo ya kutumia vifaa vya umeme wa jua yanatolewa kwa akina mama ambao wanatoka maeneo ambayo yanatumia umeme wa jua, baada ya kumaliza

mafunzo hayo, akinamama hao wanapatiwa nyenzo za kutengenezea kwa lengo la kujiajiri kama mafundi wa umeme panapotokezea hitilafu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapongeza hatua zilizofikiwa na Wizara katika kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuweza kujikwamua na umaskini. Hata hivyo, Kamati inaitaka Wizara kuwa na utaratibu maalum wa kufuatilia na kuhakikisha kwamba, mafunzo pamoja na vifaa vinavyotolewa kwa wahitimu vinatumika kwa ajili ya kuleta tija na kufikia malengo ya kuondoa umaskini.

Mhe. Mwenyekiti, Ni jukumu la Wizara, kufuatilia kwa ukaribu, wale wote wanaopata mikopo ili kuhakikisha mikopo hiyo haitumiki kinyume na makusudio, lakini pia kuhakikisha inazalishiwa na hatimaye inalipwa, ili kuiwezesha miradi hii iwe endelevu.

Kwa upande wa wahitimu wa ujasiriamali, Wizara iwe na utaratibu wa kuajiri Watu maalum, kwa mfano, kuwaajiri wanafunzi ambao wanamaliza vyuo vikuu katika fani ya Biashara, ambao watatumika kuwasimamia na kuwaelekeza wajasiriamali waliomaliza mafunzo yao, ili kuweza kuendeleza biashara zao na hatimaye kuweza kuzalisha kwa faida. Wasimamizi hawa pia watawasaidia wajasiriamali hao, wakati wanapokwama na kuonekana kukata tamaa ya kwenda mbele.

BAJETI YA WIZARA 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti, Kwa ujumla Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto imepangiwa kukusanya jumla ya shilingi 487,400,000 (Mia nne na thamanini na saba milioni na laki nne)kwa mwaka 2016/2017, mapato ambayo yatakusanywa kupitia vyanzo mbali mbali vya Wizara, kwa mfano ada ya ukaguzi wa maeneo ya kazi, ada ya uandikishaji vyama vya ushirika, ada ya ukaguzi wa Mikataba ya Ajira nje ya nchi, n.k. Kamati inaliomba Baraza hili tukufu kuidhinisha makusanyo hayo na inatoa wito kwa Wizara kuweza kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kujiongezea makusanyo, lakini pia kuwa na mbinu madhubuti za kuzuia uvujaji wa mapato katika sehemu za makusanyo. Miongoni mwa mbinu hizo ni kufanya malipo kwa njia ya benki, badala ya kupokea kwa mikono.

Vile vile, Wizara inaomba kuidhinishiwa matumizi ya shilingi 12,104,460,000 (Kumi na mbili bilioni, mia moja na nne milioni, laki nne na sitini elfu)kwa mwaka 2016/2017**,** ambapo kwa upande wa matumizi mengineyo ya Wizara (*OC*) ni shilingi 8,097,500,000 (Bilioni nane, tisini na saba milioni na laki tano)ni matumizi ya kazi za kawaida, (kati ya hizo bilioni 6.5 kwa ajili ya

pencheni ya wazee na bilioni 1.5 kwa ajili ya matumizi ya Wizara), na shilingi 2,241,000,000 (Bilioni mbili na mia mbili arobaini na moja milioni) ni kwa ajili ya mishahara, maposho maalum na Mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Na kwa upande wa kazi za Maendeleo ni jumla ya shilingi, 1,065,960,000 (Bilioni moja, sitini na tano milioni, laki tisa na sitini elfu)ambazo zimepangwa kutolewa na washirika wa maendeleo na shilingi 700,000,000 (Milioni mia saba) ni mchango wa SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaliomba Baraza kuidhinisha matumizi ya fedha hizo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Hata hivyo, Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaomba kutoa masikitiko yake kwa Serikali kupitia Wizara ya Fedha, kwamba kwa tathmini ya Kamati iliyoifanya ni kwamba zaidi ya asilimia 60% ya bajeti hii ya Wizara ni mishahara na maposho. Vile vile, fedha za maendeleo, ambazo ni mchango wa SMZ ni kidogo sana, milioni 700 tu. Hivyo basi, kupitia Baraza hili tukufu nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, kwamba hicho kidogo ambacho Wizara imepangiwa kupata, basi ni nyema wakaingiziwa kwa wakati ili waweze kutekeleza malengo waliyojiwekea. Lakini pia kwa mwaka wa fedha 2017/2018, tunaiomba Serikali kuongeza zaidi ukomo wa bajeti ya Wizara hii ili iweze kuwa na bajeti inayoiwezesha kutekeleza kazi zake ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii inasimamia utekelezaji wa Programu kuu tano, ambazo ni Programu Kuu ya Q0101 (uwezeshaji Wananchi Kiuchumi), Programu Kuu Q0102 (kukuza usawa wa Kijinsia na uendelezaji wanawake), Programu Kuu Q0103 (kuimarisha huduma za Ustawi), Programu Kuu Q0104 (Uongozi na Mipango ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto) na Programu Kuu Q0105 (Kuratibu Uzalishaji, Upatikanaji wa Ajira za Staha na Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria), na kila programu Kuu ina programu zake ndogo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipitisha Makadirio kwa Programu hizi zote pamoja na programu zake ndogo, hata hivyo kulikuwa na makosa ya uandishi katika Programu Kuu ya tano (Q0105), ambayo ilitakiwa kuwa na programu ndogo tatu, lakini badala yake katika mswada wa makadirio ulioletwa na Wizara ya Fedha na Mipango, ilionekana kuwa na Programu ndogo 1. Hata hivyo, baada ya kupata ufafanuzi kutoka kwa Wizara husika na Afisa bajeti kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Kamati ilijiridhisha kuwa program ndogo za Programu Kuu ya Tano ni tatu, na fedha zake ni kama ifuatavyo:

Programu Kuu QO105 Uratibu wa uzalishaji, Upatikanaji wa Ajira za Staha na usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria za kazi. Jumla ya Programu kuu ni shilingi 129,201,000 badala ya 28,877,000 kama inavyoonekana katika mswada wa makadirio. Pia, Programu hii ina program ndogo tatu ambazo ni:

1. Q010501: Ukuzaji na upatikanaji wa Ajira za Staha, jumla ya shilingi 29,512,000
2. Q010502: Usimamizi wa Viwango vya kazi vya Kimataifa na majadiliano ya pamoja, jumla ya silingi 37,339,000

3. Q010503: Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini, jumla ya shilingi 62,350,000

Mhe. Mwenyekiti, Mwisho kabisa naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa mashirikiano yao mazuri waliyonipa kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kazi hii. kwa ruhusa yako naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	- Mwenyekiti
2.	Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma	- Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Asha Abdalla Mussa	- Mjumbe
4.	Mhe. Maryam Thani Juma	- Mjumbe
5.	Mhe. Zaina Abdalla Salum	- Mjumbe
6.	Mhe. Hassan Khamis Hafidh	- Mjumbe
7.	Mhe. Jaku Hashim Ayoub	- Mjumbe
8.	Mhe. Mussa Foum Mussa	- Mjumbe
9.	Mhe. Suleiman Makame Ali	- Mjumbe
10.	Ndg. Latifa Saleh Suleiman	- Katibu; na
11.	Ndg. Makame Salim Ali	- Katibu

Nimalizie kwa kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza kwa umakini na kwa utulivu mkubwa, pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii, kwa mashirikiano yao.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema, kwa niaba ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari naunga mkono hoja hii ya Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha lakini pia nakuomba kwa ruhusa yako unigawie dakika mbili tatu nichangie kama Mwakilishi ninayatumikia jimbo la wananchi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, sasa ninaingia katika nafasi ya Uwakilishi wa Jimbo langu la Kijitoupele. Niseme tu kwamba ninamshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika mambo mbali mbali kwa kutoa kauli yake nzuri juu ya ufugaji wa ng'ombe katika maeneo yetu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kuwa nimeguswa na Wilaya ya Magharibi "A" na "B", nitazungumzia kadhia ya Wilaya hizi mbili juu ya matatizo yaliyojitokeza katika nchi yetu. Mhe. Rais imani yake kubwa kwa wananchi wake hataki kuwadhalilisha, wala hana nia ya kuwasumbua katika maisha yao. Ndiyo maana ikaundwa wizara maalum (Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na mambo mengineyo. Na katika Mkoa wetu wa Mjin/Magharibi, Wilaya ya Magharibi "A" na Magharibi "B" wenzetu kwa asilimia 80 kazi yao ni ufugaji na kilimo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, bahati mbaya hii taarifa ninajua itafika lakini nilifikiri Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais yupo, lakini wametoka nje kwa bahati mbaya, ninaiomba serikali kwa dhati kabisa. Ng'ombe Wilaya ya Mjini naunga mkono wasiwepo. Ninaunga kwa asilimia mia moja na sababu ninazo. Tumetembea katika miji mbali mbali kwenye nchi za wenzetu ng'ombe huwakuti wakatembea ovyo mjini na kuhatarisha usalama wa wanaotembea katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Kwa kuwa Wilaya zetu mbili hizi; kuna Wilaya ya Magharibi "A" na "B". Magharibi "A" imeanzia Mfenesini mpaka Mwakaje, Kizimbani, mpaka Fuoni, *no* mpaka Mwera. Na Wilaya ya Magharibi "B" imeanzia Fumba unakuja zako mpaka Kijitoupele, Kwarara mpaka unafika Mwanakwerekwe na kwengineko. Hii ni Wilaya ya "B" na "A", lakini asili tokea asili ya mwanzo wenzetu hawa ni wakulima na wafugaji. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, sababu ya kusema hapa hii ni Wizara ya Kazi, Vijana, Wanawake, Watoto na Wazee, kwa asilimia 80 vijana wetu wanataka ajira. Sisemi ng'ombe waruhusiwe kuchukua mchanga ninapinga kwa asilimia mia moja, sisemi ng'ombe wale wakafanye kazi za magendo ambayo hayatakiwi. Lakini ng'ombe wale wanasaidia jamii kutokana na mambo mbali mbali, vikundi vya ushirika vimo humu vina ng'ombe wao Fuoni, Mwanakwerekwe,

Kwarara, Kijitoupele na kwengineko. Ng'ombe hawa wamehifadhiwa kwa usalama na salimini hawana tatizo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri husika na kuiomba serikali kwa ujumla. Kauli ya Mhe. Rais ni nzuri, lakini tuliochukua madaraka tumekwenda nje ya utaratibu. Kwa makusudi ninaiomba serikali leo na sizuii bajeti ya wizara hii, sina mamlaka hayo kwa sababu mimi ni mwenyekti lakini nitakuwa na ushauri wa kutosha. Kwa sababu akinamama wamejiajiri, akinababa wamejiajiri na vijana wote wamejiajiri na hasa ukizingatia. Hivi sasa kuna Kiwanda cha Maziwa cha Bakheressa asilimia 80 ya maziwa yanategemewa kwa wakulima wa nchi hii hii. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, leo unasema tu kwamba kwa kuwa Manispaa zimekatwa mpya. Mimi ninazipongeza zimekatwa mpya Magharibi "A" na "B", lakini hazina hadhi. Maji hakuna, barabara za ndani mbovu, umeme huko tunakosema Kwarara Madina kila siku hakuna. Bado hatujafikia lengo la kuwazuia wafugaji wetu wasifuge ng'ombe wao huko katika maeneo yao. Ningefurahi angekuwepo Mhe. Haji Omar Kheir hapa na Waziri wa Nchi wa (OR) Makamu wa Pili wa Rais ambaye ni mtendaji mkuu wa Serikali. Mhe. Mwenyekiti, tusifanye masikhara, tumefika hapa kwa ajili ya wananchi wetu na wananchi wanatutegemea kwa asilimia mia moja tutawasemea mia moja tutawasemea matatizo yao. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina uchungu na machozi yatanitoka, kwa sababu asilimia 80 ni wafugaji, hawakeri kwenda kuchukua mchanga wala kitu gani. Wanalofanya wao ni kutafuta riski yao, wanauza maziwa yao, mifugo yao ikiwa mikubwa wanauza ng'ombe wao. Leo ng'ombe wale wanaambiwa katika maeneo ya Mkoa mzima wa Mjini/Magharibi hawatakiwi. Hilo ni kosa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi sote tuungane. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum SMZ aje hapa atueleze suala hili, bado linatuathiri na linaathiri wananchi wetu mitaani, hali mbaya sana. Mimi ninasema haya sina ng'ombe hata mmoja ninayefunga lakini na ng'ombe wananchi wetu wa jumla ya Zanzibar hii, ng'ombe imo katika bajeti Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kasoma bajeti yake. Wizara ya Kazi anawategemea hawa hawa. Hawa vijana wanaojiari akinamama pia wamejikusanya wana ng'ombe wao kwenye maeneo. Leo wanaambiwa ng'ombe wakifika tu wanachukuliwa. (*Makofi*)

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, ninalotaka tu kusema ng'ombe hawa watakutikana wamefungwa pia wanachukuliwa, wamekusanywa katika eneo salama pia wanachukuliwa. Na ng'ombe mmoja ukamlipe shilingi laki tatu, eeh! maskini ya Mungu ana pesa kazipata wapi? (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, haya nimeyasema kwa niaba ya wananchi wetu wa Zanzibar hasa wa Mkoa wa Mjini/Magharibi, lakini zaidi ya Wilaya ya "A" na "B". Wilaya ya Mjini siingilii. Amri ya Rais ni halali kabisa lakini Mhe. Rais anapotoa amri yake wengine tunachukua koti kubwa, tunawaathiri wafugaji wetu. Waheshimiwa ninaomba tuungane hili suala wananchi wetu wanapata usumbufu. Mfano wa Bumbwisudi huko, sijui wapi, Fumba, Bweleo anasema yote ni Manispaa. Manispaa tokea asili watu wanafuga. Manispaa itakuja baadae kwa maeneo maalum lakini tusisitize tu kwamba wananchi wetu maisha yao wanategemea kilimo na mifugo. (*Makofi*)

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, narudia tena kuiunga mkono hotuba hii, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kijitoupele na wafugaji wote wa Mkoa wa Magharibi wataniunga mkono kwa hili, nashukuru ahsante *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa hotuba yako nzuri na uwasilishaji wako mzuri nakushukuru kwa hilo na pia nikushukuru kwa dakika zako tano ulizoniomba kuhusiana na suala zima la wafugaji ng'ombe, nadhani muhusika waziri atalifanyia kazi suala hili. Tukiendelea, tuendelee na wachangiaji.

Nilikua naomba sana Waheshimiwa Wajumbe muda wetu ni mdogo na wachangiaji ni wengi, kwa hivyo nawaomba sana tuchangie katika mada husika sana, tutumie dakika zetu vizuri na tuwasilishe michango yetu vizuri pasi na kutoka nje ya michango yetu. Kwa hivyo, naomba sana Waheshimiwa Wajumbe kwa hili. Mchangiaji wetu wa mwanzo katika bajeti hii ni Mhe. Nadir Abdul-latif, akifuatia Mhe Saada Ramadhani Mwendwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said ajitayarishe. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Bismillah Rahman Rahim. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima wa afya, na niwapongeze viongozi wote waliohudhuria hapa kwa afya njema. Vile vile nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na wizara yake yote kwa ujumla kwa kazi nzuri aliyoianza.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri. Mimi nitaanza na suala la ushirika na vikundi. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Ali Suleiman Shihata kwa msimamo wake wa mifugo. Mimi vile vile nitalizungumza suala hili la mifugo. Kwanza wizara yake imeeleza ndani ya kitabu chake hiki kizuri kwamba ushirika ndani ya Kaskazini A, hasa jimbo langu mimi kumeandikwa vikundi vya ushirika vitatu tu, ni jambo la kusikitisha sana wakati nina vikundi vya ushirika karibu 200.

Mhe. Waziri ningekuomba sana hawa waliofanya utafiti wa kuonana na hivi vikundi au ushirika, hesabu hii haikubaliki kabisa. Mimi binafsi nimepita kwenye vikundi vyangu vilivyosajiliwa na vilivyokua havijasajiliwa mwezi uliopita viko karibu 400 katika Jimbo la Chaani. Leo nakuja kuambiwa kuna vikundi vitatu humu ndani vilivyosajiliwa, vimetokea wapi hivi vitatu wakati kuna vikundi zaidi ya 200. Mhe. Waziri nakuomba sana hizi idadi zinazoandikwa zifuatiliwe kwanza ziwe za ukweli halafu ndio ziingizwe kwenye vitabu. Leo nakuja kuona hapa kuna Mchezashauri, vikundi viwili na Moga kikundi kimoja Kaskazini A nzima ambapo vinatambulika na wizara yako.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, suala alilozungumza Mhe. Ali Suleiman Shihata naliunga mkono sana kwa sababu katika vikundi vya ushirika pamoja na vikundi masuala ya mifugo yamo. Mimi sio mwakilishi wa mjini, au katika Mkoa wangu wa Mjini Magharibi, lakini wananchi wetu wa Zanzibar nzima tuko nao pamoja tunayafanyia kazi. Mhe. Rais anapotoa kauli basi kauli yake huwa nzuri na keshaipima, lakini wale anaowapa utendaji basi hugeuka wao mabeberu.

Mhe. Mwenyekiti, nakuomba sana mtu asivae koti akajifanya yeye kuliko Rais, afuate amri ya Rais alivyoelekeza. Leo Mhe. Rais anaonekana kote kwamba katoa kauli, kumbe yeye siye aliyefanya hivyo, waliofanya hivyo ni watendaji wake, kwenda kutoa ng'ombe ndani ya nyumba. Sijui kwenye sehemu ambayo hatoki kwenda kuwanyang'anya watu mnawanyanyasa, haipendezi. Mhe. Mwenyekiti, kama wizara hii haina fedha basi msitafute fedha kwa njia hii ya kudhulumu watu.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Waziri suala hili likafuatiliwa vizuri, ushirika wenye vikundi wanalalamikia sana serikali na wanachama kwa jumla, wakati sivyo Mhe. Rais alivyosema. Leo watu wananyanyaswa na kudhulumiwa, kisa kutafutwe fedha kwa njia yoyote ile. Kama hakuna fedha basi zitafutwe kwa njia nyengine.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir naomba sana turudi kwenye mada, kwa sababu Mhe. Ali Suleiman Shihata tayari ameshaliwasilisha hili suala na waziri husika, ameshalipata naona litafanyiwa kazi vizuri. Kwa hivyo, naomba urudi kwenye michango yako.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna vikundi vya ushirika kwenye wizara yake na mambo ya ajira. Sasa na vikundi vya ushirika wanao ng'ombe kwa nini nisizungumze. Mimi nazungumzia vikundi vya ushirika vyenye ng'ombe wananyanyaswa. Kama nilivyosema narudia tena, kama wizara haina fedha kwenye masuala mengine basi wasiende kufanya wanavyotaka wao, wafuate amri ya Mhe. Rais sio mtu anakwenda kuingiliwa ndani ya nyumba. Haya ni matatizo tuzungumze ukweli, hakuna kuoneana haya hapa, mtu afanye kazi aliyopewa. Waziri kama hawezi kazi basi akatafute kazi nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende kwenye suala la ajira ya vijana. Imeorodheshwa kwamba wizara hii inatambua kwamba kuna vijana 9,542 ndani ya Zanzibar nzima. Hii kwa kweli inasikitisha ajira ni ndogo, maana kama tulivyokua sisi Zanzibar tuna vitega uchumi vingi vya watu binafsi; mahoteli, viwanda na mambo mengine, kuwa na ajira 9,542 ni ndogo. Kwa kweli hali hii hairidhishi na namuomba sana Mhe. Waziri na wizara yake yote kwa ujumla ifuatilie hili suala vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile suala langu namuuliza Mhe. Waziri aje kunijibu kwenye kupitisha bajeti kwamba hawa vijana 9,542 Wazanzibari wangapi, Tanzania Bara wangapi na wa nchi nyengine wangapi ili nipate kujua kwenye 9,542. Ni wapi na katika vitega uchumi gani wameajiriwa ikiwa ni hoteli, viwanda au *restaurant* ya vyakula, tujuwe hii ajira ya watu 9,542 ni ya miaka mingapi hata wakafikia watu hawa kwenye ajira hii. Hilo ni suala langu moja kwenye upande wa vijana.

Vile vile niende kwenye mada ya matumizi ya matukio ya udhalilishaji wa watoto mwaka 2015/2016. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hapa kunasikitisha kweli kweli yaani Zanzibar imeshafika hatua tena tutakuja kuitwa sote wabakaji na wadhalilishaji kwa hali hii tunayokwenda nayo. Hapa kuna waliokashifiwa 355, kubakwa 501, kulawitiwa 35, ujauzito 132; hii ni mwaka 2014/2015 na 2016. Jumla ya kesi hizi ziko 1,014 hivi kweli kesi hizi zinaingia akilini kweli. Kwa mwaka mmoja kesi hizi kwenye nchi ndogo kama hii ndogo. Mhe. Waziri ningekuomba sana hawa wote waliofanya matukio haya wachukuliwe hatua za kidikteta. Haiwezekani watu wanabaka watoto halafu wanachiliwa au tunaambiwa ushahidi haupo. Inasikitisha sana, au tunataka

tufike hatua mpaka mtoto wa mwakilishi au mtoto wa waziri abakwe ndio tuchukuwe hatua. Kwa kweli tunawanyanyasa watoto wa watu na hatua hazichukuliwi vizuri. Mimi nawapongeza sana polisi, wanawakamata wale watu lakini mwisho wazee na wizara inakua nyepesi mtu anaondoshwa na kesi inafutwa.

Mhe. Mwenyekiti, ningemshauri vile vile Mhe. Waziri na Polisi, ikiwa mtoto keshafanyiwa vitendo hivyo na ushahidi upo mzee anakwenda kufuta kesi, basi akamatwe yule mzee awekwe ndani, kesi kama hii hatuwezi kuiwachia mzee kuitetea. Mhe. Waziri inasikitisha sana kuona kesi ziko 1,014 kesi za maajabu ajabu za ubakaji. Halafu leo tutakuja kuambiwa katika kesi 501 za ubakaji eti kesi 400 hao waliobaka hawajajulikana inaingia akilini hiyo.

Mhe. Waziri nakuomba sana hili suala uje ulisimamie, hata kama ni mgeni kwenye wizara hii lakini mimi mwakani nakuja kukuuliza tena.

Vile vile maswali yangu kwenye kesi hii ningeomba aje anijibu kwenye kupitisha bajeti. Ni watu wangapi wamekamatwa kwenye kesi ya ubakaji, wangapi wameshachukuliwa hatua na wangapi waliofanya tendo hili na ambao watasema wao hawajawakamata hawajajulikana. Nataka aje kunijibu hili swali kwenye hotuba yake, namuomba sana suala hili. Vile vile kwenye *topic* hii aje anijibu kwamba hatua gani wale waliokamatwa wanachukuliwa na hufungwa kwa muda gani na adhabu gani hupewa pia aje kunijibu.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la watoto Mhe. Waziri watoto wengi wanatumwa na kupewa kazi ambazo sio kazi zao hasa wakati wa elimu. Wengine wanabebeshwa ng'ombe na wengine wanakwenda kuuza maji, michanga tena *illegal* maana yake wanavunja mpaka sheria na wazee wako tayari kuwatuma watoto wale kwa njia za magendo. Kuuza maandazi, ningemuomba sana Mhe. Waziri aje kunijibu, ni hatua gani alizochukua kuwasimamisha watoto hawa badala ya kusoma hutumwa tu.

Vile vile swali langu jengine kwenye mada hii aje anijibu mpaka sasa hivi hatua gani amechukua, na wazee wangapi ameshawachukulia hatua wanaowatuma watoto kwenye masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye mada yangu nyengine kuhusu matukio ya udhalilishaji wa wanawake yalioripotiwa wizarani. Kwa kweli hapa mambo mengi yapo madai ya mirathi, madai ya migogoro ya ndoa. Mimi ningewashauri ndugu zangu wanawake au wazee wangu, haya matatizo

wanapotaka kuolewa kwanza wamsome yule mwanamme, wasivamie tu saa nyengine ndio matatizo kama haya yanapotokea, wanaume wengine sio.

Mambo kama haya mngekuwa mnatafuta mtu ambae mnamjua au mnasikiliza wazee wenu basi yasingekukuteni, sio mnavamia vamia tu kwa kitu au kwa mtu tu labda ana uzuri au kwamba ana mali au mnataka kitu hiki. Msifanye hivyo, nendeni kwenye muongozo unaotakiwa. Fuateni muongozo wa dini yenu unavyokuelekezeni. Kwa Waislamu dini inaeleza kila kitu, vipi kumtafuta mwanamme. Leo kesi nyingi ziko hapa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niende kwenye mada ya kulelewa watoto yatima na kuozeshwa. Ningemuomba Mhe Waziri aje kunijibu, watoto hawa walioolewa 49 wanawake ni vigezo gani wizara yake inachukua kwenda kuwaozesha watoto hawa. Vile vile sheria inawalinda vipi na mwanamme gani ambae wanakubali aolewe yule mtoto ambae anatoka nje au wanamjua vipi, ili mpaka wanamuozesha yule mtoto, wakati yule mtoto ni yatima. Kwa sababu hili suala ni zito, yule mtoto ni yatima anapopewa tu mwanamme, tujuwe ni mwanamme gani na wanafuata vigezo gani hasa kumuozesha yule mtoto. Kwa sababu tumeshaambiwa yatima hana wazee, hata wazee wake kama wapo wanaomlea lakini sio wazee wake waliomzaa. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri swali langu aje kunijibu.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la wazee wanaopewa pencheni na wasiopewa pencheni. Hawa wanaopewa pencheni mwaka 2016 mwezi uliopita wa Arili, waliolipwa ni 18,371. Lakini wasiolipwa kwa mwaka huu huu mwezi huo huo 2,892. Ukenda mwezi Mei 2016 waliolipwa ni 19,333, na wasiolipwa ni 2,873. Mimi naomba kumuuliza Mhe. Waziri aje anijibu ni sababu zipi zilizosababisha wazee hawa zaidi ya 2,000 wasilipwe fedha zao na ni njia gani wanazotumia kwenda kuwalipa hawa wazee, na ni kwa nini hasa mpaka hivi sasa tunaona mpaka mwezi uliopita kwamba ni zaidi ya wazee 2,800 kwenda 3,000 hawajalipwa fedha zao. Naomba aje anijibu kwenye maswali yangu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitamalizia tu kwa kusema kwa kumuuliza Mhe. Waziri kuhusu hili suala la ubakaji Zanzibar litamalizika lini na hatua gani kali hasa atazichukua. Kwa sababu mimi sitaki kuvunja sheria, lakini nawalaumu sana wale wanaomkamata mbakaji halafu wakamfikisha kituoni. Huyu mtu hata sio wa kufikishwa kituoni. Sisemi mtu afanye hivyo, lakini kwa kesi kama hii sio wa kufikishwa hata kwenye kituo na wizara. Mimi namuomba Mhe. Waziri aje anijibu suala la ubakaji Zanzibar litakwisha lini. Ahsante sana naiunga mkono kwa asilimia 90 na asilimia 10 yangu naibakisha kwenye hotuba yake atakapokuja hapo mbele, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kwa mchango wako mzuri, na pia nikupongeze kwa kutumia muda ipasavyo. Sasa namwita Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa, akifuatiwa na Mhe. Suleiman, na Mhe. Bahati Khamis Kombo na Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo) wajitayarishe.

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma kwa kunijaalia leo kuweza kufika hapa na kunyanyuka kuzungumza niliyokuanayo. Pia nikushukuru wewe uliyeweza kunipa nafasi hii nikapata kuzungumza niliyonayo ndani ya nafsi yangu. *(Makofi)*

Tatu, niwashukuru wapiga kura wangu wa Mkoa wa Mjini wanawake walionichagua nikaweza kufika hapa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina machache tu ya kuzungumza yaliyokaa ndani ya nafsi yangu na yaliyokuwa yananiumiza ninapoishi mitaani na kuona watoto wanateseka. Mhe. Mwenyekiti, mimi nazungumzia ajira za watoto mitaani. Sisi ndio tunaishi mitaani tunaona watoto wanavyotumika wa kuanzia umri wa miaka 9 mpaka miaka 10, wanavyotwikwa sinia za ndizi, sinia za tungule na sinia za madagaa Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana. Utamkuta mtoto keshachoka amelala barazani, dagaa linang'ong'wa na nzi na yeye kurudi nyumbani anaogopa ataulizwa kwa nini dagaa halijesha.

Mhe. Mwenyekiti, sina mchango mkubwa ila nina maombi kwa kupitia kwa wazee wenzangu kwanza, tuwache kuwatuma watoto, tuwaache wasome hawa ni taifa la kesho watakaokuja kutusaidia sisi wenyewe na jirani zetu.
Pia nimwambie Mhe. Waziri kwamba analichukuliaje jambo hili, ni kweli siku nyingi tunaisikia serikali inasimamia sana kuhusu ajira za watoto ziachwe, lakini bado wananchi wanaendelea kuwatuma watoto. Je, Mhe. Waziri analichukuliaje kuhusu hizi ajira za watoto na kuweza kuwakomesha hawa wazazi wanaofanya kazi hiyo ya kuwatuma watoto wao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye sehemu ya mikopo. Wanawake wa Mkoa wa Mjini wanajua serikali yao haina uwezo wa kuwaajiri watu wote, hivyo wanajua kuwa lazima wengine watapata ajira na wengine watajituma kwa nguvu zao kwa kupitia *SACCOS* zao wanazofanya, lakini pia na vikundi vyao vidogo vidogo wanavyojikusanya wanawake wakakaa pamoja na wakafanya kazi na wakapata maendeleo ya kuweza kuwakidhi wao na watoto wao, wakaweza kuwasomesha.

Mhe. Mwenyekiti, malalamiko yangu yako hapa. Katika kipindi kilichopita, Mhe. Waziri aliyepita alikua anapita katika vikundi anatuhimiza wanawake tuende tukachukuwe mikopo. Kweli tulikua tunakwenda na nina uhakika ninachokisema, kuna vikundi vingi sana vya wanawake wa Mkoa wa Mjini walishaajiriwa, lakini na walichukua fomu wakafuatilia kule wizarani, kule Forodhani wanakwenda wakirudi kila siku. Lakini kwa kweli wanawake wengi mikopo ile hawakupata. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nilikua namuomba Mhe. Waziri akija hapa aniambie. Wale wanawake wa Mkoa wa Mjini wanaofanya biashara zao hususan hawa wenye biashara ndogo ndogo, aje aniambie anawasaidiaje wanawake wale ili kupata mikopo. Kama ana uhakika, kwa sababu mambo mengi yamezungumzwa sana hapa watendaji wake waliomuandikia, lakini nina uhakika vikundi hata 50 nitamletea vya wanawake wa Wilaya ya Mjini waliokua hawajapata mikopo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri akija hapa aniambie, wanawake hawa wa Mkoa wa Mjini wanaojitegemea wenyewe kimaisha yao, ni lini atawapatia mikopo ili wapate kuendesha maisha yao na familia zao, ili waache kunyanyasika. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana sina mengi, ahsante sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia 95 na asilimia 5 mpaka atakaponiambia wanawake hawa watapata mikopo lini, ili niende nikawaambie tupate kwenda huko kunakotoka mikopo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Saada Ramadhan. Anayefuata Mhe. Suleiman Sarahan Said, Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mhe. Ali Khamis wote wajitayarishe.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii na mimi niendelee kuungana na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha hapa tukiwa salama wa salmini na Ramadhani hii.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nataka nichangie kidogo kuhusu hotuba hii ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, jambo la kwanza mimi nataka nizungumzie kuhusu habari ya, kama alivyozungumza mjumbe mwenzangu Mhe. Nadir Abdul-latif pale kuhusu suala la wazee na pencheni.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili kwa upande wa kule Pemba nilivyouona, kwa sababu sheria ipo lakini wakati mwengine tunatizama na hali halisi. Kwa mtazamo wangu mambo haya yalianza kama hayakua rasmi, watu wengine

walichukulia kama ni masihara tunajua kawaida yetu, watu wengine unajua katika muda wa kisheria waliandikishwa katika vitambulisho mtu akiliulizwa miaka yako anasema haijui, kwa hivyo muandikishaji wa cheti wa kadi ya Uzanzibari mwengine alikuwa akiandikisha akimwambia miaka 40 mtu anafika miaka 60, miaka 50 mtu anafika miaka 70 hatua hii imefikia. Kuna watu wana miaka 80 bado wana miaka 65, bado wana miaka 67 ile haki ambayo iliyokuwa ni haki yao wanaikosa.

Kwa hivyo ningemshauri Waziri akafuatilia tena masuala haya kwa kuangalia kwa kina kwa sababu ule si msahafu ni vitu ambavyo vinaweza kutambulika na vinaweza kubadilika, ili wale watu ambao wana haki ya kupata basi Mhe. Waziri wapate haki ile, ningeshauri suala hili ulichukue ili lifanyiwe taratibu hizo.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ningesema katika Serikali za awamu tafauti zilizopita ukweli wanafunzi na watu wengine hasa vijana vijana walikuwa na sheria tofauti ambazo zilikuwa tuseme kama adhabu fulani. Nakumbuka sijui kama Mhe. Rais Aboud Jumbe, yeye ilikuwa sheria miaka mitano kufungwa, lakini watu wale walipokuwa wanafanya mambo yale kinyume na sheria miaka mitatu anachukua mwanamme, miaka miwili anachukua mwanamke. Yote hii ni kufanya kila hali kukomesha jambo hili. Kwa sababu Mheshimiwa nataka nikwambie wanawake ni wetu tunawapenda lakini ndio vishawishi vikubwa hata kwenye *Qur-an* hawa ndio wametajwa mara nyingi sana kwa matatizo mliyonayo. Na wewe Mheshimiwa ni mwanamke, kwa hivyo nakwambia haya matatizo mnayo mnatusababishia sisi wanaume sisi roho zetu ndogo Mheshimiwa lazima na nyie mjikaze, ili na sisi tujikaze.

Kwa ufupi hili Mheshimiwa ungelichukua tukatizama musituonee wanaume watupu Mheshimiwa na nyie wanawake ndio matatizo makubwa, nguo zenu hamujistiri vizuri na sisi kama mnavyotujua lazima tuangalie hali mbaya, nataka niangalie Mheshimiwa utizame ukweli hata hii Ramadhani na mengine. Mimi siingilii mambo ya starehe na dunia inavyokwenda nguo zote zilizokuwa hazihusu basi zivaliwe usiku *Disco Night* sio barabarani. Wakati mwengine watu wanapata ajali kwa mwanamke ajali za magari humo kwa mwanamke, ajali nguo uliyovaa mama mwenyewe mkubwa hujui unaelekea wapi, wanapiga majumba, wanapiga watu n.k.

Mheshimiwa nguo zidhibitiwe yale madira yamejengwa angalau ile hali halisi isionekane hali imekuwa mbaya kidogo, tuachie Dar es Salaam hata sisi, mimi nikitaka kufunga Ramadhani mara nyingi nakwenda Dar es Salaam kwa sababu nataka nipate ile hadhi hasa ya kufunga niiweze nafsi. Hapa Zanzibar mambo

haya yalikuwa hayapo, lakini sasa hivi sina haja ya kwenda kufunga Bara Mheshimiwa hapa Zanzibar tu pananitosha kwa nafsi yangu mambo yanakuwa mazuri sana, lakini miezi hii na mchana ningeshauri sana katika mambo haya wenzetu hawa wakajistiri.

Mhe. Mwenyekiti, wengine wana maungo mabaya ambayo kukwambia kweli ni mazito ningeshauri Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti suala hili tena nalielezea kwamba bado kuna kipindi kimoja ulineleza habari za sheria ya kugawana mali mimi hapa sijasema suala la kurithi, suala la kurithi siingilii mambo ya dini katika kurithi naingilia mambo ambayo mama watoto anakaa na baba watoto katika vipindi vyao, wanazaa watoto halafu watoto wale anamsukumizia mama hamuulizi kala wala kalamu.

Nilishazungumza kwamba ameshajenga nyumba, ana gari na kila kitu. Lakini matokeo yake watu hawa hawajulikani tena maana yake mama hafaidi matunda ya baba waliyokuwa wakila dagaa, wakila chakula kikavu na kuhangaika. Vile vile ndio *source* ya watoto wa mtaani mtoto akiwa hana baba na mama, kwa pamoja mama hamuwezi mambo yote haya yanasababisha na hawa mababa wanaowacha ovyo ovyo Mheshimiwa ndoa za kukatika ovyo ovyo zimezidi, na hawa watoto nataka nikwambie kwamba utatunga sheria mpaka utachoka, ikiwa watoto hatujawadhibiti kwanza na wazee hatujawadhibiti basi hali hii haiwi.

Mheshimiwa uliniambia kwamba Bara kuna sheria ambayo imetungwa miaka miwili tu ukiwa na mtu ambae mmekaa kindoa mnagawa mali ile iliyozalishwa katika kipindi chenu. Bara sheria yoyote ni ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzani na bara sisi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sisi tumo na tuna wabunge wetu na sheria hii imepitishwa, sifikirii kwa nini na hapa Zanzibar isipitishwe wakati ambapo pia kule kwamba ni *BAKWATA*, lile nalo limo na hapa kwetu Waislam wapo. Ikiwezekana wahusishwe mashekhe sheria hii waiweke vizuri. Hatuingilii katika kugawana mali za urithi hapa, hajafa baba hapa ni vituko vya baba kwa hivyo vile vituko vidhibitiwe. Ningeshauri Mheshimiwa ile sheria na hapa itumike. Naomba ukija uwe umeshawasiliana na *BAKWATA* na wengine wakufahamishe hii sheria tuipitishe Mheshimiwa hii kauli ya kila siku hamna.

Mheshimiwa ningekushauri sana hiyo ili angalau tuangalie na hili suala ambalo tunalizungumza mambo ya ubakaji na mambo mengine ninavyofahamu Mheshimiwa kila Wizara ina mwanasheria. Nina uhakika na wewe unaye mwanasheria wako wa Wizara yako. Mimi ningeshauri watu wengine labda

kesi za Polisi na matatizo mengine zinakuwa na mashaka kwenda kwao. Huyu mwanasheria wako asitumike kwako wewe tu atumike na kwa hawa watu ambao wanapata matatizo, ungeshauri watu unaowaona wana mashaka mashaka waje Ofisini moja kwa moja na mwanasheria wako aweze kulisimamia hili.

Mheshimiwa nataka nikwambie katika masuala kama haya sisi kama ni Serikali na watu wengine kama ni Serikali Mheshimiwa mzazi anakuwa na mashaka mawili; ama anakuwa anadhibitiwa au anakuwa kuna matatizo. Lakini kosa likishafanyika Mheshimiwa na likiripotiwa kwako wewe au Polisi Mheshimiwa mzazi asiwe na *say* tena moja kwa moja liwe liko kwenye Serikali, kama ni sheria watakwenda kutoa ushahidi, kama hakuna litaonekana huko huko lakini asisikilizwe mzee tena.

Mhe. Waziri kwanza nataka nikwambie sababu kubwa inayotufanya mambo haya ni umasikini, mtu akifanya jambo tu kapeleka kitu suala linafutwa lakini matatizo yanakuja kwa Serikali itakuwa kila siku sisi tunahangaika kwa ajili ya Serikali lakini matokeo yake yatakuwa ni zero. Kwa hivyo ningeshauri wewe ukishakuripoti nimefanyiwa tatizo unaambiwa wewe basi tunataka mashahidi, hamna tena umsikilize kesi iende wala hamna. Kesi iichukue Serikali na mkondo wake moja kwa moja ningeshauri sana Mheshimiwa hiyo.

Mheshimiwa pia nishauri kitu kimoja nashauri kwamba kuhusu habari Wizara yako ina Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto; Mheshimiwa na wanaume watiwe humo humo angusha tena kigezo kimoja na wanaume humu mna udhalilishaji wa wanaume wa sekta tatu.

Kuna udhalilishaji wa wanaume, watoto wadogo wanachukuliwa na wazee wenye pesa wanawadhalilisha watoto wa kiume, hivyo hivyo wanawachukua, mzazi hataki wazee hawataki mama kashachukua mtoto mdogo anajisikia hasikii. Sasa na nyinyi tukichukua watoto wadogo mnatufunga kwa nini sisi hamutuachi na hawa watoto wadogo wa kiume nao wanauma. Unamlea mtoto wako halafu anakuja kupata shangingi sijui dude gani lile linakuwa linamdhibiti, linamharibia maisha yake yote wanaume nao wafunguliwe.

Mhe. Mwenyekiti, wengine wanakuwa wameoa Mheshimiwa huko kwenye ndoa kuna vishindo kweli kweli huko, kuna matatizo wengine wanapigwa vibao, wengine wanafanya mambo chungu nzima na pa kwenda kusemea hawana; hawana idara hawa, Idara ya Wanaume Mheshimiwa iwekwe humu.

Kuna wengine Mheshimiwa sasa nataka niingize tena hii ya Wazee Mheshimiwa wazee wako wa kiume au wazee wengine wa kike ndio washapata pa kukimbilia. Wazee wowote ni wazee wa Serikali. Kwenye familia wanazalilishwa wazee ndio tukaweka zile sehemu ambazo wazee wanatunzwa.

Sasa tunaangalia kwenda familia kama mtoto anampiga baba yake usiulize chukua polisi mchukue mzazi mpeleke sehemu ambayo aende akatunzwe…….

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika tatu.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mheshimiwa nina dakika tano nimeanza saa sita kamili sipingi lakini dakika zangu nazitizama nisamehe Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea una dakika tatu.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Wizara nzito Mheshimiwa ina mambo lakini aa haya wale wazee wanaokuwa wanadhalilishwa tukawachukue hawana shida nao ukenda ndani mtu kafungiwa huko kila kitu huko huko. Tukawachukue halafu mtu asiseme baba yangu unamwambia wewe huna baba ungekuwa baba ungemuacha sasa hivi hawa tukawachukue tena tuwaambie hasa aliyekuwa hataki kumtunza baba yake na mama yake, mchukue Mheshimiwa hili nakwambia.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikwambie sasa hivi habari ya *DNA* mpaka leo kipimo cha *DNA* hakijafika matatizo haya yanatuumiza kwa sababu sasa hivi kila asubuhi wanaachana; mtoto si wangu mtoto akizaliwa anapimwa pale pale baba anajulikana. Sasa tufanyie haraka *DNA,* hebu Mheshimiwa hata kama si Wizara yako ni Wizara ya Afya lakini piga kelele *DNA* inavunja ndoa mmeshapata watoto watano wasita katoka mweusi inakuwa balaa, siku nyengine mweusi ni bibi yako, babu yako urithi huo.

Sasa pengine ile *DNA* ndio mwenyewe hasa kulikuwa na kipindi kimoja cha Mzee mashaka alisema huyu ndio mwenyewe lakini katika rangi mimi mweupe Mke wangu mweupe kazaa...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa zungumza na kiti.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Kwa hivyo Mheshimiwa ningesema kwamba ingawa katika dini yetu tunasema kitanda hakizai haramu lakini tungejitahidi sana katika hali ya kawaida kwamba *DNA* ipatikane haraka Mheshimiwa, lakini mimi ningesema kwamba sasa hivi wakati wa ndoa mara nyingi ndo zetu

tunazifunga Kiislam, tunazifunga vizuri anakuja mtu na barua sijui karatasi anajaza umeolewa vipi, sijui tieni saini.

Mheshimiwa kwa kuondoa matatizo haya ya kuachana ovyo, unda kamati ya kila eneo ya Mashekhe wakati wa kutaka kuozesha kamati iwepo sio iwepo wakati wa harusi tu na wakati wa kuvunjika, ndio ipelekwe kamati ikae maana yake tunaozesha kiislam wanaitwa mashekhe, lakini siku ya kuachisha zinaanza wazee watu wangapi wangapi.

Anzisha kamati ili mtu anapokuwa anaoa inakaa kamati inamwita yule bwana anaambiwa bwana unaoa kwa salama salimini. Kuachana ni ruksa patakapokuwa na matatizo, na siku ya kuacha kamati irudi itizame kosa la nani, ili mtu huyo ajue kupata haki yake ni ya mume au ni ya mke. Kwa sababu Mheshimiwa tunakwenda tu kama vile hatuna vigezo.

Mheshimiwa basi mimi naunga mkono hoja maana yake naona umenitizama vibaya sana Mheshimiwa. Ahsante sana.*(Makofi)*

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Asante sana Mhe. Mwenyekiti, naitwa Bahati Khamis Kombo. Kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeweza kutufikisha hapa tukiwa wazima wa afya. Pia nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa hotuba yake nzuri, ambayo hutuba hii imetupa mambo mbali mbali ya kuweza kuyatekeleza na sisi kama ni wawakilishi wa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda moja kwa moja katika vyama vya ushirika, ndani ya vijiji vyetu au shehia zetu tunavyo vikundi vya ushirika vya aina tofauti, lakini vikundi hivi vimeonekana kufa kwa haraka kwa sababu mbali mbali. Tuna vikundi vya ushirika ambavyo vinapewa hati na vinapewa misaada mbali mbali na Serikali na badala yake kutokuthaminiwa na wananchi, kutokuzingatia zile sheria walizozitunga wao wenyewe basi vikundi hivi vinakufa na kulaumiwa Serikali ambayo baadhi ya wakati sio yenye matatizo.

Kwa hivyo nikuombe Mhe. Waziri hili ukae uliangalie sana jinsi ya vikundi hivi tulivyonavyo ambavyo vimepewa usajili na vimeweza kupewa ruzuku mbali mbali, lakini wamshindwa kuzitekeleza vizuri na vikaweza kuendelea mpaka leo.

Mhe. Waziri vile vile tunavyo vikundi vya vikoba vikundi hivi viko katika vijiji vyetu ambavyo wao wanaweka pesa zao wenyewe katika visanduku, na hivi visanduku vinakuwa na kufuli tatu sasa imebainika kuwa wao wenyewe binafsi

ule utaratibu wa kuvihifadhi vile vikundi vizuri vikakosekana, upotevu wa zile pesa hawana.

Mhe. Waziri nakuomba kwamba hawa watu wanahitaji elimu ya kutosha kwa sababu wao wenyewe wanatafuta na baada ya kutafuta huweka, ili baadae kile wanachokipata waje watumie kwa lile lengo walilolikusudia, lakini utakuta lile lengo halifikiwi na wao wenyewe binafsi wanakuwa wanagombana mara kwa mara.

Kwa hivyo Mheshimiwa utakapokuja nakuomba sana uniambie jinsi gani utaweza kuwasaidia hawa watu wa vikoba, ili vikoba vyao visiweze kuanguka kabisa kabisa na vikawa havijulikani tena.

Mhe. Waziri niende moja kwa moja katika ajira za watoto wadogo, hawa watoto wadogo tunaamini kwamba wazazi wao kutokana na hali ngumu ya maisha waliyonayo ndio wanasababisha hawa watoto kupewa biashara wakati wanapokwenda skuli wakakosa kwenda chuoni, au kwenda chuoni wakakosa kwenda skuli wazee hawa wanauza biashara zao lakini kutokana na ile hali ngumu waliyokuwa nayo inasababisha na wale watoto wale baadhi yao wamewapeleka katika shule za kulipia na wanakosa ile huduma ya kuwapa. Inasababisha watoto hawa na wao kupewa kazi ambayo ni kinyume na utaratibu. Mhe. Waziri wewe ndie Waziri wetu wa Wanawake, Uwezeshaji na Watoto tunakuomba wanawake hawa Mhe. Waziri uwaweke, uwaelekeze ili jinsi gani ya kutatua matatizo yao bila ya kuwashirikisha watoto wadogo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nimpongeze Mhe. Rais kwa kuwafikiria wazee waliotimia miaka sabiini, lakini pia wewe Ni Waziri wetu wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto sasa hapa tuna wale wanawake ambao wametimia miaka kumi ni wajane au kuendelea hawa Mheshimiwa hawakufikiriwa lolote na wao wana watoto. Tungekuomba Mheshimiwa hawa na wao ukaweza kuwafikiria angalau kwa kupewa sabuni, ili kuondosha lile tatizo la wanawake kuweza kuzalilishwa.

Mhe. Waziri, vile vile niende kwa wanawake wale ambao wako nyumbani, lakini wanaweza kujituma lakini wao kwao hawawezi kujituma, hawafanyi lolote kwao wao ni lawama tu Serikali haiwasaidii lolote ,kwa hivyo Mhe. Waziri tushirikiane kwa pamoja kama sisi Wawakilishi, masheha wanawake hawa na wao tuweze kuwapa somo, ili waweze kujituma huu si wakati tena wa kukaa nyumbani tu ukasema kila kitakachokuja wewe uletewe.

Mhe. Waziri, kwa hayo machache mimi leo nafikiria hapo kutokana na hali yangu siwezi nikachangia sana. Ahsante sana Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii kuweza kuzungumza machache. Nami niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu Muumba Mbingu na Ardhi aliyetuwezesha tukaiona siku ya leo tukiwa wazima na tukiendelea na saumu.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kumteua mama yetu mama Muldline Cyru Castico, kwa kumpa hii Wizara na hakufanya vibaya. Kwa kweli hii Wizara ni kubwa na ina mambo mengi, lakini kwa juhudi zake ninavyomjua mama huyu inshaallah kila kitu kitakaa sawa.
Pia niendelee kuwashukuru watendaji wake wote kwa kuiandaa hotuba hii nzuri ya aina yake Allah awalipe fadhila zao na inshaallah watasimamia majukumu yao jinsi inavyopaswa.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba hii imeeleza mambo mengi hususan kwenye habari za vijana, watoto, wanawake na Wazee, kwa kweli mimi mchango wangu leo nataka nigusie suala la watoto kwanza. Licha ya changamoto nyingi ambazo zinaikabili Wizara hii kutokana na kwamba ubakaji wa watoto umekithiri siku hadi siku. Hii inaonekana kwamba kutokana na hali ambayo sasa malezi ya zamani yaliyokuwepo na sasa hivi yamekiukwa kila mmoja analea mtoto wake, kwa vile anavyotaka yeye.

Niiombe Wizara kwa kupitia serikali ichukue juhudi za makusudi kuwakusanya wazee wetu na kuwapa taaluma nzuri juu ya malezi ya watoto kutokana na kwamba hali hii ya ubakaji na kesi ndogo ndogo zimekithiri, ili waweze watoto hawa kupewa taaluma nzuri wazazi wao na kuwaelekeza katika mambo mazuri.

Tukikumbukia zamani ilikuwa kuna ulezi wa watoto kwamba kila mtu alikuwa hakuna mtoto wake yeye pekee, wakisaidiana wazee katika malezi ya watoto ili wafikie katika mazingira mazuri. Ni imani yangu ilikuwa wao wanawasimamia kidete katika juhudi hizi kuona kwamba watoto wale wanafikia malengo ambayo yanastahiki. Lakini kwa sasa kila mmoja ndio imekuwa ni mlezi wa mtoto wake mwenyewe hata kama kuna tatizo mtu akiliona analifumbia macho na mtoto yule kuweza kupata matatizo. Nimuombe waziri kupitia wizara hii akae *benet* na wazee pamoja na watendaji wake walione hili kwamba wawashajiishe wazee wetu kurudia ule mfumo wa zamani wa malezi ya pamoja, ili kuona jamii inakaa vizuri na watoto na bila kupata matatizo.

Nije kwenye uwezeshaji wa vijana. Kama tunavyoona wizara hii imebeba mambo mengi tena mazuri lakini wizara hii pia imekabiliwa na kuwaona vijana kama vijana ndio nguvu kazi ya taifa. Sasa hivi hali ya uharibikaji wa vijana umekuwa mkubwa kutokana na kwamba hawana ajira, hawana mikopo ya kujiendeleza, licha ya hotuba alivyoisoma Mhe. Waziri alisema kwamba kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017 kuna mambo mengi ambayo yatafanyika, licha ya hayo mimi ningependa kuwe na mfumo maalum wa Waziri wa Fedha. Kwa sababu hali hii ya bajeti yao pesa zao nahisi zimeonesha kwamba kiwango chao mara hii walichotengewa ni kidogo sana; wawaongeze fedha kutokana na majukumu makubwa na hii wizara kwa kusema ukweli sio ndogo kila mmoja anaelekezea macho hapa.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, mimi nije kwenye upande wa wazee, kama tunavyoona pale Sebleni kuna wazee wetu wanalelewa, najua serikali inajitahidi kutoa michango yake kwa ajili ya kuwapelekea wazee wale lakini kadiri ya siku zinavyokwenda na wao wakiona wanalelewa basi hali ile inakuwa nzuri lakini nimpendekeze Mhe. Waziri kwamba wale wazee kungetengwa muda maalum labda Jumamosi na Jumapili na wao wasibakie tu mule ndani, wachukuliwe waingizwe kwenye mabasi kidogo angalau leo wanapelekwa Kiwengwa ili kuona na wao wamo katika jamii na bado wanaendelea kulelewa. Kwa hivyo wanahitaji huduma mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikiongezea nimuombe Mhe. Waziri atoe taarifa kwani kesho kutwa ni mwezi Mtukufu wa Ramadhani tunakabiliwa na sikukuu, kero nyingi zinazokuwepo kutokana na hali ya ubakaji wa watoto, wazee wetu wao wenyewe nao ni mas-ul katika suala hili kila mmoja ni mchunga ataulizwa kwa alichokichunga. Kuna wazee maalum sasa hivi wameshatenga fedha zao maalum, washauza makuti, washauza mwani kwa ajili ya kuwatafutia watoto wao vitambaa vya thamani. Keshokutwa kama mnavyoona hali nyingi zinapigiwa kelele kwamba watoto wanabakwa, lakini moja linaloonekana ni kutokana na mtoto yule kumvalisha mavazi kama mwenzangu alivyosema yaliyokuwa hayastahiki.

Mtoto bado mdogo, mwari ndio kwanza anakua unamvalisha nguo za maajabu ajabu, maneno ya watu vitu vya ndani vinaonekana. Ile ni hali ambayo yule mtoto mwenyewe anaanza kujivunjia heshima na hasa ukilinganisha kwamba asilimia kubwa ya wazanzibari wengi wetu ni waislamu. Kwa hivyo si jambo la busara kuona watoto wale wanakatiwa nguo za maajabu jambo ambalo halipendezi. Ni vyema mzazi yule awasimamie watoto wake kabla ya kutoka nje awaulize mnaenda wana na hizo nguo mlizovaa ili ajue. Kwa sababu siku

hizi watoto wenyewe pia wameshakuwa watu wazima, mtu anaweza akaondoka pale na baibui lakini nguo za ndani alizovaa hazijulikani. Kwa hivyo mama kama mama nyumbani pamoja na wazazi awe yeye mwenyewe alione kwamba hebu huyu mwanangu kavaa nguo gani, lakini je, hiki kitambaa nilichomkatia kinastahiki.

Kwa hivyo ni jambo ambalo linahitajika kulisimamia sote kwa jumla kwanza kuanzia hali ya kule mtoto nyumbani wale wazazi wenyewe na mtoto mwenyewe lakini vile vile kuwepo na sheria maalum ambayo itafuatwa juu ya ukiukwaji wa hizi sheria kwa wale ambao watakwenda kinyume na hizi sheria, kwamba atakaeonekana kavaa mavazi ya maajabu ajabu basi akamatwe na kuhifadhiwa aitwe mzazi wake aulizwe hivi ndio mwanao ulivyomvalisha siku ya leo, ili na yeye kidogo iwe nafsi inamsuta kuona kwamba vile alivyofanya hakufanya jambo zuri.

Vile vile aendelee kutoa michango hii Mhe. Waziri kwa wazee kuwaelimisha juu ya taaluma ya kuhusiana na habari hii ya kuwa keshokutwa unapofika mwezi Mtukufu wa Raamadhani kumalizika, kunakuja sikukuu. Wawatake watoto wale ambao watatoka kwa ajili ya matembezi, wawafatanishe na wenzao ambao wako na akili zao nzuri na wataweza kuwalinda na wale watu ambao wataangalia kwa macho ya husda.

Kwa mfano katika hali ya kuwashawishi kuwaingiza katika vitendo vya jinsia. Aweze kuona kwamba pana mtu muhimu ambae likitokea tatizo yeye anaweza kukabiliana nalo na asiwaache watoto wale kutembea mmoja mmoja, watembee kwa vikundi na hii naona itapunguza hali ya kuhujumiaka kijinsia kwa watoto. Kwa hivyo pakiwa na tatizo kama hili kama hapana mtu basi kijana yule au mtu yule anaweza akamshawishi akamwambia njoo hapa mimi nina pesa chukua, hizo ukatumie fanya hivi, kwa hivyo ionekane hilo na wazee wapewe taaluma. Serikali itoe taarifa kwamba watoto watembee wakiwa wana mtu ambae kidogo anaweza kuangalia yale majukumu yao kwa siku ile.

Vile vile nikiendelea kwa mchango wangu wa leo Mhe. Mwenyekiti, nimuombe waziri kwamba hii wizara ni kubwa na imekabiliwa na mambo mengi ambayo inshaallah nimtakie dua Mwenyezi Mungu awaajalie hili ambalo wamelieleza humu waweze kulisimamia, kwa sababu kila mmoja ndio anawatolea wao macho kuona kwamba hii Wizara ni ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee Vijana Wanawake na Watoto. Ina majukumu makubwa lakini kwa uwezo wa Mungu lakini pia majukumu haya kwa kuwaachia peke yao hawatoweza kuyakabili mpaka sisi sote tuwe mas-ul kuwasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu leo si mkubwa nilitaka kusema haya kwa sababu, wengi wetu huko majumbani huwa tunakaa tu na kutupia lawama serikali, jambo ambalo serikali kuna mengine ni kweli ya serikali lakini kuna mengine sisi wenyewe tunapaswa kuyaangalia hususan wazee wetu wa kiume. Pale nyumbani wazee siku hizi wameacha kusimamia majukumu yao baba kama baba lakini anamuachia mzigo mama ambae mama huyu anapaswa kuwatunza watoto, anapaswa kuangalia kila kitu, mama huyu huyu wengine wanaachiwa jukumu la kutafuta chakula, wengine unawakuta humo sehemu wamo wanafanyakazi kubwa ambazo akirudi mama kachoka. Motto hajui kaenda wapi, mtoto kafanyaje, kwa hivyo tuwapunguzieni mizigo wazee wetu wa kike. Tuwasaidieni haya mambo, tuliwaoa kwa ajili tunawapenda. Kwa hivyo tusiwapende kwa masuala mengine tu, yote tuwasaidie haya majukumu, ni yetu na sisi ndio tunaostahiki kutoa hizi huduma tusimwamchie mama.

Mama jukumu lake ni la nyumba tu, ni kuipamba nyumba na kuwatunza watoto lakini majukumu mengine ni sisi kama baba. Tujuwe mtoto kaenda chuoni kwa mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani. Sasa hivi ukiangalia humo masokoni na madukani watoto wengi wamekaa hawendi chuoni na huu ndio mwezi ulioteremshwa Qur-an na wazee wana majukumu makubwa kuwasimamia hawa watoto. Kwa mfano Pemba mimi sasa hivi nikenda kule kwenye sehemu za uvuvi au fukweni, utawakuta watoto wadogo wanaparishwa samaki, jambo ambalo halipendezi.

Kwa hivyo hili nimuombe Mhe. Waziri alifatilie kuondokana na kadhia hii inayotufika. Kuna watu maalum wanawafanya watoto kwamba wao hawana kazi za kufanya, wanawashawishi na kuwapa hizi kazi ambazo wao wanaona wakiwapa zile shilingi kumi kumi ni faida lakini huko mbele wanawajengea hasara kubwa kwa sababu wanakosa haki zao za msingi.

Baada ya hayo machache ninaiunga mkono hotuba hii asilimia mia moja lakini nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha kwa kweli Wizara hii kiwango ambacho kitaidhinishwa kwa pesa zake ni ndogo na wasaidiwe kupewa pesa nyingi, ili kukabiliana na majukumu.

Tukizingatia humu muna vikundi vya ushirika, muna wazee wetu wanataka wawezeshwe na wazee hao kulelewa bila ya fedha haiwezekani. Lazima wazee wanahitaji huduma, watoto ndio hapasemeki, vijana ndio halkadhalika, ili waweze kuondokana na yale majukumu yao madogo madogo wapate kuondokana na yale mambo ya madawa ya kulevya na mengineyo. Ahsante.

Mhe. Masoud Abdulrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia mchana huu kukutana hapa. Mimi niende moja kwa moja kwenye usajili wa vikundi vya ushirika. Bahati nzuri serikali inahimiza sana uhamasishaji wa kuunda vikundi vya ushirika na mimi niwapongeze sana wananchi wamelikubali suala la kuunda vikundi vya ushirika. Lakini nataka niseme kwa wilaya yangu ya Magharibi "A" na Magharibi "B", sasa hivi wilaya zimegaiwa kuna wilaya mbili.

Nimuombe sana Mhe. Waziri awaombe maofisa wake wa Vyama vya Ushirika au maafisa wake au Katibu Mkuu wahakikishe ndani ya Wilaya ya Magharibi "A" kunakuwa na Afisa wake wa Vyama vya Ushirika na Magharibi "B" kuwe na Afisa wake wa Vyama vya Ushirika. Maafisa hawa wanapata kazi kubwa ya kutoa elimu kwa wanavikundi, kwa hivyo niombe sana Mhe. Waziri atakapokuja atuhakikishie pamoja na kuwa utaratibu wa kuundwa hii Magharibi "B" bado kunasua sua lakini ahakikishe anapatikana afisa ambae atatusaidia kwenye vikundi ili wapate kutoa taaluma kwa wananchi wetu wa kuunda hivi vikundi vya ushirika.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende kwenye ajiza za nje. Mhe. Waziri alipokuwa anasoma alitwambia kuna ajira za nje 498. Niipongeze tu serikali kwa kupata ajira hizo kila mmoja aliyekwenda huko ana familia yake naamini watakuwa wanafaidika kwa njia moja au nyengine. Lakini Mhe. Waziri ajira hizi zina mitihani kidogo kuna watu wanaondoka Zanzibar wanachukuliwa wanapelekwa huko kwenye nchi ambazo wanakwenda, lakini hatima yake wakifika kule wanapata udhalilishaji mkubwa sana na wengine huwa wanarudi baada ya miezi 2, baada ya miezi 3, wengine baada ya mwaka mmoja kabla ya ule muda ambao walitegemea wakae kule haufikii. Na hii zaidi kwa upande wa kinamama, maana yake wenzetu wanaweza wakachukuliwa hapa anaambiwa anakwenda kupata ajira huko anakokwenda lakini hatima yake atategemea yeye kuwa atakwenda kufanya kazi ile kwenye nyumba moja. Lakini akiondoka akifika huko anatakiwa afanye kazi kwenye nyumba 4 kwa siku moja, kuanzia usiku kuna nyumba anakwenda kufua nguo, akoshe watoto, akoshe masufuria, awekee watu chakula aondoke ende kwenye nyumba nyengine kwenda kufanya kazi kama hizo.

Kwa hivyo wananchiwetu wanapata tabu sana wanaokwenda huko, akiondoka hapa anategemea kuwa nitakwenda kule nitapata ajira nitakuja kujikwamua na huu umaskini. Lakini hatima yake anakwenda kule anakutana na mazingira magumu sana, wanaowapeleka watu hawa ni wafanya biashara ninaamini wana *percent* yao ambayo na wao wanapata.

Niombe sana anapotokezea mtu kutaka kupeleka watu basi ufanywe uchunguzi mzuri na hiyo kazi ambayo mwananchi wetu anakwenda kupewa kule kwa sababu tuna mabalozi wetu wapo huko nchi za nje basi wafanye kazi nzuri ili kuhakikisha watu wetu kazi wanazopata hawendi kudhalilika.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ajira za ndani. Serikali ina nia nzuri ya kutoa ajira na sasa hivi kuna Tume ya Utumishi Serikalini. Kuna kipindi kiasi miezi sita nyuma ilitangazwa ajira kwenye eneo la Chuo cha Kilimo Kizimbani. Ajira zile tulitegemea zitakuwa 26 lakini bahati nzuri waliokwenda kuomba kazi karibu elfu moja na ajira ziliopo pale 16. Kuna wazee ambao wanasomesha watoto wao kwa muda mrefu sana na wazee hao maskini sana, hatima yake wale watoto wanakuwa na usumbufu mkubwa wa kupata ajira.

Ajira hizi zikitoka 26 sisi tuliomo ndani, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na wengine wanapeleka vimemo vyao kwenye Tume ya Utumishi, wale watoto wao ndio wanachukuliwa. Hatima yake yule mzee maskini ambaye kasomesha mtoto wake mpaka kufika Chuo Kikuu siku nyengine alikuwa na vigombe kauza, mbuzi wake kishamba chake kauza mtoto wake anaendelea kubakia nyumbani ajira haipati. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri itakapotokea ajira sasa hivi zisiangalie watoto labda wa fulani au wa fulani, iangalie uwezo wa mtu ili vijana wetu wote tuhakikishe wale waliotoka kwenye familia za kimaskini, wazee angalau na wao wapate tamaa mzee mwengine akiona mtoto wake wa fulani ambae katoka kwenye familia ya kimaskini kapata ajira na yeye aweze kufanya kazi ya kumsomesha mwanawe kwa tegemeo lile la ajira.

Nikiondoka hapo Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye mfuko wa kujitegemea. Ni kweli serikali ina nia nzuri na tumepata takwimu nzuri ya watu waliopata mifuko hii ya kujitagemea. Lakini nimepata waswasi kidogo na Mhe. Waziri utakapokuja hapa basi utwambie, nimeambiwa fedha hizi ambazo zinatolewa mikopo wanapewa wafanyabiashara wakubwa, wanapewa wafanyabiashara wa maduka madogo madogo lakini pia wanapewa wakulima. Hoja yangu ambayo imenipa wasiwasi isije kuwa fedha hizi ambazo serikali inatoa kwa nia nzuri tu ya kuwaondoshea watu umaskini wanaenda kupewa wale wafanyabiashara wakubwa ambao wanaagizishia michele, sukari na mambo mengine. Wanakuja nayo hapa Zanzibar kila siku wanatupandishia bei isije kuwa wanatupiga kwa bakora yetu.

Kwa hivyo Mhe. Waziri, utakapokuja hapa utuambie ni wafanyabiashara gani wakubwa ambao wanapewa mikopo hii.

Nikiondoka hapo Mhe. Mwenyekiti, kwenye eneo hilo hilo hapa umesema pia wakulima wanapatiwa hii mifuko ya kujitegemea labda Mhe. Waziri utakapokuja hapa utwmbie ni wakulima wa wilaya gani au katika shehia gani au katika kilimo cha mpunga pengine wa kumwagilia, pengine wa mboga mboga au wa mihogo wamepatiwa mkopo huu. Atwambie atakapokuja hapa.

Mhe. Mwenyekiti, pia niwaponeze Mhe.Rais wa Zanzibar kwa kuwapatia pencheni hizi za shiling elfu ishirini kwa wazee. Huko nyuma nakumbuka kulikuwa na pencheni ya shilingi elfu tano. Sasa nataka nijue hili shilingi elfu tano kwa wale wazee waliokuwa wakipata elfu tano ndio wamegeuka wengine wanapata shilingi elfu ishirini au wale waliokuwa wakipata shilingi elfu tano mpaka leo wanapata ile ile elfu tano. Nimuombe kama wale waliokuwa wakipata shilingi elfu tano wanaendelea kupata shilingi elfu tano mpaka leo nikuombe Mhe. Waziri hawa angalau na wao wapate shilingi elfu ishirini kwa sababu sasa hivi shilingi elfu tano ukimpa mtoto wa shule wa chuo basi anakuhisi labda hujamsaidia lolote.

Ajira za watoto, Mhe. Mwenyekiti, suala la ajira za watoto sasa hivi ni mtihani kwa Zanzibar na mchangiaji Mhe. Sada alisema kuna watoto wadogo kabisa unawakuta wanapita wanauza dagaa, wanauza mihogo, wanauza na mboga mboga. Niseme suala hili ni gumu na Serikali lazima iliekee mkakati maalum, ikiwezekana askari huwa wanakaa barabarani kukamata vyombo vilivokuwa havina leseni na wizara yake nayo iandae utaratibu mzuri ikiwakuta watoto kama hawa wanaranda mitaani na sinia za madagaa na vitu vyengine wakamatwe, wapelekwe kwenye Wizara yako wahojiwe wazee wake waje pale na ikiwezekana hao wazee washtakiwe.

Mhe. Mwenyekiti, suala zima la vikundi vya SACCOS. Mheshimiwa kwa kweli sasa hivi zimekuwa ndio zinazosababisha wananchi wetu kupata kujiajiri. Unapoweka pesa zako kwa wingi na wewe siku ya kuvunja kile kikoba chenu cha SACCOS unapata pesa nyingi. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri hawa maofisa wake hawa pamoja na yeye mwenyewe ili kuwapa nguvu watu wenye vikundi hivi vya SACCOS na vikundi vya vikoba iwe mara kwa mara vikundi hivi vinatembelewa na viongozi wale wakuu wa wizara hii. Ninaamini wana kikundi wakisikia leo Mhe. Waziri anawatembelea watakuwa na hamasa kubwa sana na watategemea baba kaja au mama kaja basi watapata faraja.

Kwa hivyo nikuombe sana Mhe. Waziri uwe unaweza kuvitembelea vikundi hivi mara kwa mara ili wapate kuimarika.

Mwisho niseme tu kuwa juzi nilikuwepo Mwera nikaitwa na Sheha wa Mwera akanambia suala la ukamataji wa ng'ombe wamekuja kukamatwa Mwera. Lakini jana usiku pia nikaitwa eneo la Dole kuna mzee kanipigia simu niende alipofika akaniuliza suala la ng'ombe na kukamatwa. Nikamwambia kesho Mwenyezi Mungu akitujaalia tutakutana na Waziri wa Tawala za Mikoa nitamuuliza anaweza akanipa jibu sahihi. Yeye anasema kuwa wale askari wanakwenda kukamata ng'ombe mpaka maeneo ya Dole na maeneo mengine sasa ameniomba mimi nikampe jibu kuwa sasa hivi serikali inakataza kufuga mpaka maeneo ya shamba. Sasa mimi nikamwambia hili siwezi kukupa jibu, lakini naamini serikali haina mpango wa kuwakataza wananchi kufuga ng'ombe hata maeneo ya shamba.

Sasa ni vizuri baadae Mhe. Waziri labda atwambie ile mipaka ambayo wafugaji wetu wanatakiwa wafuge ili wasiwe na hofu na hasa kwa mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani, waondoke kwenye madrasa na maeneo mengine wasiwe na hofu kuwa ng'ombe wao wanaweza wakachukuliwa na askari na wakapelekwa maeneo ambayo wenyewe watapata usumbufu wa kuwapata.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niunge mkono hotuba hii ya Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani tukaweza kuikamilisha swaumu hii kwa hali ya uzima na afya.

Nikiingia katika mada Mhe. Mwenyekiti, ningeomba kwanza nianze na suala la ajira na vijana. Mhe. Mwenyekiti, suala la mpango wa ajira kwa vijana tunapolizungumza suala la ajira, ajira yenyewe ni neno moja, lakini kama utaliangalia lina maana kubwa na lina maana nyingi. Unapomwambia kijana kuhusu ajira yeye moja kwa moja atajua labda ameshapatiwa kazi ya kuajiriwa, lakini tufahamu kwamba suala la ajira lipo katika uwanja mpana na linatumika vikubwa. Vijana wetu wengi wao asilimia kubwa sana wana ukosefu wa ajira hususan wanawake, lakini pia tukiliangalia suala hili tunaweza tukalitatua kwa kupitia pande nyingi tu.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wanawake wanaweza kujiajiri wenyewe na wakaweza kukidhi mahitaji yao bila ya kubughudhiwa na mtu, bila ya kufanyiwa unyanyasaji wa aina yoyote. Kuna vijana ambao wana vipaji tofauti

ukitoa vya kuimba na kufanya mengine, kuna vijana ambao wana uwezo wa kufanya ujasiriamali wao wakaweza kupata kazi na wakaweza kukidhi mahitaji yao kwa kupitia ajira zao hizo.

Mhe. Mwenyekiti, namwambia Mhe. Waziri kama anafahamu kuna vyuo vingi hivi sasa, kuna Chuo cha Utalii ambacho kinasomesha vijana wengi, lakini kuna vyuo vya ufundi na nafikiri humo mna vijana wengi ambao wanakwenda katika vyuo hivyo. Sio kama kila kijana anapokwenda katika vyuo hivyo anafikiria kwamba yeye atapata ajira labda kwenye hoteli au kwenye chuo chochote, lakini kila kijana anakuwa ana malengo yake. Pia kjana anapotoka mule basi anakuwa yeye ana uwezo wa kufanya kitu chochote ambacho amekisomea. Vijana hao wanaweza kujiajiri kwa kupitia mikahawa, vijana hao wanaweza kwa kupitia viwanda, vijana hao wanaweza kujiajiri kwa kupitia hata mashamba. Lakini utakuta kikwazo anajiuliza je, vipi nitaweza kujiajiri, kwa sababu tu hana nyenzo ambazo zinamsababisha yeye aweze kujiajiri kutokana na ile elimu aliyonayo.

Kwa hiyo, ningekuomba Mhe. Waziri uwaangalie sana vijana kuhusiana na suala la ajira na ujasiriamali wao ambao wanao. Mhe. Mwenyekiti, wakihitaji kufanya hivyo watahitaji mikopo, lakini Mhe. Waziri amini kwamba kwenye suala la mikopo nako kuna kikwazo chake, lakini pia kwenye suala la vikundi pia kuna vikwazo vyake, kwa sababu tu kama kijana hatoweza kufanya labda kazi ile tuseme peke yake atahitaji kuwa na kikundi, lakini tuangalie kwamba pia hiki kikundi kinamlolongo mkubwa wa mpaka kuweza kusajiliwa na kuweza kupata ule mkopo. Kwa hiyo, Mhe. Waziri ningekuomba sana kwanza hili suala la usajili wa vikundi lingefanyiwa utaratibu mfupi ili vijana hawa wakaweza kuweka hivi vikundi vya ujasiriamali na kuweza kupatiwa mikopo, ili waweze kujiajiri wenyewe na waache kuilalamikia serikali juu ya suala la ajira.

Je, Mhe. Waziri hawa watoaji wa mikopo nao kweli tuseme wana lengo hili la kuwasaidia vijana au wana lengo la kuukandamiza huu umasikini zaidi. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu mtu wa mikopo atakujia, kuna wengine wanapita wenyewe vijiji huko ili waweze kutoa mikopo hiyo na wanatoa elimu hiyo ya mikopo, lakini utamkuta anakwambia kwamba mkopo unaoanza 400,000 pesa hizo anakwambia kurejesha yake kwa mwezi, lakini ukiipiga hesabu ile miezi ambayo anakupangia kulipa utakuta umelipa zaidi ya 700,000.

Sasa je, kweli huyu mtoa hii mikopo ana lengo la kuimarisha au ana lengo gani? Kama ana lengo la kuimarisha basi wajitahidi kwenye kutoa hii mikopo

ili waweze kuwasaidia vijana na waweze kuwasaidia kwenye suala lao la kujiajiri.

Mhe. Mwenyekiti, pia nitazungumzia suala la hawa watu wazima wa miaka 70 ambao wanapatiwa posho. Mhe. Mwenyekiti, lilipokuja hili suala kuna wahusika ambao walipita kwenye mitaa wakaanza kuwasajili hawa watu wazima, lakini kule sehemu ambayo niliyokuwepo mimi walikuwa wana maoni ambayo wanasema kwamba kuanzia miaka 70 ndio wazee ambao wanatakiwa kupatiwa hiyo pesa. Pia wakawa wana kikwazo kwamba kwa mzee yeyote mwenye mtoto ambae kaajiriwa serikalini hatoweza kuorodheshwa katika hiyo idadi, hata kama ana miaka 200. Ni kwamba walisahau kuwa huyu mtoto aliajiriwa kwenye serikali hii hii na yeye ana familia yake ambayo inamtizama kwa kila hali. Vile vile mtu yule yule hajui kwamba huyu mtoto ambae ameajiriwa kwenye serikali je, anamshughulikia ipasavyo huyu mzee.

Kwa hiyo, hili walishindwa kuliangalia na huko nje kuna malalamiko makubwa juu ya suala hili kwa wazee ambao hawakuorodheshwa katika orodha hii na wazee hawa nao ukiwaangalia wana kila sababu ya kuorodheshwa katika hii orodha ya kuweza kusaidiwa.

Kwa hiyo, ningekuomba Mhe. Waziri hili suala liangaliwe tena na kama kutakuwa kuna uwezekano basi lifanyiwe kazi upya kwa hawa wazee ambao walifikiwa na changamoto kama hizo za kuambiwa kwa kila mzee mwenye mtoto ambaye anafanya kazi serikalini hawezi kupata hiyo fursa.

Mhe. Mwenyekiti, pia nizungumzie suala la udhalilishaji kwa wanawake. Mhe. Mwenyekiti, hili suala lipo na kwa asilimia kubwa sana tunaona kwamba vijana wanawake tunadhalilishwa sana na baba zetu hawa. Hata kwenye jamii nyengine tunaona kwamba wanawake hawa wanadhalilishwa kwa sababu tu kama kijana mwanamke tuseme kama amemaliza skuli *Form Two* hana kazi ambayo anaifanya yupo nyumbani, basi huyu kijana atatafutiwa kila njia ili aweze kupewa mume aolewe, ili aondoke pale nyumbani asifanyie watu zogo. Lakini ukimuangalia kijana yule ana uwezo wa kufanya kila kazi ambazo zinaweza zikamnufaisha yeye pamoja na familia yake. Vijana wa kike kama mtu hataki labda na yale mambo anayotaka yeye kama hayo ya kumuozesha au kumsomesha anaweza akamtafutia sababu yoyote tu hasa ya kukamatiwa ili waozeshwe. Hapa hapa anapokamatiwa mtu inabidi akapelekwe hospitali kwa ajili ya vipimo.

Mhe. Mwenyekiti, kaka zetu hawa wanakula rushwa pamoja na madaktari na askari ili mtu huyu amdhalilishe wampeleke huko kwa nguvu.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri ningeomba kwa hisani yako ulisimamie zaidi suala hili la udhalilishaji kwa wanawake ambao wanakamatiwa na kuozeshwa, wakati mwengine inakuwa ile ni *issue* ambayo imechezwa na wale kaka au baba wa familia ilimradi tu wamuondoshe yule kijana katika macho yao na wampeleke katika suala hilo la ndoa na majukumu mengine. Wakati ukimuangalia kijana yule hajakuwa na hata upeo wa kufanya lile suala la ndoa.

Kwa hiyo, ningekuomba Mhe. Waziri kwa upande huu uwaangalie wanawake zaidi kwa vile na wewe ni mwanamke mwenzetu ambaye unayajua haya masuala na unayaona umuhimu wake na unayajua ugumu wake, tungekuomba sana utuangalie vijana wa kike hususan katika suala la udhalilishaji, lakini pia katika suala la ajira.

Mhe. Mwenyekiti, wanawake tunapata tabu sana na kazi zetu zinakuwa ngumu kutokana na hali zetu, akina baba wakati mwengine huwa hawatujali wala hawana muda hasa na wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika suala hili hili la udhalilishaji kwenye ndoa tunaona wanawake wengi wanaolewa na waume ambao hawastahiki, kwa sababu mzee anaweza akarubuniwa akishakuja kijana vile alivyo amevaa pengine nguo za kuazima amekuja pale na makoti na alivyo pengine mwenyewe amependeza. Kwa hiyo, baba huyo anaweza akashawishika na mtu huyu akampeleka mtoto wake bila ya kumjua yule mtu yuko vipi, na anapofika kule nyumbani yule kijana madhaliliko anayoyapata kule ni makubwa na hayastahiki katika jamii yetu.

Kwa hiyo, wazee wa kiume nao wawe makini sana na vijana wao wa kike hasa wenye umri mdogo kuwanyima fursa hata maneno ya kumwambia huyu mzee, ili mtoto huyu aweze kujitetea kwa njia yoyote basi hana uwezo wala hana sababu ya kujitetea, yeye kwa vile amezaliwa inabidi afate masharti ya baba.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Waziri uziangalie pia na ndoa hizi ambazo hazina msimamo, kwa sababu hizi ndoa zinakuwa hazina msimamo huwezi ukam-*force* tu kijana kwa vile umemuona amekaa tu pale haendi skuli wewe baba ndio mwenye uwezo wa kumsomesha yule na kumtafutia mahitaji yake mengine ili na yeye mwenyewe aweze kujitegemea, sio kwamba ndio akutegemee wewe tu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi zaidi mchango wangu mkubwa ulikuwa ni huo, kwa hiyo ningekuomba sana Mhe. Waziri utuangalie kwa jicho la pekee

wanawake na watoto na wazee, mimi nina hakika ukiweza kuyafanya haya utawasaidia sana jamii ya wanawake wa Zanzibar na Watanzania kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, tunamuamini sana Mhe. Waziri na tuko na wewe bega kwa bega kuhusu suala hili la udhalilishaji wa wanawake na watoto kwa kila hali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda niunge mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri asilimia mia kwa mia, zaidi hasa akiweza kuyatekeleza kwa ukamilifu haya ambayo yameandikwa humu kwa sababu ni mengi na ni mazuri na yanaenda na wakati.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi naiunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri nzuri asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia katika wizara hii muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake ambayo aliyotusomea, hotuba ambayo imejaa huduma kwetu sote kuanzia watoto wetu, vijana wetu pamoja na wazee.

Mhe. Mwenyekiti, kitu ambacho ninachotaka kuanza nataka nianze na kilio cha pamoja, na kilio hiki cha pamoja nitaomba kilio hiki kiwe kwa serikali nzima kisiwe kwa Mhe. Waziri tu peke yake. Kilio ambacho walikizungumza wenzangu Waswahili wanasema ukiona watu wazima wanalia basi ujue kuna jambo. Kuhusu zoezi la ukamataji wa ng'ombe, punda na mbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kwenye hotuba yake ameeleza analea watu wengi wakiwemo vikundi vya ushirika kama walivyozungumza wenzangu. Katika vikundi vya ushirika wamo wafugaji wa ng'ombe, punda, mbuzi na wengine. Sasa hili naomba serikali itumie busara sana na kwa kuzingatia wananchi wetu katika kipindi hiki wamepata misuko suko mikubwa sana.

Kwanza maradhi ya kipindupindu yameondoa shughuli nyingi sana za wananchi wanyonge, shughuli zao za kiuchumi. Kuna kina mama walikuwa wanapika chapatti sasa hivi hawapiki, walikuwa wanapika maandazi sasa hawapiki na shughuli nyengine zote ikiwemo samaki na wengine. Sasa shughuli haijakaa sawa tayari ng'ombe ambayo mtu anayakama maziwa angalau aweze kuuza kupata watoto nguo za sikukuu na viatu na vitu vyengine kwa hiyo imekuwa mtihani.

Sasa hili zoezi kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati kwa upande wa Wilaya ya Mjini hatutaki sote kumuona ng'ombe, mbuzi labda kuku katika Wilaya ya Mjini, lakini katika Wilaya ya Magharibi hili zoezi lazima tuliangalie upya, lazima tukae kama viongozi tukae shura maana yake hili tukae tubadilishane mawazo ili tutoke na jawabu muafaka. Kwa hapa hapa tu katika hadhira hii nadhani sio rahisi kuweza kupata jawabu muafaka, lakini tuna taratibu zetu tunaweza tukakaa tukaweza kutoa ushauri serikali ifanye nini ili kuwapunguzia machungu wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka na hilo nakuja katika suala zima la ajira kwa vijana. Mheshimiwa sasa hivi sio Zanzibar peke yake dunia nzima na tumeshahudia mpaka maandamano katika baadhi ya nchi vijana wanaibana serikali kudai ajira. Mimi nataka niwapongeze vijana wa Zanzibar, sijawahi kuona barabarani wakaingia na mabango kuharibu vitu vya watu kwa kufanya maandamano kuidai serikali ajira. Wanadai ajira katika njia za kidemokrasia, katika njia za kistaarabu. Kwa hiyo, nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri hebu uandae programu maalum kwa ajili ya vijana waliomaliza vyuo vikuu hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, vijana hawa waliomaliza katika vyuo vikuu wamesoma elimu mbali mbali, wengine wamesoma uchumi, wengine wamesoma masuala ya *finance*, wengine wamesoma masuala ya biashara, wamesoma taaluma mbali mbali hawa. Lakini vijana hawa baadae wanaangalia mazingira ukishakutana nao ujaribu kushauriana nao ili kuweza kuunda makampuni madogo madogo ya kuweza kuajiri vijana wenzao, wao vijana wa vyuo vikuu watakuwa wao wana fikra nini cha kufanya. Kuandaa miradi, kuandika katika taasisi za fedha lakini kuna vijana wetu ambao waliomaliza JKT ambapo waheshimiwa wengi wamekuwa wakilalamika vijana wanatoka JKT hawana ajira. Lakini vijana waliotoka JKT ukikaa nao mmoja mmoja kila mmoja ana ujuzi ambao amerudi nao, lakini hajui ujuzi ule akaweza kuji-*organize* vipi na wenzake ili kuweza kupata masuala ya ajira.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nilikuwa namuomba Mhe. Waziri namuachia kidogo atulie ofisini, akishatulia mimi nitamfata. Mimi nimeanzisha chuo cha *Vocational Training* jimboni kwangu, Chuo cha Amali kwa ajili ya kuwatafutia vijana ujuzi, lakini vile vile huku wakisubiri ajira kama hawajapata ina maana tayari ile ajira yake ujasiriamali watakuwa wameshaipata. Kwa hiyo, nitamuomba Mhe. Waziri tupate siku kwa nafasi yake nikamtembeze katika chuo changu kile kwa sababu pale nina mahitaji mengi. Tunahitaji vyarahani, tunahitaji vifaa vya umeme, tunahitaji vitu mbali mbali ambapo ule ufundi wa pale vijana ambao wameamua kuja kutafuta ujuzi.

Kwa hiyo, baada ya kuona naamini na yeye katika mihangaiko yake anaweza akapata taasisi mbali mbali ambazo za kuweza kutusaidia kupatia vifaa mbali mbali vya kuweza kuendeleza vijana wale. Lakini vile vile kuna ujenzi ambalo jengo lao kwa sababu sasa hivi tumejishikiza katika skuli ya *nursery* ambapo vijana wetu wa *nursery* kwa kweli wakati mwengine tunawa-*disturb* kwa sababu vijana wa *nursery* wanaposoma yale madarasa yao wakitoka hawatakiwi waingia watu wengine kutokana na vile vyao vya kuchezea. Sasa kuna mradi wa ujenzi pale tumekusudia kujenga jengo kubwa tu ambao halitochukua tu vijana wa jimbo langu, lakini watachukua na vijana kutoka katika majimbo mbali mbali katika kuweza kujiongezea na kujipatia ujuzi na vile vile kuweza kupata ajira.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri. Nataka nimpongeze Mhe. Waziri, aliyepita Mhe. Zainab Omar, kwa kuandaa programu nzuri ya wazee, lakini vile vile Mhe. Castico ambaye ni Mhe. Waziri, kwa kuja kuendeleza programu hii. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi Zanzibar suala la posho la shilingi elfu ishirini kwa wazee, kuna watu waliibeza elfu ishirini, lakini kwa kweli Zanzibar inatamba sasa hivi, inahitajika duniani na Mhe. Dkt.Shein amejadiliwa sana katika vyombo mbali mbali vya kimataifa ikiwemo *BBC, CNN* na vyombo vyengine katika kuzungumzia ile shilingi elfu ishirini kwa wazee. Na wao wamesema hili ni jambo kubwa sana, katika nchi masikini ambayo uchumi wake haujitoshelezi, lakini imeweze kuwafikiria wazee wao waliowazaa, kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, kupitia hili jambo mlilolifanya naamini Mwenyezi Mungu atashusha baraka nyingi na nchi yetu itapata uchumi mkubwa ili wazee hawa baada ya hii elfu ishirini basi hapo baadae ifike mpaka laki mbili.

Kwa sababu hii bajeti ndogo uliyokuwa nayo, amesikitika Mhe.Waziri, hajasikitika yeye tu na sisi tumesikitika baada ya kuona kitabu, bajeti ndogo lakini hiyo hiyo bajeti ndogo ameweza kutoa pesa nyingi kuwalipwa wazee. Sasa Mhe. Waziri, nchi yetu ikishapata uchumi mkubwa akapata bajeti kubwa, wazee hawa atawafikiria nini, atawafikiria mambo makubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, naipongeza Serikali, Dkt. Shein tunampongeza sana, kwa kweli uono wake huu umeweza kutoa taswira ya namna gani masikini akijipanga vizuri basi ile fedha yake anaweza akawasaidia mpaka masikini ambao wasiojiweza. Lakini vile vile nataka nikupongeze Mhe. Waziri, kwa kuendelea kuwatunza wazee wetu wa Sebleni, kwa kweli Zanzibar inaendelea tena kupata sifa.

Mhe. Mwenyekiti, ulikuja msafara kutoka Namibia safari moja, wakaja wakauliza, tena wao walikuja kutufundisha sisi programu za hifadhi za wazee, walipokuja wakatukuta kumbe sisi tulitangulia sana, wakasifu sana kumbe wakasema huyu aliyeanzisha jambo hili kwa kweli ni mtu ambaye alikuwa na upeo mkubwa sana.Kwa hiyo, Mhe. Waziri, nakuomba wazee wale uendelee kuwaenzi ili maisha yao yaendelee vizuri pale.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine jambo ambalo ni habari ya mjini. Mhe. Mwenyekiti, suala la uzalilishaji wa watoto kwa kweli Mheshimiwa, suala hili lazima tulikemee tena tulikemee kwa sauti kubwa sana. Mhe. Mwenyekiti, mimi niliwahi kwenda Pemba na Kamati yangu, kipindi hicho Kamati ya Kusimamia Afisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Nilitembelea kule katika *Marcuz* ya Olo Kianga, wale *Maustadh* waliokuweko pale walitupa orodha ya watoto zaidi ya mia moja na ishirini, orodha ya watoto tayari wamepata udhalilishaji katika maeneo mbali mbali, tena watoto wadogo sana na wakatuomba sana Waheshimiwa, tungeni sheria kali ambazo zitaweza kupiga vita udhalilishaji wa watoto.

Mhe. Mwenyekiti, jana nilikuwa nasikiliza ule mjadala ambao na mimi niliingilia kati kidogo alouzusha Mhe. Simai. Mheshimiwa, suala hili tusilifanyie masihara, kama nilivyosema jana sheria tunazo nyingi tena Zanzibar tuna sheria nzuri sana, bado naomba wale ambao wanaoshughulikia utekelezaji, usimamizi ndio sisi, wale watekelezaji wa hizi sheria watusaidie sana kumsaidia Mhe. Waziri, ili aweze kuondoa hili tatizo la udhalilishaji wa watoto, watoto wetu leo hawana raha, hawana furaha, leo hata mzazi anakwenda kazini akirudi kwanza *astaghfirullahi lladhim*, mpaka ampekue pekue mtoto, haya kwa kweli hii tumeshafikia *stage* mbaya sana, na katika maeneo ambayo Mhe. Mwenyekiti, ambayo yaliyoharibika sana ni maeneo ya Kaskazini; - Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba.

Sasa pia naomba Mhe. Waziri, hebu fanya utafiti huku Kaskazini watu wa Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba kuna tatizo gani ambao watu wazima wanafika pahala akili zinawatoka mpaka kuwadhalilisha watoto wadogo, lazima tufanye utafiti. Kwa sababu haya mambo tusifikirie tu masihara, tuangalie huu ukanda. Kwa sababu ukiangalia katika ile takwimu utakuta ukanda huu kwa kweli umeharibika sana katika uzalilishaji wa watoto.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine suala la mikataba ya ajira. Mhe. Mwenyekiti, hili bado limekuwa donda ndugu, hili ni tatizo kubwa, waajiriwa wengi katika hasa sekta ya mahoteli.Mhe. Mwenyekiti, mahoteli ya kitalii, Serikali yetu kwa nia njema kabisa imeweza kuwakaribisha wawekezaji hasa katika setka ya

utalii, lakini wengi wao bado wanawafanyisha kazi wafanyakazi bila ya mikataba ya ajira, wanawafanyia ujanja mtu akishakaribia ule muda wa sheria wanawaondoa.

Leo wafanyakazi wa mahoteli Mhe. Mwenyekiti, wamekuwa kama ni watu wa *part time*, kila msimu *season* ikimaliza, *season* inayokuja kijana yule aende akaombe kazi tena, haya sio maisha.Mhe. Mwenyekiti, vijana wetu hawa wamejiajiri na sio kama wamejiajiri, wameamuwa kuajiriwa katika sekta ya utalii ili waweze kuendeleza familia zao. Sasa ikiwa kila mtu na kila ikishafika mwaka ukimaliza *season low* ile wafanyakazi wanapunguzwa na wakirudi tena mtu hana uhakika wa kuweza kupata kazi yake. Kwa hivyo, hili nilikuwa nakuomba sana Mhe. Waziri, vile vile, ulishughulikia.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ajira ya watu wenye ulemavu. Mhe.Mwenyekiti, watu wenye ulemavu, nafikiri hii lugha iko sahihi. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kuna haya maazimio ya kimataifa yanaelezea kabisa, lakini vile vile na sisi tumetunga sheria hapa Mhe.Mwenyekiti, na vile vile, tuliagiza kwamba katika kila ajira inapofanyika kila Wizara lazima katika zile ajira waweze kuajiriwa watu wenye ulemavu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia katika vitabu vyetu ajira zinazotoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kweli ni aibu, hatuwatendei haki watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, ninatoa wito na Waheshimiwa, wenzangu ninawaomba katika bajeti inayokuja bajeti hii tuwasamehe, katika bajeti inayokuja Mawaziri wote watakaokuja hapa kila mmoja katika kile kifungu cha *human resources* tuhakikishe tunazuiya fungu mpaka watuambie wameajiri watu wenye ulemavu wangapi.

Mhe. Mwenyekiti, watu wenye ulemavu sasa hivi wamesoma, watu wenye ulemavu wana ujuzi, hakuna sababu ya ndugu zetu hawa wasiweze kupata ajira na tukiwapatia ajira hawa tunapata fungu kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu hawa wengine wenye maguu na maguvu yao watakwenda kubeba mizigo na kufanya kazi nyengine, lakini watu wenye ulemavu masikini ya Mungu watafanya kazi gani? Kwa hiyo, naomba sana na Waheshimiwa, hili nafikiri tulieke katika kumbukumbu na Mawaziri wanatusikia na Mhe. Waziri Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, anatusikia, atawaambia Mawaziri kwamba, Baraza linalokuja Waheshimiwa, tayari wameshachonga ukali na sisi tunaitwa '*watchdog', 'watchdog'* maana yake mbwa mkali unaona mambo mengi na unafichua mambo mengi.

Kwa hiyo, haya tunayoyasema hapa ndio kazi yetu '*watchdog'* maana yake kazi yake kufichua. Kwa hiyo, nataka katika bajeti inayokuja Wizara zote tuhakikishe kwamba katika ajira katika Wizara zote za SMZ tuhakikishe watu

wenye ulemavu lazima wameajiriwa, *otherwise,* hapa fungu la *human resources* tutakuja kulizuia, tutazuia mshahara wa Waziri ili asende ofisini mpaka tuhakikishe watu wenye ulemavu wameajiriwa.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia kabla hujanambia nimebakisha dakika mbili. Sheria za Kazi. Mhe. Mwenyekiti, nataka Mhe. Waziri, aje anambie mkataba wa kimataifa, Sheria za Kazi unasema masaa mangapi ya kufanya kazi. Leo Zanzibar hii hii tena kuna Taasisi za Serikali watu wanafanya kazi masaa kumi na mbili, kama masaa kumi na mbili, ina maana ni masaa ambayo yako katika mkataba wa kimataifa, mimi *layman* ninajua masaa manane, lakini Waziri atakuja kuniambia masaa mangapi. Je, haya masaa ya ziada, yaani masaa manne wanafanyiwa nini, ina maana hapo lazima kuwe kuna *incentive* ya kuweza kumlipa mfanyakazi masaa ya ziada.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, Serikali imetoa tamko katika kubana matumizi na vile vile, nilisema kwamba mtakata baadhi ya posho mbali mbali, lakini bado Mhe. Waziri, hili naomba usimame kidete, najuwa wewe ni Waziri lakini unapokwenda kwenye *cabinet* bado utetee Taasisi yako, unapokata maposho mbali mbali, Mhe. Mwenyekiti, kuna maposho mengine yana maelezo, maposho yamaziwa, mfano kuna watu kazi zao inabidi wapate virutubisho, ina maana maposho haya na maposho mengine ambayo muhimu, kuna maposho kama hayo baada ya saa za kazi, kuna maposho nyeti, kuna watu wana kazi nyeti sana, kuna posho, sasa posho zile mkija mkizikata Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wafanyakazi hawa tutawavunja moyo na watashindwa kufanya kazi zao kwa vizuri na kwa kweli hata uwajibikaji wao utakuja kuwa si mzuri.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema namalizia hili la mwisho la suala la ajira za nje. Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara, lakini vile vile nakuomba sana Mhe.Waziri, hebu katika mipango yako ya kazi hebu andaa safari ya Qatar, nenda Qatar na kule kwa bahati nzuri mimi niliwahi kupata msafara na nikenda tukakutana na yule Mkurugenzi wa Uwekezaji wa pale, lakini vile vile katika mambo ambayo tuliyoyazungumza kule katika masuala ya kuwatafutia ajira vijana wetu wakatuahidi na kutwambia kuna ajira alfu tano zilitengwa kwa Tanzania wakati alipofanya ziara Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano kipindi kile Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda.

Kwa hiyo, ajira zile zipo elfu tano na mgao wake basi tuliambiwa Bara ajira zao mgao wao ni ajira elfu tatu na Zanzibar ni ajira alfu mbili hizo ziko *official.* Kwa hiyo, kazi moja iliyotakiwa ni nini, Taasisi zinazotafutia watu ajira zilizokuwepo Zanzibar na zilizokuwepo Tanzania Bara waende kule

wakazungumze na ile Taasisi inayohusiana na masuala ya ajira kuangalia ufungaji wa mikataba. Lakini suala hili Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri, usiwaachie Taasisi binafsi kwanza, nenda wewe mwenyewe ukazungumze na Mkurugenzi anayeshughulika na vitega uchumi na mambo mengine ya ajira ili akuthibitishie zile ajira, sasa wewe ukirudi ukae na Maafisa wako ili sasa kuangalia utaratibu na mafunzo au kuwapatia utaratibu kwa zile Taasisi zinazotoa ajira za nje ya nchi zilizokuwepo hapa Zanzibar ili waende wende wakatohoe ajira zilizokuwepo kule.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili nampongeza sana Mheshimiwa, mwenzetu mstaafu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kwa kweli amefunguwa Kampuni yake, sasa hivi inafanya kazi vizuri na nakuombeni Waheshimiwa, mimi tayari nimeshampelekea vijana wangu, tayari anaanza kupeleka vijana, lakini hao vijana anaosafirisha wanatakiwa wawe na ujuzi maalum lakini na lugha japo kidogo ya Kiingereza cha kuombea maji ya kunywa kule unapofikia kule. Kwa hiyo, ninampongeza sana aendelee, basi namuomba tu Mhe. Waziri, bajeti yako mimi hii siitoi hata nusu shilingi, nakupa asilimia mia moja, lakini nakuonea huruma kwa bajeti yako na ninaamini mwakani tutakusaidia na Mhe. Waziri wa Fedha, hayupo lakini Mhe. Waziri Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais yupo ili kukuongezea fedha uje utuhudumie sisi na wake zetu pamoja na watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja asilimia mia moja kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Shaurimoyo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hamza, sasa anafuatia Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi na Mhe. Mihayo na pia, namuomba Mhe. Zaina Abdalla Salum, ajitayarishe akifuatiwa na Mhe. Wanu.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuwa miongoni mwa wanaochangia mada hii ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wanawake na Watoto. Kwa kweli mimi niseme Mhe. Hamza, kayazungumza yale ambayo nilitaka kuyazungumza na siwezi kusema kanifilisi kwa sababu mazungumzo yanayozungumza au ajenda inayozungumzwa mmoja anaweza kuzungumza hiyo na mwengine akazungumza hiyo hiyo kwa pande nyengine na ikafahamika pia. Kwa hiyo, nategemea sana sitorudia yale yale aliyoyasema Mhe. Hamza, bali nitaeleza kivyangu. Na kwa kupitia kwako nampongeza sana Mhe. Hamza, kaeleza vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa kweli hii Wizara ni Wizara ya jamii, ni Wizara ambayo jina

lake hili ni Wizara inayokusudia kupunguza au kuondoa kabisa umasikini katika nchi yetu. Sasa umaskini katika nchi yetu husababishwa na mambo mengi sana, inafaa Wizara yetu hii iyajue na inayajua lakini iangalie kwa kina iyafanyie utafiti iyapatie ufumbuzi.

Mhe,. Mwenyekiti, mambo yenyewe ninaweza kuyataja hapa; kwanza kuna mambo ya kiuchumi yanasababisha umasikini, kuna mambo ya kijamii yanasababisha umasikini, kuna mambo ya kisiasa pia yanachangia, kuna hisia za watu wenyewe, yaani *attitudes* zao au zile *mind set* zao, kuna sera na mipango na utekelezaji wake, kuna matumizi ya nyenzo kwa maana ya *resources* nazo pia zinachangia katika umasikini, kuna maarifa, yaani ule ujuzi *skills* za watu wenyewe, halafu kuna ukosefu wa nafasi za kuwasaidia kupata njia za kuendesha taratibu za kujipatia kipato, hayo ni mambo kwa kweli yanasababisha.Sasa Wizara hii inatakiwa matatizo haya iyatatue.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia katika jamii zetu, huko majimboni, wilayani huko kadhalika, kwa kweli kuna watu wengi, vikundi vingi sana vinahitaji kuwezeshwa, uwezo wa kuwezesha ni mdogo kifedha, lakini uwezo wa kuwezesha watu wakaweza kupata muelekeo upo mkubwa tu, ni kuwasomesha, ni kuwashauri na hata kuwapatia au kuwaeleza mahala ambapo wanaweza wakapata mahitaji yao. Kwa kweli katika majimbo huku kuna vikundi vya ushirika vingi sana, vingi kweli, vingine vimesajiliwa na vingine havijasajiliwa, vilivyotajwa hapa ni vichache lakini nadhani kwa mwaka huu ambao umemalizika mwaka jana, lakini viko vikundi vimeshaanza siku nyingi na vinafanya kazi na Wizara hii inavijua, kwa sababu tumeshirikiana nao sana katika kuvipatia zawadi na kuviwezesha vikundi vingi tangu enzi za Maalim Haroun siku zile alipokjuwepo katika Wizara hii kule Kaskazini nakumbuka tuliwawezesha vikundi visivyopunguwa hamsini nadhani kama sikosei ili viweze kwenda kufanya kazi na vikundi vile vipo na vinafanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kinachotakiwa vikundi kama vile ni kuvipitia na kuvipa ushauri ili viendelee kufanya kazi za ujasiriamali kwa lengo la kukuwa, sio pale pale walipo tena, vikundi hivi lazima vikuwe, washauriwe pia waweke fedha benki na sio hao tu hata hawa wajasiriamali wengine ambao tunawawezesha wenye vikoba, wenye visanduku, wenye *SACCOS*, wote ni vizuri wafunguwe *account* benki, kwa maana wakifunguwa *account* benki Wizara inaweza ikawawezesha pengine, lakini pia mabenki inaweza ikawapatia mikopo wakaweza kufaidika kutokana na mikopo hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa narudi tena kwenye Majimbo. Kwenye Majimbo nimesema kuna watu wengi wanaohitaji kuwezeshwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Dkt. Makame, sita kidogo nampisha Naibu Spika, ili aendelee na utaratibu. (*Makofi*)

(Hapa Mhe. Naibu Spika, alikalia kiti)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Dkt. Makame, endelea.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Naibu spika, nimesema kwamba kwa kweli huko Majimboni viko vikundi vingi sana ambavyo vinahitaji kuwezeshwa, kuna wazee na wazee ndio hao wanawezeshwa kupatiwa hizo pesa ambazo zimekusudiwa kupatiwa ili waweze kujikimu, lakini pia kuna wazee ambao hawatawezwa kuorodheshwa kwa sababu hawatimia masharti. Kuna mtu miaka arubaini keshakuwa mzee kabisa hawezi kufanya lolote, wapo hao, kuna miaka hiyo sabiini wao tuseme ndio hivyo, pengine kuna mtu ana miaka sabiini anajiweza vizuri naye. Sasa uzee huu unakuja kutokana na maradhi labda, sasa tuwatizame, tutizame wote ambao wanastahiki kuwezeshwa basi tuwawezeshe kwa njia moja au nyengine, hata kwa kuwaandikia miradi sio vibaya, kama fedha hakuna kwenye wizara husika basi waandikiwe miradi ili waweze kuwezeshwa. Kwa sababu hii wizara sio kutoa pesa inazopata ruzuku tu ya serikalini bali hata wao wakiweza kuandika miradi kuwasaidia basi pia inafaa.

Sasa kuna kundi la watoto ambao pia wametajwa kwenye wizara, kuna watoto ambao kwa kweli wazee wao hawana uwezo wa kuwasomesha na ni watoto mahodari kabisa, wanalazimika kubaki nyumbani kwa sababu ya tatizo hilo la uwezo wa wazee. Sasa nasema wizara husika ni vizuri ikaliangalia sana suala hili na wale nao wawezeshwe ili waweze kuendelea kupata elimu ili nao waje wawe miongoni mwa raia, ama wajasiriamali, ama wafanyakazi serikali au vyovyote itakavyokuwa. Kwa sababu huwezi jua hao hao pengine unaweza ukamtoa kijana huyo ukamsaidia akasoma akaja akawa *pilot*, akawa kapteni wa meli, *engineer*, daktari au akawa chochote. Kwa sababu hawa madaktari na wengine hawatoki hewani bali wanatoka huko huko. Kwa hivyo, tukiweza kuwasaidia basi naamini kabisa tutaweza kuondoa tatizo hili la umasikini.

Nikienda kwenye kitabu hiki kidogo ukurasa wa 22, Mhe. Waziri, amesema kwamba; "wajasiriamali waliojiunga na kituo kupitia vikundi vilivyoanzishwa wamesaidiwa kuanzisha kampuni 17". Hongera sana. Kampuni hizi za majaribio; mbili kati ya kampuni hizo zimeweza kupata mafanikio na kufungua ofisi nje ya kituo na kujiajiri, kampuni 9 tayari zimepata mafanikio lakini bado zipo kituoni.

Halafu akasema mwisho kwamba, kuna kampuni sita zimefeli. Sasa ukichukua 17, sita zimefeli, maana yake ni karibu asilimia arobaini na zaidi zimefeli, hii ni *failure* kubwa sana. Sasa mimi nashauri tu kwamba, nadhani iko haja kwanza hivi vikundi tunavyotaka kuviwezesha kuvifanyia utafiti wa kutosha kama vinaweza kuendelea, tukishahakikisha kwamba vinaweza kuendelea basi hapo ndio tuanze kuvipa hizo nyezo za kuendelea. Kwa sababu vikundi vyenyewe vitakapojiweza kabisa kabisa vinaweza hata kuja kuwawezesha na wenzao ambao wako mitaani na wao hawa wanajuana, wanajua huyu tumuwezeshe vipi, tumuwezeshe kwa kitu gani, tumpe nini ataweza. Kwa hivyo, nadhani ufanyike utafiti wa kutosha wakati wa kuchagua vikundi ambavyo tunataka kuviendeleza.

Jengine ambalo ningependa nilizungumzie hapa leo kwa sababu hii ni Wizara ya Uwezeshaji basi uwezeshaji una mambo mengi, umuwezeshe mtu aweze kupata mambo yote ambayo yatamfanya awe katika hali ya utulivu na afanye mambo yake kwa ufanisi.Miongoni mwa mambo ambayo ataweza kuyapata kwa wakati anapoyataka ni ya maji. Najua kuna wizara ya maji, lakini wizara hii sasa madhali kuna suala la uwezeshaji basi tusaidiane uwezeshaji,wawezeshwe wananchi waweze nao kupata maji. Uwezeshaji ichangie kwa sababu maji peke yake haiwezi kufanya hii shughuli.

Jengine ninalopenda kuchangia ni kuhusu huu udhalilishaji. Udhalilishaji Mkoa wa Kaskazini tumeushughulikia, hata mimi ni miongoni mwa watu ambao tumeshughulikia na kuna *research* kule ilifanyika, imetoa mapendekezo mazuri tu ya namna ya kupiga vita udhalilishaji. Miongoni mwa sababu za udhalilishaji zilizotajwa na hiyo kamati iliyofanya utafiti huo ni umasikini, tamaa tu za watu wenyewe wanaofanya mambo hayo na hata ikaingia kuwa kuna hasada. Sasa nadhani iko haja na sehemu nyengine zote zifanye utafiti kama uliofanywa Kaskazini ili tatizo hili lipatiwe ufumbuzi, bila ya hivyo ni tatizo kubwa na litaendelea kuwepo. Kwa sababu jamii yetu ndio hiyo hiyo na inaendelea kuwepo jamii hiyo, vitendo vinafanywa na hao hao, kwa hiyo, si rahisi kabisa kuzuwia moja kwa moja ghafla, lazima pafanywe utafiti wa kutosha wa kina kabisa zipatikane sababu halisi hasa zinazosababisha udhalilishaji wa kijinsia.

Hizo kesi zilioko Mahakamani ambazo zinakwenda sasa hivi zifanyiwe haraka ili zipatiwe ufumbuzi na zile ambazo hazijafikishwa Mahakamani basi zifikishwe haraka. Lakini pia ningeshauri kwamba pamoja na juhudi yote hii tunayoifanya nadhani iko haja ya kufanya utafiti hasa kama nilivyosema mwanzo utafiti wa kwa nini jambo hili linaendelea. Moja katika sababu kubwa inawezekana ikawa hizo kesi kuwa zinaachiwa, hata mtu akifanya anajua mimi nikifanya hata nikikosea na kufanya kitu fulani nitaokoka. Kwa hivyo,

anaendelea kufanya ujambazi, kwa sababu huo ni ujambazi, wewe mtoto mdogo ukamuharibu, huo ni ujambazi ambao hauna mfano.

Baada ya kusema hayo sitaki niende mbali sana kwa sababu hii hotuba imeeleza vizuri, nadhani na kwenye bajeti huko kuwe vizuri. Kwa hiyo, niseme tu kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, lakini nasisitiza kuwa haya aliyoyapendekeza Mhe. Hamza Hassan Juma, na haya niliyopendekeza mimi, nadhani tungeyachukulia kwa nguvu zote, basi tunaweza tukaondoa matatizo makubwa sana ya umasikini katika nchi yetu.

Baada ya kusema hayo narudia kwa kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Dkt. Makame Ali Ussi, mchangiaji anayefuatia ni Mhe. Mihayo Juma, baada ya Mhe. Mihayo, atafuatia Mhe. Tatu Mohammed Ussi, hayupo.

UTARATIBU

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, naomba mwongozo wako, wakati Mwenyekiti anakuachia kiti aliacha mchangiaji anayefuatia baada ya Mhe. Mihayo Juma, akifuatiwa na Mhe. Zaina Abdalla Salum, badala ya hapo nikifuatia na mimi. Naomba mwongozo wako.

Mhe. Naibu Spika: Sawa tuendelee hivyo, ina maana baada ya Mhe. Mihayo, atakuja Mhe. Zaina Abdalla na baadae atakuja Mhe. Wanu Hafidh Ameir. *(Makofi)*

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana nami kwa kuniona au kunipa fursa ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Kwanza kabisa nitumie fursa hii kuweza kumpongeza Mhe. Waziri, kwa hotuba yake nzuri ambayo ina maslahi ya kuwatetea Wazanzibari wote kwa ujumla bila ya kuwabagua.

Mimi naomba niende moja kwa moja kwenye mada ama mchango wangu kwa wizara hii.Nianze na suala la ajira kwa vijana. Tunaona na tunatambua fika dhamira kubwa ya serikali ni kuhakikisha raia wake wanaweza kupata ajira kwa namna moja ama nyengine, lakini pia inatambua kabisa taifa hili bado lina asilimia kubwa ya vijana, kwa maana linahangaika kadri iwezekanavyo vijana hawa kwa namna moja au nyengine nao wapate nafasi za ajira, ima iwe katika taasisi za serikali au nje ya taasisi za serikali.

Mhe. Naibu Spika, lakini hapa wizara hii inajitahidi sana, lakini mara nyingi nafasi hizi zinavyotengenezwa hasa katika taasisi zisizo za serikali, vijana hawa inakuwa hatuwafanyii *follow-up* kwa kujua kule walikokwenda kama kweli bado wapo katika maeneo yale ama hawapo. Kwa kutoa mfano nichukulie katika tasnia nzima ya utalii. Kama ambavyo Mhe. Waziri, ametueleza hapa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 wizara yake iliweza kutoa elimu kwa vijana takriban 264 katika masuala ya utalii. Sasa ni vyema serikali kwa kushirikiana na wizara hii ikawa inatumia utaratibu angalau wa kutizama wale watu waliokwenda katika maeneo ya mahoteli kama kweli watakuwa wamepewa mikataba ya kufanyia kazi ama laa. Kwa sababu kufanya kazi bila mkataba kuna manyanyaso makubwa sana na taifa letu linategemea sana utalii.

Mara nyingi vijana hawa wanapoajiriwa katika maeneo ya mahoteli wanakuwa wakihudumia katika maeneo yale kwa kipindi cha msimu mmoja mmoja tu wa utalii, kitu ambacho hakitoi uhakika wa maisha yao hasa kwa kuwepo katika maeneo yale. Sasa kwa kufanya hivi tunakuwa hatuwatendei haki ama ile dhamira njema ya kuwasaidia vijana hawa kupata nafasi za ajira tunakuwa hatujaweza kuikamilisha vizuri kama inavyotakiwa.

Pili, niende katika sekta ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Tunatambua sana Mhe. Waziri, sehemu hizi ni sehemu nyeti katika taifa letu. Tunapozungumzia uchumi wa taifa unatoka katika maeneo mengi, tukizungumzia kuwasaidia watu kiuchumi kunatokana pamoja na wale ambao wanatoka kwenye *SACCOS* na katika vikundi vya ushirika, lakini wale wote ambao inawezekana wakaunda makundi kwa dhamira ya kujikwamua kiuchumi kwa namna moja ama nyengine.Tuipongeze serikali maana imekuwa ikitumia jitihada kubwa kwa kuweza kuwasaidia mtaji watu hawa kuweza kufanya shughuli zao ili kupata kujikwamua kwa namna moja ama nyengine ili nao kuweza kuipunguzia mzigo serikali pindi wakitaka kuwapa nafasi za ajira.

Sasa tunapofanya hivi kuwasaidia watu katika makundi yao ama katika *SACCOS* zao au vikundi vya ushirika tunakuwa tumeweza kuipunguzia mzigo mkubwa serikali. Inawezekana kwa kufanya hivi tukawa tumeweza kutengeneza na kutoa fursa nyingi kwa nafasi za ajira kwa wananchi wetu.

Vile vile, nimuombe Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwamba maombi haya ya wananchi wanaokuja kutaka kuwezeshwa kwa mujibu wa vikundi vyao ni mengi sana, wengi wamekuwa hawapati fursa ile kama ambavyo takwimu zimetuonesha hapa. Kwa sababu wapo watu wengi walioweza kufika katika wizara yake ili kupata kuwezeshwa, lakini bado hawakuwa wakipata majibu mazuri ama msaada wa kutosha ili nao kuweza kupata mitaji na kuweza

kujikwamua kiuchumi na kuipunguzia mzigo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, naomba nizungumzie suala jengine ambalo kama wazungumzaji waliopita wamekuwa wakiligusia ni suala zima la udhalilishaji wa watoto. Kama tunavyofahamu mazingira ya taifa letu la Zanzibar ni madogo sana, lakini suala zima la udhalilishaji wa watoto ni kubwa, jambo ambalo hata taasisi za kimataifa zinapopata taarifa hizi zinakuwa zinashituka sana. Pamoja na yote bado watu wanaofanya matendo haya ya kudhalilisha watoto kumekuwa na jitihada ndogo sana za kuweza kuwashughulikia na kuwawajibisha, hatujui kuna kigugumizi gani hapa baina ya watu hawa ambao malalamiko yao yapo katika sehemu stahiki za serikali.

Sasa mimi wito wangu ni kumuomba Mhe. Waziri, pamoja na mfano wake kwamba kwenye kesi 49 ambazo zipo katika ngazi za Mahakama ni kesi mbili tu ambazo zimeshafikia ngazi za maamuzi. Si jambo zuri sana kulisemea lakini wakati mwengine linatia ukakasi kwa kuwa taasisi na nchi kama hii kwamba tukaweza kutoa hukumu za kesi mbili tu kwenye kesi 49, ni jambo ambalo linakatisha tamaa kwa upande mwengine, inakuwa kama tunahalalisha haya masuala ya udhalilishaji, maana mtu anafanya tukio au tendo baya kwa jamii, lakini hakuna msukumo wowote wa yeye kumuwajibisha au hakuna uharaka wa kuwajibishwa kama vile ambavyo inatakiwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa hili tuwaombe wenzetu wa serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Afya kuweza kusaidia Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja kupata baadhi ya vipimo kama vile vya *DNA,* ambavyo imekuwa ndio sababu pekee katika taasisi hizi ambazo zimekuwa zikifanya maamuzi haya. Kwa sababu jukumu hili liko kwa Mhe. Waziri, sisi leo tutasema, kesho tutasema na keshokutwa tutasema, tusipofanikiwa Mhe. Waziri, hili litakuwa linakufelisha wewe, maana dhamira ni kuhakikisha udhalilishaji huu katika taifa letu unapungua sana na kadri siku zinavyokwenda badala ya kupungua matendo haya yamekuwa yakiongezeka katika jamii zetu. Kwa maana hiyo, Wazanzibari wanyonge wamekuwa wakidhalilika sana maana wanaotendewa matendo haya ni wale ambao wako katika maisha ya kawaida.

Jengine hapa hapa kwamba ufuatiliaji wa kesi hizi umekuwa ni mdogo sana na hata wakati mwengine wale watendaji au maafisa waliokuwepo katika ngazi za wilaya wamekuwa hawana taarifa kamili za udhalilishaji unaofanywa katika wilaya zao. Sasa ni jambo ambalo limekuwa lina kigugumizi kwa namna moja ama nyengine, maana dhamira ni kwamba wakati mwengine unapohitaji

takwimu hizi iwe ngazi ya kwanza kuzipata kutoka katika ngazi ya wilaya, ukifika katika ngazi ya wilaya ukikutana na maafisa pale wanakwambia sina taarifa kamili labda nijaribu kwenda kwa sheha, kitu ambacho si kizuri sana. Ni vyema sasa na wao watendaji wakawa wanaweza kutumia fursa na wajibu wao ili kuwa na takwimu hizi katika hali nzuri tofauti na kwamba anakwenda mtu kutaka takwimu pale katika ngazi za wilaya kunakosekana takwimu halisi, unakuja unazipata takwimu za kitaifa ambazo zinatokana katika mikoa, ni kitu ambacho sio kizuri.

Pili, hapa hapa tunasema kwamba bado kama wizara na serikali tuna wajibu wa kuendelea kutoa elimu ya kutosha katika jambo hili la udhalilishaji wa kijinsia hasa kwa watoto hawa. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kuisaidia na kuweza kuihabarisha jamii yetu kwamba hiki kinachotokea si kitu kizuri na si kitu cha kuungwa mkono hata kidogo. Kwa sababu tunapoendelea kudhalilisha watoto hawa wadogo tunakosa kizazi chema huko baadae. Kwa sababu ukimfanyia kitendo kiovu mtoto mdogo anaharibika kisaikolojia, jambo ambalo litaharibu mwenendo wake mzima wa afya hasa katika maeneo ya kupata elimu na mambo mengine. Hivyo, tuwaombe wenzetu wa serikali tuongeze jitihada hii ya kuweza kuhakikisha watu hawa wanaweza kusaidiwa sana na kupunguza matatizo haya ya udhalilishaji wa kijinsia kutoka kwa watoto hasa kinamama.

Kwa sababu tunajua bado wapo baadhi ya watu wanakuwa na tabia za kuwanyanyasa wake zao kitendo ambacho sio kizuri, maana mwanamke si mtu wa kupigwa, ni mtu wa kupewa maneno matamu, mazuri na ni jambo ambalo linaweza kusaidia jamii yetu kwa ujumla kuweza kufika mbali.

Lakini jengine naomba nimpongeze Mhe. Rais Dkt. Ali Moh'd Shein pamoja na wizara yako kwa jumla kwa kuwa na dhamira ya dhati ya kuweza kuwapa wazee hawa stahiki zao za shilingi elfu ishirini kila mwezi. Mwanzo huu ni mzuri na tunakuomba sana Mhe. Waziri, jambo hili lina fitna kubwa sana, miongoni mwa mambo ambayo yanaweza yakakuadhibisha sana ni pamoja na pesa hizi za wazee, maana watendeji wetu hawa wakati mwengine wanakuwa si wote ambao wana dhamira ya dhati na muono wa Mhe. Rais. Sasa jambo hili linahitaji sana kusimamiwa kwa hali yoyote ile ili mradi stahiki hizi za wazee ziende kama hivyo ambavyo Mhe. Rais, amekusudia.

Lakini pia kama ambavyo kuna baadhi ya wachangiaji waliopita wamegusia kumekuwa na dosari mbili tatu katika stahiki hizi za wazee; wapo wazee ambao hawakuwa wakijua uhakika wa miaka yao ya kuzaliwa. Jambo ambalo walipokwenda katika uandikishaji wale waliokuwa wakiwaandikisha walikuwa wakiwakadiria tu umri wao. Sasa tukija tukitizama kigezo hichi cha miaka 70

na wapo watu wengine ukiwatizama *physically* unaona huyu ameshazidi hii miaka 70 na 80, lakini ukitizama kitambulisho chake kinakuwa kinaonesha kwamba ni mtu ambaye bado ana umri wa miaka 49 au 50.

Sasa tuombe sana wizara kwa busara ya hali ya juu ili kwa kuweza kunusuru janga hili la wazee waweze kupata stahiki zao kwa utaratibu uliokuwa mzuri, turudi tufanye tena utaratibu wa kuwatizama wale ambao wanakidhi na kustahiki kupewa stahiki hizi basi tufanye hivyo. Maana kwa kufanya hivyo, tutaweza kupunguza yale maneno na migogoro ambayo leo katika jamii imeshaanza kutoka na si kitu kizuri kama kusaidia wazee ambao wachache na wengi wakabaki.

Natambua sana jitihada zako Mhe. Waziri, utalisimamia hili kwa umakini mkubwa na nina imani kwa imani yako na nguvu zako hawa wazee wengi watanufaika na mchango wako hasa katika kiwango hichi ambacho Mhe. Rais, amekuwa ikikisemea.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, wakati Mhe. Waziri, anawasilisha hotuba yake na nikasikiliza kwa makini mawazo ya kamati nilitafakari lakini sikupata jibu. Hapa leo tunajadili Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, nimepata ukakasi mkubwa sana. Pamoja na kutambua kwamba suala zima la watu wenye ulemavu liko chini ya Afisi ya Makamu wa Rais. Lakini tukizungumzia suala zima la Uwezeshaji, maana kunako wazee hawa watu wenye ulemavu wapo, kunako Vijana hawa watu wenye ulemavu wapo, lakini kunako kina mama hawa watu wenye ulemavu pia wapo. Sasa nao hawa kupitia vikundi vyao wana kila sababu ya kupata neema ama stahiki ya kuwezeshwa kuwa katika Wizara hii ya Uwezeshaji.

Sasa nikuombe sana Mhe. Waziri, utakapokuja hapa katika majumuisho yako ni vyema sasa angalau ukatwambia katika kipindi hicho cha nyuma kilichopita wizara yako imeweza kuwezesha walemavu vijana kwa kiwango gani. Lakini wizara yako imefanikisha kutoa elimu kwa walemavu kina mama na wazee kwa kiwango gani ili kuweza kutoa ule mtangano wa ubaguzi, maana kwa kuwabagua hapa wazee tutakuwa tumewa-*isolate* kisaikologia na haitakuwa kitu kizuri, maana wazee hawa bado nao wanahitaji *equal treatment* kama ambavyo kina mama, vijana na watoto wameweza kupata heshima ya pekee katika jambo hili.

Sambamba na hilo, kwa sababu jamii yetu hii bado ina watu wenye ulemavu wengi ambao wanastahiki kusaidiwa. Lakini jamii yetu hii bado ina watu wenye ulemavu wengi ambao wana uwezo wa kufanya kazi katika sehemu

zote. Lakini bado wapo watu wenye ulemavu ambao wanaweza kujikusanya katika vikundi vya Ushirika wakaa na kubuni baadhi ya miradi yao ili wakaweza kuwezeshwa. Leo tukitizama Wizara ya wenzetu ya Muungano imekuwa na utaratibu wa kuwawezesha watu wenye ulemavu. Sasa iweje sisi kitengo hichi cha watu wenye ulemavu kikawekwa chini ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, tumeombwa tutumie neno "watu wenye ulemavu" sio "walemavu", tutumie "watu wenye ulemavu".

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, sasa nikuombe sana Mhe. Waziri, angalau utakapokuja watu hawa nao waweze kupata faraja. Watu hawa nao katika elimu ambazo wanapewa kutoka kwenye wizara yako nao waweze kunufaika na hili. Maana kwa kufanya hivyo, tutaweza kusaidia jamii kubwa bila ya kuwa na utengano wa aina yoyote katika jamii hii, maana tukiamini dhamira ya Mhe. Rais, ni kusaidia watu wote katika maeneo stahiki.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, wizara hii ni wizara ya uwezeshaji na tukizungumza suala zima la uwezeshaji tunazungumza watu kuwawezesha katika maeneo yao. Lakini tukifungumza suala zima la uwezeshaji inawezekana ikapatikana kikundi cha watu wachache labda kumi au kumi na tano wakabuni kitu chao wakafika wizarani pale na wakaweza kuhudumiwa. Lakini wapo watu ambao wamepata mikopo kwa kuwezeshwa na wakaamua kuchukuwa jukumu la kuweza kufuga mifugo katika maeneo. Sasa ni vyema natambua kwamba wachangiaji wengi waliopita wamelizungumza kwa kina suala zima la ukamatwaji wa mifugo hii. Sikusudii kulisema sana kwa sababu...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, una dakika moja ya kumalizia.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, wamelichangia kwa kina. Sasa niseme tu kwa sababu serikali ina dhamira ya dhati, niwaombe sana tuwe na utaratibu mzuri ili kuwapa hawa watu ambao wamekopa pesa kwa dhamira ya kuzalisha na kuweza kujipatia kipato tuweze kuwafikiria zaidi. Lakini pia hata katika yale maeneo ambayo yamekuwa yapo nje ya miji tukaweza kuyafikiria, maana tukigusa suala zima la wafugaji tunazungumzia asilimia 65% ya mifugo yote inayofungwa Zanzibar ipo katika Wilaya ya Magharibi "A" na Magharibi "B". Sasa naomba sana busara za serikali katika hili, maana tutapoharibu hapa tutakuwa tumeharibu jamii kubwa ambayo inaitegemea serikali yao kuweza kuwahudumia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema maneno yangu machache, nasema kwamba naunga mkono hotuba hii ya Wizara kwa asilimia zote mia ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu alietujaalia uhai na uzima na afya nje hata kufika hapa sote tukiwa wazima na salama. Kwa wale wenzetu wanaoumwa Mwenyezi Mungu awaafu awapunguzie maumivu awape afua wapate kupoa waendelee na kazi zao za kila siku na kwa wale wenzetu waliotangulia mbele ya haki Mwenyezi Mungu awasamehe makosa yao pamoja na sisi. *Amina*.

Mhe. Naibu Spika, pili, napenda nikupongeze na wewe mwenyewe kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuweza kuzungumza machache. Pongezi nyengine napenda nimpongeze Mhe. Waziri, kwa hotuba yake hii nzuri ambayo imepangika na ameisoma vizuri na tumeielewa na tumeifahamu vizuri. Kwa hiyo, napenda nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na wakufunzi wake wakiwemo Makatibu na watendaji wake wote nawapongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani nitakuwa sina mengi ya kuzungumza kwa sababu wenzangu naona wamechangia vizuri sana. Sasa ule usemi ambao niliokwisha kuusema pale nilipokuwa nimeanza kuchangia mwazo kusema kwamba, kuwa jamii sisi watu wenye ulemavu inatuelewa vizuri, lakini serikali ndio bado haijatutambua vizuri. Leo hii imethibitika wazi katika Waheshimiwa wenzangu Wawakilishi wameweza kutuchangia vizuri na kusisitiza katika serikali ili na sisi katika kila wizara tuweke kipengele cha watu wenye ulemavu ambacho kinachotuelezea na sisi tuweze kufaidika na yale ambayo yanayofanywa katika wizara zile. Nashukuru sana Waheshimiwa wangu kwa kunichangia vizuri sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilipenda kusisitiza tu kwamba sisi watu wenye ulemavu kwa kusema la uhaki tunapa mafunzo kupitia kwa wafadhili na wahisani. Lakini serikali yetu bado haijaweza kutupatia mafunzo kikamilifu hasa ya vikundi kwa mafunzo ya ujasiri amali kupatiwa mikopo ya kuanzisha miradi, tuna vijana wengi katika watu wenye ulemavu wanaweza kazi zote, lakini kwa kungalia serikali bado haijaweza kutupitia katika chama chetu na kutoa mafunzo ya ujasiriamali.

Kwa hiyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri, hii bajeti yake basi na watu wenye ulemavu awatilie mkazo apitie katika jumuiya zetu ili atujue kuwa na sisi tupo na tuna vikundi na vipate mafunzo ili ziweze kufanya kazi zake nzuri.

Mhe. Naibu Spika, tukija katika kesi za ubakaji na udhalilishaji, kuna Waheshimiwa wengine wanasema wanadhani kuwa kwamba siwezi kusema kuwa natetea kwa wanawake wenzangu huwa wanavaa ngua za kubana, sijui wanakuwa na nini. Lakini tuweze kujiuliza sisi sote tuliokuwemo humu hivi kwamba mtoto mwenye ulemavu wa akili akawa anatoka madenda na mtoto huyo huyo anabakwa, hii imeshawishika kitu gani kwa mtu kama huyo kumshawishi au tujiulize kwamba mtoto wa kiume au mtoto mdogo wa miaka miwili au mitatu anabakwa na baba au kijana wa miaka ishirini au miaka kumi na nane kamshawishi kitu gani mtoto kama huyo. Leo unamkuta baba ana mkewe ndani basi kama ana mtoto mwengine aliezaa kwa mume mwengine ni mtoto wa kiume anakwenda anambaka hali ya kuwa mkewe yumo ndani. Sasa ni nini kilichomshawishi kafanana na mama yake au? (*Makofi*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa wenzangu hili tulizingatieni kuwa hawa watu ni madhalili na roho zao mbaya. Kwa hiyo, hawa wanastahiki adhabu kali ambapo watakapopatikana, sio kusema tu kwamba eti vishawishi, vishawishi kweli, sisi wanawake tunakuwa na vishawishi lakini kuna mengine wanafanya kwa uzalili na roho zao zilivyokuwa katili, hivi ni vitendo vya ukatili. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mhe. Waziri, tunakuomba uwape mafunzo mazuri maafisa wako wa Wilaya waweze kufanya kazi zao vizuri katika Shehia zao ili kesi kama hizi ziweze kubainika vizuri na viweze kubainika kwa wakati na zifanyiwe kazi kwa wakati. Kwa sababu ikiwa kama hazifanyiwi kazi vizuri maafisa wako utazikuta kesi hizi wanabakwa watoto wa kike au watoto wa kike wakishabakwa kina mama au baba kesi zao zinaishia majikoni pengine hukaliwa vibarazani na kutandikiwa majamvi na kutolewa posa anasema kwamba nitamlea mimi mpaka akiwa mkubwa nitamuona kwa sababu tu hakuna ufatiliaji, mama anapewa shilingi elfu mbili au tatu ananyamaza kimnya anakosa kutoa ushahidi.

Nakuomba sana na nakusisitiza sana kama sisi ndio wanawake na wanawake ndio sisi na sisi ndio tunaoumia, hakuna anaeumia, mwanababa yeye akishafanya kosa anatoka akuachia wewe mama. Nakuomba sana Mhe. Waziri, kwa haya yangu machache nauinga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Na pia nakupongeza sana Mhe. Waziri, kwa hotuba yake nzuri. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niseme machache katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana na Watoto.

Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa, lakini nimshukuru zaidi kwa kutujalia afya na uzima kwamba tumekutana hapa na kuendelea katika majukumu yetu ya kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, pili, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii. Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Waziri, kwa wasilishaji wake mzuri na wa ufasaha wizara ina changamoto kubwa, lakini mimi naamini mwenye wizara ni mama na mwenye uwezo mkubwa kabisa ambaye Mhe. Rais amemuamini pamoja na sisi tumemuamini kwamba ataweza kuzishughulikia changamoto ambazo zinapatikana katika wizaraa hii.

Mhe. Naibu Spika, na tunaamini kwamba ilipo hivi sasa mpaka 2020 *inshaalla* wizara itakuwa imepiga hatua kubwa kwa sababu naamini waziri ni mtendaji na timu yake ya utendaji, *alhamdulillahi,* Katibu Mkuu mzuri na watendaji wote tunaamini kwamba wanaweza kufanyakazi vizuri. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nimesisima hapa kama Mwakilishi ambaye nimeletwa na kina mama wa Kusini Unguja. Lakini Mhe. Naibu Spika, Wawakilishi wanawake tuko wengi, naomba nisizungumzie masuala ya wanawake nitawaachia Wawakilishi wenzangu na mimi naomba nijikite katika masuala ya watoto ambao wao hawana Uwakilishi humu ndani na wanategemea sisi mama zao kusimama na kutetea haki zao ambazo kwa muda mrefu sana wemekuwa wakizikosa.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka katika Baraza lililopita wewe mwenyewe uliwahi kuleta hoja binafsi juu ya masuala ya uzalilishaji wa watoto na tukatoka na maazimio mazuri kabisa kwa maana kwamba yangefanyiwa kazi leo hii tungekuwa tunazungumzia namba ndogo zaidi ya kesi hizi kama kweli yale maazimio tungeliyafanyia kazi serikali ingeyatilia maanani.

Mhe. Naibu Spika, kati ya maazimio ambayo tulianzimia hapa kutokana na udhalilishaji wa watoto tulisema kwamba, tunahitaji sheria zetu ambazo zina ile mianya ambayo inasababisha hawa wabakaji ama hawa wafanyaji wa haya matendendo huwa wanaachiwa *free* na baadae wale *victims* wa udhalilishaji hawapati haki yao ambayo walitakiwa kuipata.

Mhe. Naibu Spika, sheria mbali mbali kama mfano *The Evidence Act* Sheria ya Ushahidi ni ya zamani mno, najua sasa hivi iko katika *process* ya kuletwa Barazani ili kufanyiwa marekebisho. Lakini naiomba serikali sana iharakishe sheria hili ili watoto pamoja na makosa mengine ushahidi uende yaani muda unavyobadilika sheria iendane na iwe *upto date* na *time* ambayo tupo hivi sasa.

Sheria iliyokuwepo ni ya zamani mno sana, ni aibu hata kutaja mwaka ambao wa sheria tunayoitumia katika uliwengu huu wa sasa.

Mhe. Naibu Spika, mimi *concern* yangu ipo katika Sheria ya Mtoto wanaita, *Act No. 6 of 2011,* kifungu cha 18 (1) Mhe. Naibu Spika, cha sheria hii kinaanzisha Uanzishwaji wa Mahakama ya Mtoto. Mhe. Naibu Spika, naishukuru serikali sana Mahakama ya Mtoto imeanzishwa na kumekuwa na jitihada za makusudi kabisa ambazo zilikuwa zimechukuliwa. mimi tangu nimeanza Baraza hili ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria nimeshawahi kutembelea Mahakama ya Watoto na yaani ukiingia pale huhisi kama upo Mahakamani. unahisi labda upo kwenye Nursery School ya watoto ambayo inatakiwa kabisa ili mtoto aji-*feel* yupo sehemu ambayo si ya kutisha.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia kuna *system* ile ya kusikiliza ushahidi wa mtoto ambayo kulikuwa na kifaa kimoja hakijakamilika, lakini tunashukuru kwamba wafadhili wameshakamilisha kifaa kile, kwa hiyo, ushahidi wa mtoto unapochukuliwa unaenda kama inavyotakiwa. Lakini tatizo langu lipo katika sheria hii kifungu cha 18(b), ambacho kinasema Mhe. Naibu Spika, naomba kunukuu kama sheria inavyosema:-

"Hearing and determining criminal charges against a child for an offence alleged to have been committed before the child reaches the age of 18 years other than a charge of murder, manslaughter, treason or rape"

Mhe. Naibu Spika, tatizo langu hapa kifungu hichi kiufupi kimetaja makosa ambayo hayapaswi kusikilizwa na Mahakama ya Watoto. Lakini sina tatizo na makosa ambayo yametajwa, lakini tatizo langu Mhe. Naibu Spika, lipo katika kesi za *rape* ambapo kwa bahati mbaya sana kesi hizi ni kubwa katika jamii yetu ya Wazanzibari. Lakini kwa nini Mhe. Naibu Spika, kesi hizi zisikilizwe na Mahakama ya Watoto ambao utaratibu wa kusikiliza kesi hizi na utaratibu wa kuchukua ushahidi ama utaratibu wa kutoa hukumu ya kesi hizi ni sawa sawa na ule ambao Mahakama ya Watoto inasikiliza kesi nyengine na kutoa hukumu kama kesi nyengine za watoto zinavyosikilizwa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, kulawiti inasikilizwa katika Mahakama ya Watoto, lakini kubakwa inasikilizwa katika hizi Mahakama nyengine. Sasa ninajiuliza hivi kweli kuna ile *good will* ya kuwataka hawa watoto kuwa-*protect* kwamba, yasikutwe na haya yanayowakuta. Mhe. Naibu Spika, Mahakama zetu hizi za kawaida zina mambo mengi ya kushughulikia; Kuna wezi, majambazi na wanaodhulumu huko, wote wanasikilizwa huko. Mahakama zitakuwa na muda saa ngapi wa kusikiliza hizi kesi za watoto za kubakwa. Ndiyo maana unaona

kesi hizi zinaripuliwa ripuliwa baada ya miezi miwili mitatu, mtu anatozwa faini elfu thalathini, kishaharibu mtoto wa mtu siku ya pili munadunda naye mtaani kama kawaida. (*Makofi*)

Hapa ndiyo pale ambapo wananchi wanaona serikali haiwatendei haki juu ya suala hili. Na ndiyo sababu hii ambayo inayosababisha kwamba huu ubakaji unaongezeka, kwa sababu hao wafanyaji wanaonekana mitaani. Mtu akishakutoka *wallahi* anakwenda kumtafuta mtoto mwengine anamuharibu. Kwa hivyo. hii inakuwa *unfair*. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, namuomba akija hapa atuelezee. Inawezekana sheria tumetunga sisi na inawezekana sheria huwezi kuona kila kitu. Humu sisi sote sio wanasheria. Inawezekana imetupitikia hatukuona, lakini inawezekana hao *drafters* wa hizi sheria wameitunga kwa sababu wana maana yao. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, akija hapa ninamuomba aje atueleze, kwa nini hizi kesi za kulawiti zinaruhusiwa kusikilizwa katika kesi za Mahakama ya Watoto, lakini kubakwa hairuhusiwi kusikilizwa katika kesi zile.

Mhe. Naibu Spika, naomba ni-*support* hoja yangu ambayo nimesema. Ukiangalia jaduweli kwenye ukurasa wa 77, Kiambatanisho Nam. 13, yaani inazungumza *clearly* kwamba, hili tatizo ndiyo linalosababisha uongezaji wa hizi kesi. Ukiangalia Hospitali ya Mnazi Mmoja kesi za kubakwa zimepokelewa 369 kwenye kipindi cha 2015 mpaka Aprili/Juni, Julai 2015 mpaka Aprili 2016. Lakini kulawitiwa ni kesi 15.

Mhe. Naibu Spika, lakini ukiangalia kesi ambazo zimesikilizwa, yaani ni kesi nyingi sana za kubakwa hazijasikilizwa *compare to* kesi ambazo zimesikilizwa katika kulawiti. Kwa hivyo, katika kulawitiwa kuna kesi chache kabisa ambazo zimebaki. Na kwa sababu hakuna kesi hizi zinazosikilizwa kwa utaratibu kama ulivyokuwa na kwa sababu ile Mahakama ina-*deals* na hizi kesi za watoto tu. Kwa hivyo, tatizo linakuja huku kwenye kubakwa. Mahakama za huku zipo *busy* sana hazisikilizi hizi kesi. Kwa hivyo, naomba sana kama nafasi ya kurekebisha hii sheria ije tuirekebishe ili tuone kwamba kesi za kubakwa pia zinasikilizwa katika Mahakama ya Watoto. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, lakini jambo jengine naomba kuzungumzia kuhusu Idara ya Ustawi wa Jamii. Mhe. Naibu Spika, Idara ya Ustawi wa Jamii, idara hii inahusiana sana, yaani inategemea sana na kazi ambazo zinafanywa na Mahakama ya Watoto. Yaani kuimarika kwa idara hii ninaamini ni kuimarika kwa haki za watoto ambazo zitapatikana.

Mhe. Naibu Spika, Kifungu Nam.41 cha Sheria hii ya Mtoto kinasema kwamba;

"*Any child who has been arrested for the alleged commission of an offence shall be assessed by probation officer or a welfare officer, if practicable before he is brought before the Children's Court, in order to,...*" inaonesha.

Yaani kwamba kutolewa hukumu kwa hizi kesi za watoto kunategemea ripoti ambayo ustawi wa jamii itapeleka Mahakamani.

Mhe. Naibu Spika, Ustawi wa Jamii haipati fedha ipasavyo. Kwa hivyo, inashindwa kufanya kazi ipasavyo na ndiyo maana unaona hata huu usikilizwaji wa kesi za watoto katika Mahakama za kawaida unakuwa mgumu, kwa sababu ushahidi unaopelekwa pale *sometimes* hao Ustawi wa Jamii wenyewe wanashindwa hata kwenda, mfano kesi imefanyika Nungwi. Atatoka siku ya kwanza atakwenda, siku ya pili ataambiwa hamna mafuta ya kuweka kwenye vespa ya SMZ anakaa kitako na yeye hayendi. Kwa hivyo, wakati huku yeye anakaa kitako na Mahakama inategemea ripoti yake kutoa hukumu, huku pia kesi inalala. Malalamiko yanakuwa makubwa. Siku ya pili yule yule mbakaji kabla haijasikilizwa kesi yake anakwenda kutafuta mtoto mwengine anamuharibu kwa sababu tu hamna chochote kinachokuwa.

Sasa ninaomba sana serikali iangalie hii Idara. Wanaweza kuona labda haina umuhimu fulani hivi sana, lakini niseme kwamba iangaliwe sana hii Idara ili waone kwamba, wanapatiwa fedha za kutosha ili kuona kwamba kesi hizi za watoto zinasikilizwa na watoto wanapata haki zao, na wale wanaharamu wanaobaka wapate adhabu kama inavyostahiki kutokana na sheria ambazo tumeziweka. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa kuna kituo hichi cha *One Stop Centre*. Tunashukuru sana wafadhili wamekuwa wakitusaidia katika kituo hichi, lakini Mhe. Naibu Spika, *it's so sad* kwamba. kituo hichi wafadhili walikichukua na kikawa kinafanya vizuri. Lakini tu baada ya kurejeshwa kwenye mikono ya SMZ kituo kimeanza kushuka zile huduma zake. Mhe. Naibu Spika, tutabebwa mpaka wapi? Tunapobebwa na sisi lazima tujikaze na tujishushie kule nyuma, mbebaji anachoka na yeye. Lakini tushukuru kwamba hichi kituo kimerudi tena baada ya wafadhili kuona kwamba mambo yanakwenda mrama wamekichukua tena. (*Makofi*)

Kwa hivyo, sasa hivi mambo yameanza kwenda vizuri. Hivyo, niseme Mhe. Naibu Spika, kwamba serikali, *please,* wajitahidi pale tunapobebwa basi na sisi tubebeke. Siyo mushabebwa munaachiwa kitu kinakwenda kuporomoka mpaka munarudi *down to ziro,* hairuhusiwi na wala haipendezi. Kwa hivyo, niiombe sana serikali pale inapobebwa nayo ijibebe. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi leo nimesema sitoingia popote ninataka nilie na watoto, kwa sababu wazazi hasa wa kike tunaumia na mimi mwenyewe ni mzazi. Hivyo, Mhe. Naibu Spika, sitaki kuzungumzia lolote, ninasubiri maelezo ya Mhe. Waziri, ambayo ninamini sana kwa uwezo wake atakuja na maelezo mazuri tufahamiane ili bajeti yake ipite. *Otherwise,* tutakuja kujibiana kwenye vifungu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, sizuii shilingi yoyote lakini ninasubiri maelezo mazuri ya Mhe. Waziri. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, ahsante ninakushukuru. Sasa hivi Waheshimiwa ni zamu ya Mhe. Tatu Mohammed Ussi, baadae atafuata Mhe. Hamad Gerei na baadae atafuata Mhe. Suleiman Makame Ali.

Mhe. Tatu Mohamed Ussi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kusimama na kuichangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Nimpongeze Mhe. Waziri, jinsi alivyosoma hotuba yake lakini pia niwapongeze na watendaji wake, kwani bila ya wao hotuba hii leo isingeweza kufika hapa na tukaweza kuijadili.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu moja kwa moja utalenga kwenye vikundi vya ushirika vya wanawake. Ni kweli Mhe. Naibu Spika, kama tulivyoiona wizara kuwawezesha wanawake kujikwamua kiuchumi, niseme tu katika Mkoa wangu wa Kusini Pemba wanawake wengi wameitikia wito huu wa kuunda vikundi vya ushirika. Na wanawake hawa wanajituma kweli kweli kwa lengo la kujipungizia ukali wa umaskini. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, niishauri tu Wizara hii na hususan Idara ya Vikundi vya Ushirika, wanawake wenzetu wanapotaka kupata hati za ushirika, wajitahidi kupeleka mapema wasiwacheleweshe sana. Kwani Mhe. Naibu Spika, wanawake walio wengi wameunda vikundi lakini upatikanaji wa hati unakuwa kidogo ni tatizo hasa kwa Wilaya ya Mkoani. Na ushahidi ulio wazi kwamba,

mimi mwenyewe binafsi nilivitembelea hivi vikundi vya ushirika, lakini wengi wa wanawake hawa walikuwa wakilalamika suala zima la kupatiwa hati za ushirika. Kwa hivyo, naiomba wizara hii ilitilie maanani suala hili la kupata hati za ushirika ili wanawake waweze kujikwamua na umaskini. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, bila ya kuwa hati ya ushirika inakuwa ni kundi la watu tu, siyo kikundi cha ushirika na wala hakitambulikani. Hivyo, suala la kupata hati imepatikane kwa mapema. (*Makofi*)

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, niishukuru Idara ya Mikopo Pemba. Idara ya Mikopo kweli wanatoa mikopo, lakini ninataka niwashauri kabla ya kutoa mikopo kwa ajili ya kuwawezesha wananchi au kuwawezesha watu wenye vikundi vya ushirika, basi kwanza wawaweke na kuwapa elimu ya ujasiriamali. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, walio wengi wanachukua mikopo, lakini mikopo ile ikishachukuliwa hawajui namna ya kuitumia kutokana na ukosefu wa elimu ya ujasiriamali. Kwa sababu mjasiriamali anatakiwa kwanza abuni mradi wake, lakini aangalie nini atapata faida na hasara itakuwaje. Kwa hivyo, hii ninashauri Idara ya Mikopo kuwapa elimu wajasiriamali wetu kabla ya kutoa mikopo.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye kifungu chengine ambacho kwenye kitabu cha Mhe. Waziri, alizungumzia kwamba, kuna dhamana ya fedha na hii ipo kwenye ukurasa wa 18, kifungu cha 42. Waziri ameeleza kuwa kuna dhamana ya fedha shilingi milioni mia moja na hamsini katika benki ya *CRDB* kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vijana. Lakini ninamwambia siyo vijana tu pamoja na wanawake wanachukua mikopo katika benki hii. Kwani mimi mwenyewe nikiwa Katibu wa Kikundi cha Tuishi kwa Usalama *SACCOS* nimeshachukua mikopo zaidi ya mara tatu katika benki ya *CRDB*. Kwa hivyo, ninawaomba na wanawake wenzangu wajiunge katika benki hii. Ninaishukuru sana inatusaidia sana. Lakini vile vile pia Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja kujibu hoja zangu au kujibu hoja za Wajumbe anieleze ni vikundi vingapi vya *SACCOS* au vya ujasiriamali ambavyo vimejiunga na benki ya *CRDB* kwa Unguja na Pemba. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoka hapo niende kwenye suala la udhalilishaji wa watoto. Mhe. Naibu Spika, sisi akinamama zaidi kwa sababu kila linapotokea suala la udhalilishaji basi akinamama tunakuwa tunanyonga roho na tunaona kwa nini watoto wetu wadogo wafanyiwe vitendo vya udhalilishaji. Na tukizungumza kila siku ushahidi haupatikani. Sasa je, Mhe. Naibu Spika, suala hili tutakuwa tunalilia kila siku kilio ni hichi. Ninakumbuka tokea tulipoingia ndani ya Baraza hili suala la udhalilishaji wa watoto tunalizungumza. Lakini jibu hasa hatujalipa.

Sasa tujiulize sote kama wazazi. Ni chanzo gani hasa kinachosababisha hata ikawa watoto wetu kudhalilishwa. Wengine wanasema kuwa vijana wa kike wanajiuza lakini hawa watoto wadogo na watoto wanaodhalilishwa zaidi ni wale wadogo wenye umri wa miaka miwili, mitatu, mitano. Sasa kwa kweli Mhe. Naibu Spika, hichi ni kilio chetu sote kwa sababu kila aliyekuja kalizungumzia suala la watoto. Tumelizungumzia hili kwa sababu linatuumiza ndani ya nafsi.

Lakini pia sisi kama wazee tujiulizeni. Yale malezi ambayo sisi tulilelewa ndivyo tunavyowalea watoto wetu. Hili linakuja kwa sababu yale maadili ya malezi yamepotea. Zamani sisi tulikuwa ukifanya kosa hupigwi na mzee wako aliyekuzaa, wala huhukumiwi na mzazi wako, anakuhukumu mzee wa jirani. Lakini leo sisi kama wazee tumeacha maadili yetu ya kuwalea watoto wetu. Kwa hivyo, naomba sisi kama ni walezi tukaeni tutafakari na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, tukaeni na tutafute kitu gani kinachosababisha hili, baadae tupite kwa wananchi wetu, kama ni tofauti za kisiasa au tofauti za kidini lakini lazima tukubali kuwa malezi tuliyolelewa siye, siyo tunayowalea watoto wetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo mdogo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Tumpishe basi Mhe. Gerei, ninakuomba sana muda utumie mchache ili tuweze kumpa Mhe. Khadija Omar Kibano na kama tutaweza kupata na Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis. Kwa hivyo, Mhe. Gerei, ujitahidi pamoja na Mhe. Suleiman Makame.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi ninapenda kwanza kukushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Naibu Spika, na mimi ninataka nipunguze muda kidogo niseme kwa haraka, nitasema kwa *speed* tu muda utapungua, haina tatizo. Mhe. Naibu Spika, mimi katika mchango wangu kwanza nimpongeze Mhe. Waziri, kwa hotuba yake nzuri ambayo ninaamini ana wataalamu wa uhakika waliomsaidia katika kupanga mambo haya na kuisoma kwetu kwa lugha fasaha kabisa. Ninashukuru na ninampongeza na ninamwambia kwamba tumeielewa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye michango. Mhe. Naibu Spika, mimi moja kwa moja ninajikita na kile kipengele cha kesi za udhalilishaji. Kama alivyotwambia Mhe. Waziri, na ninaomba kunukuu katika ukurasa wa 41, unaeleza wazi kwamba;

> "Programu imepokea jumla ya matokeo ya udhalilishaji wa watoto 1,014 kutoka vituo vya mkono kwa mkono Unguja na Pemba ambapo 139 kutoka Chake Chake, Wete na Mkoani na 875 yameripotiwa kutoka vituo vya mkono kwa mkono vya Mnazi Mmoja".

Mhe. Naibu Spika, inasikitisha kuona kwamba kesi 1,014; kesi tatu tu ndizo zilizopatiwa ufumbuzi ndani ya mwaka. Mimi ningependa kumwambia Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, na nina imani kwamba kuna makosa madogo madogo yanayochangia kutokupatikana au kucheleweshwa kwa ushahidi.

Labda nianze kwenye Jeshi la Polisi. Mhe. Naibu Spika, inaonekana dhahiri kwamba kwenye Jeshi la Polisi yule mtendaji mkuu anayewekwa pale, siye muhusika halisi wa kufuatilia kesi. Matokeo yake anazunguka sana na kupoteza muda, halikadhalika na kuchelewesha ule ushahidi.

Nasema hivyo mfano mzuri ninao ndani kwangu mimi, nina kesi ya mwanangu kabisa, ni muda sasa hivi mrefu ni zaidi ya miaka miwili uwamuzi haujapatikana, lakini ushahidi ukiutizama uko wazi kabisa. Kwa hivyo, nafikiri wale watuhumiwa wanaoshughulikia hizi kesi na sio polisi tu hata madaktari, kwa sababu ingekua polisi muhusika anasoma kesi ile na anayajua yale mambo.

Kwa mfano, daktari anaweza kwenda kumpima yule mtuhumiwa wakati ule wa tukio lilipomalizika kufanyika, lakini polisi yule haelewi hata zile *terminologies* za kidaktari anazoandika pale kuweza kujua ni kitu gani. Kwa mfano daktari anaweza kumia neno "*rapture"* lakini polisi hajui neno "*rapture"* maana yake ni nini. Ina maana ushahidi anaopeleka kule Mahakamani hautoshelezi kabisa. Daktari wa maabara anaweza kupima akaona vipimo vile vya *sperms* walioingia katika sehemu ile ambayo imefanyiwa tatizo, yule polisi haelewi, ina maana ni wepesi kwa daktari akipata rushwa ndogo tu, anaweza kumdanganya yule shahidi au mpelelezi kuupoteza ushahidi wa kesi ile na matokeo yake kesi ile inatupiliwa mbali.

Lakini sio hilo tu, ni jambo la ajabu kusikia *file* la kesi limeondolewa kwa sababu mtuhumiwa hafiki Mahakamani. Hivi tujiulize mtuhumiwa kwa nini asifike Mahakamani. Raia anaishi hapa, mtuhumiwa aliyefanya kosa yupo, lakini hafiki Mahakamani na *file* linaondolewa, ni jambo la kusikitisha na

inaonesha dhahiri kwamba labda jeshi letu la polisi au wizara yenye haifuatili kwa ukaribu kesi hizi za udhalilishaji.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye udhalilishaji mwengine ambao unafanyika nchi za nje. Mimi kwanza ningependa kujua wale wananchi wetu wanaopelekwa nchi za nje kama waziri alivyoeleza, kule nako tumepata fununu wengine wanafanyiwa udhalilishaji mkubwa wa kijinsia, na matokeo yake wanarudi hapa nchini. Wengine kwa ushahidi wapo, pale Chake Chake kuna mmoja anaumwa kabisa. Nimuulize Mhe. Waziri, wanachukua hatua gani kwa wananchi wetu kwa wale wanaodhalilishwa nchi za nje? Wanarudi nchini kwetu wanaudhunika na kusikitika sana, lakini hakuna hatua zinazochukuliwa. Mimi namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa kufanya majumuisho basi anipe maelezo ya kina ni hatua gani wanazochukua si kwa ndani tu, lakini hata kwa wale wanaofanyiwa udhalilishaji mkubwa nje ya nchi hasa nchi za Kiarabu. Ni hatua gani wanachukua kuweza kuwatetea wananchi wetu wale kwa udhalilishaji wanaofanyiwa kule, wakati ruhusa tumetoa sisi wenyewe kuwapeleka kule.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye kifungu chengine, kuhusu vikundi vya ushirika. Mimi nafurahi kwamba katika Mhe. waziri, katika wizara yake kuna wataalamu wa ushirika wengi, na nashukuru kwamba, kuna mmoja ni mwanafunzi wangu kabisa, nilizungumza naye na yuko tayari kuja katika jimbo langu kunisaidia namna ya kukuza hivi vikundi vya ushirika. Lakini kabla ya hapo ningependa waziri akija atuambie ni vikundi vingapi vya ushirika Pemba vimesajiliwa na vimefuatiliwa na vimepata huduma. Aniambie vimefaidika vipi pamoja na serikali katika ushirika huu, kwa sababu kwa muono wangu naona kwamba vikundi hivi mara nyingi baada ya kusaidiwa tu na kupatiwa mikopo, vinachukua muda mfupi sana kufa na matokeo yake vikundi vile huvioni tena, mpaka wasikie tena kuna mkopo vinakwenda kwenye mkopo kuanza tena upya. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri, atakapokuja aniambie ni ufuatiliaji gani mwingine unafanyika hapo baada ya vikundi hivi kupewa mkopo ili vijiendeleze. Kwa sababu nia nzuri ya serikali ni kuwapa mikopo vikunvi hivi viendelee kuwepo, vijiendeleze na kupunguza lile tatizo la ajira nchini, lakini mara nyingi huwa vinakufa. Ningependa Mhe. Waziri, yule mwanafunzi wangu nimemuomba na kakubali kabisa kuja kwenye jimbo langu, na nitamchukua, namuomba ampe ruhusa nikimtaka nimchukuwe ili na mimi akanipe elimu au akawape elimu wananchi wangu wa Jimbo la Wawi, ili kuweza kufanya vikundi vya ushirika tena vya kujiendeleza na nitaomba kuwe na ufuatiliaji wa

uhakika tukishirikiana mimi na yeye na Wizara nzima hii ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo mimi napenda niunge mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri, kwa asilimia 98, nampunguzia asilimia 2 tu, mpaka nitakapopata majibu haya ya wananchi wetu wanaodhalilishwa nchi za nje na wanaporudi nchini, ni hatua gani zinachukuliwa kwa wale waliowadhalilisha. Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia 98. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Nakushukuru sana sasa Mhe. Suleiman Makame Ali, anafuatia Mhe. Khadija Omar Kibano, na Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia kwenye Wizara hii ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitaki niseme mengi kwa sababu pia ni mjumbe wa kamati hii ya wizara hii, isipokuwa nataka niipatie baraka tu kidogo na kama ushauri. Mhe. Naibu Spika, kwanza kwa dhati nawashukuru wale wote waliokaa wakatafakari kwa kutulia kabisa na wakaitunga bajeti hii ya hotuba hii kwa uangalifu na uono mzuri, kusema kweli hii hotuba imejengeka kwa vina na kila kitu. Nawapa pongezi sana kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wengine wa wizara.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye suala la pencheni. Kwanza nampongeza sana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein kwa uamuzi wake na kukaa kwake akatafakari na kuona kwamba wazee wetu hawa wapatiwe pencheni kuweza kujisikia na wao kama wazee wengine.

Mhe. Naibu Spika, nadhani kwa Tanzania au kwa Afrika ya Mashariki hii, itakuwa Zanzibar ni ya kwanza kulitekeleza hili. Kwa hivyo, mimi niiombe wizara wahakikishe kwenye suala hili la wazee wanaopatiwa pencheni hii, iwe ni wale wale wazee waliokusudiwa na mwenyewe Mhe. Rais, sio wale vijana. Kwa sababu inawezekana ikawa kuna vijana au kuna watu wenye nguvu zao huko ambao wanaweza kubeba polo za mkaa, za viazi na za vitunguu na kuweza kupata pesa. Kwa hivyo, naiomba wizara sana wawe waangalifu na watendaji wao kwenye suala hili la wazee, pesa hizi zilikusudiwa kwa wazee basi wapewe wazee na isiwe vyenginevyo.

Vile vile, niwaombe wawakilishi wenzangu, kwa sababu Zanzibar imejengeka majimbo, wilaya, mikoa na shehia na wengi humu tumetoka majimboni, hebu

tumsaidieni Mhe. Waziri, kwa sababu hili suala linaniuma kweli. Mimi jimboni kwangu Mhe. Waziri, namuahidi nitamsaidia, nitahakikisha kwamba wale wazee wanaopatiwa pencheni hii kweli ni wazee wanaostahiki. Isiwe kama leo pesa kakusudiwa kupe mzee basi anapewa mtu mwengine aliyekuwa na nguvu zake za kuweza kufanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, pia, niwashauri na niwaombe watendaji wa wizara hii kwamba wafuatilie kwa kina, pale mzee ambapo ameshafariki, isijegeuka kama kule kwenye *welfare*, maana mara nyingi huwa nalizungumza suala hili, siku nyengine mtu amekufa tangu enzi ya Nabii Nuhu, lakini ikawa ile pesa inatoka kwa njia ya kinyemela nyemela. Pia, na hili naiomba sana wizara waliangalie, pamoja na sisi Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi huko majimboni mwetu tuwape ushirikiano watendaji wa wizara hii, ili waweze kutekeleza kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye mikopo ya wajasiriamali. Pia, serikali yetu inaimani sana na wananchi wake kwa kuanzisha kitengo hiki cha Idara ya Mikopo, kuwapatia wananchi wake mikopo iliyokua haina riba, mikopo yenye masharti nafuu. Lakini Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, cha kushangaza sana, kuna watu wamepewa mikopo hii waendeleze maisha yao kujikwamua na ukali wa kimaisha, lakini leo ukienda kuuliza pale. Mimi nilikwenda pale Madungu Chake Chake nikenda kuuliza. Nikaambiwa kwamba hii mikopo inasuasua kulipwa, kwa sababu kuna wengine wanasema ati kama hajapata fulani kuwa Rais basi hatulipi.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi nikawa najiuliza kichwani mwangu kwamba; hivi huyo aliyekuwa kama yeye Rais hajapata kuwa hamulipi mlikokopa, ilikuwa muulize yeye alichangia kwenye hii mipango kwamba hizi pesa zikapatikana, alichangia yeye huyo? Mimi nakumbuka kwamba huu mfuko aliuweka Dkt. Shein au sio? Lakini leo cha kushangaza mtu anakuambia kama hajapata Urais mtu fulani basi silipi. Huyo aliyemkusudia hata kuchangia hajachangia. Sasa watu kama hawa wanadhorotesha idara hii isiende mbele, kwa sababu kuna wengine wanasubiri wapatiwe mikopo. Leo mtu kachukua shilingi milioni 5, milioni 6, milioni 7 kazikomelea yeye hataki kuzitoa kwa kuwa fulani eti hajapata Urais.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi naomba wizara yako Mhe. Waziri, kwa kupitia kitengo hiki hapa wawe wakali sana na wawachukulie hatua wote wale ambao wameshakopa na muda umeshafika wa kulipa, lakini bado hawalipi eti kwa kusingizia kwamba Mhe. Shaib Said, hajapata basi silipi. Huo utakua ni ugonjwa.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye suala la udhalilishaji. Suala hili la udhalilishaji Zanzibar limekua kama nyimbo, kila siku udhalilishaji, udhalilishaji. Mhe. Naibu Spika, suala la udhalilishaji mimi niseme polisi wajitahidi kuifanya hii kazi ya kuwakamata wale, na siku nyengine wale wanapopelekwa kule polisi hupelekwa mahakamani, lakini sasa polisi kama polisi hatomchukua muhalifu akamuweka nyumbani kwake, atapelekwa mahakamani, lakini sasa huko mahakamani ukifika unaambiwa kesi haina ushahidi, sijui haina hichi na hichi. Kwa hivyo, kesi huwa pale mahakamani ndio zinaposhindikana.

Nakupa mfano huo Mhe. Naibu Spika, kwa sababu mimi mwenyewe nina jirani yangu kule Ndagoni, nilizungumza hapa kwenye suala la katiba na sheria, alikamatwa yule akapigwa na mume wake na kukamatiwa mundu, kesi ikaenda mahakamani ikaenda rushwa pale. Kuna Mkurugenzi mmoja kutoka Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto akaifuatilia na akaigundua ile kesi kwamba tayari kuna rushwa ilitolewa.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, kusema kweli ikiwa kama hatukuwa makini na suala hili na tukawa na moyo thabiti kabisa, itakuwa kila siku tunaimba kwamba, suala la udhalilishaji. Vile vile, Mhe. Waziri, nakuomba sana kwenye suala hili uwe makini sana. Yeyote ambaye hafanyikazi ili kukupaka matope wewe basi Mhe. Waziri, usimkubalie kabisa, na mimi nipo na nitakapobaini basi nitafichua na nitakuambia, kwa sababu sisi tuko hapa kwa kuwatetea wananchi. Lakini pale tunapofichua, tunapozungumza kwamba ni tunatumbua jipu basi lile jipu litumbuliwe na ikiwa tukifanya masihara basi hayo majibu yatakuwa majipu, yatakuwa matezi na baadae yatakuwa matende. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia 120. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Mchangiaji wetu anayefuata sasa hivi ni Mhe. Khadija Omar Kibano, na baadae Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis, Mhe. Rashid Makame Shamsi, nimekuona kama tutapata dakika mbili nitakupatia.

Mhe. Khadija Omar Kibano: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii leo na kuweza kuchangia masuala ya udhalilishaji wa kijinsia. Moja kwa moja nakwenda kwenye kesi ya ubakaji na udhalilishaji kwa wanawake ambazo sana kesi hizi zinamalizikia polisi na ndiko zinakoanzia kesi hizi. Kesi hizi wanawake wengi au watoto wanabakwa na kukamatwa na wengine wanadhalilishwa hasa wanawake wanaofanyakazi katika majumba, wanawake wakiwa na waume zao, wanawake wakiwa ni wajane wanadhalilishwa kwenye kesi hizi.

Mhe. Naibu Spika, kesi hizi zinapofika kwenye dawati la wanawake polisi zinafika pale baadae inafika kesi ile inasemewa na ushahidi kamili unapatikana, lakini bado watu wa dawati pale kesi ile haipeleki mahakamani inavyopaswa. Kutokana na hali hiyo, kuna baadhi ya kesi nyingi sana ziko pale kwenye madawati hayo ya wanawake polisi, wao wanazimalizia kesi zile, kama mfano ni kesi za ubakaji wa jinsia kwa mwanamke au mwanamme au mtoto, basi wanakuwa wao sana masuala haya yanafika kwa wazee. Wazee wanaambiwa wamaliziane wenyewe kwa wenyewe suala hili kutokana na huyu mtoto aliyebebeshwa mimba au kama ni mtoto amebakwa, basi wanasema tumalizane kwa sababu ni ndugu kwa ndugu, pengine ni mtoto wa shangazi kwa mjomba, ami kwa dada, kaka kwa shangazi, watu hawa wanaambizana masuala haya yamalizike pale, kwa sababu sisi tunachokihitaji ni kuwa kesi ziendelee kama zimekamilika hospitali na polisi, kwa hivyo, kezi zile ziendelee kama zinavyotakiwa ili zihukumiwe kihalali.

Mhe. Naibu Spika, suala la kesi hizi za mambo ya ubakaji, ni zaidi hutokea kwenye jamii na kuruhusiwa muhali, hiyo ndio inayofanyika zaidi na ndio inayosababisha kesi zisiende mbele. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, muhali huu mimi ninasema kwamba usemewe zaidi na waziri au serikali ili iweke mkondo wake wa kisheria kama kesi yoyote itakapothibitika imekamatwa kihalali na ina ushahidi kamili, basi isioneshee kama rushwa ya muhali kwa wazee au jamii, hatuitaki, kwa sababu huu udhalilishaji unakandamiza sana kwenye jamii.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika wafanyakazi wa ndani ya majumba hawa wanawake. Tunawachukua watoto wa watu na kuwaweka katika majumba yetu, kama mama au baba anamchukua mtoto yule kama ni mjane au ni mwari anakaa naye ndani ya nyumba na kuishi naye kama ni mwanawe. Kwa sababu unapomchukua mafanyakazi wako yeyote yule anakuwa ni mwanao. Lakini sasa kuna masuala ya wanaume, hawa kina baba anaishi na mtoto yule kwa muda wa miaka mingi, atampenda kuliko wewe mke wake kwa jinsi anavyoishi ndani ya nyumba, na atakuwa ana maamuzi ndani ya nyumba ile kuliko wewe mwanamke uliye ndani ya nyumba na unayemiliki nyumba ile kisheria za kidini ndani ndoa.

Mhe. Naibu Spika, kikishafikia kiwango hicho basi anakuwa mtoto yule anachukuliwa na baba yule katika gari yake au katika msafara wake wa kwenda hoteli au safari nyengine yoyote baadae huko mwisho wanamalizana kimapenzi. Wakimalizana kimapenzi, kwa hivyo, pale keshamdhalilisha mwanamke yule au mfanyakazi yule, inakuwa haistahiki kukaa naye tena, kwa sababu sheria inakuwa yule keshamdhalilisha hastahiki kuishi naye kwa sababu sio mke wake kisheria.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye masuala ya watoto. Watoto wengi wanadhalilishwa kijamii, na wengi ni wanafunzi wa skuli wanaodhalilishwa katika masuala haya ya ubakaji. Watoto hawa wanakamatwa na watu wa nje, wanawafuata katika maeneo ya skuli au vyuoni au mabarabarani humo wanaishi na watu waliokuwa sio wa kawaida. Suala hili linapelekea sana jamii kuwa unapomuambia mzazi wake yule mtoto kwamba mwanao nimemkuta sehemu fulani na mtu aliyekuwa hastahiki, basi mzazi anataka ushahidi kamili ili kuonekana kwamba mwanawe umemkuta sehemu hakubaliani na wewe, anaona kama umemdhalilisha mwanawe, kwa sababu suala hili linawapelekea sana kwa wale wanafunzi wa skuli pamoja na wa vyuoni au madrasa.

Mhe. Naibu Spika, masuala haya zaidi walimu wa vyuo wanaowamiliki watoto wa kike na watoto wa kiume kuwa nao karibu sana kwa masuala ya ndani ya vyuo. Mfano kama hawa wadhamini wa vile vyuo, au wadhamini wa skuli anakua yuko karibu sana na yule mtoto. Sasa akiishinaye vile karibu sana basi yule mtoto anakua anampenda. Maana tukitaka tusitake kwenye Usheikh na kwenye elimu, wako walimu wanaowadhalilisha wanafunzi sana, sana na kesi hizi zipo nyingi, wapo wanafunzi wanadhalilishwa na walimu sana...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ikaribie hiyo *microphone*.

Mhe. Khadija Omar Kibano: Ahsante sana. Wanawadhalilisha sana wanafunzi hawa. Zaidi wanafunzi hawa wanakuwa na walimu wao wako karibu kwa kuishi kimazingira ya elimu, kimazingira ya nyumbani, wanakuwa wako karibu kuishi katika familia zao na ni watu wa karibu sana. Sasa wao wanaishi nao hawa, mwalimu wa skuli anamiliki darasa lile kwa kummilikia mtoto yule au mwanafunzi yule tayari yeye anamjengea hisia ya upendo wa ndoa ama masuala ya ndoa. Kwa hivyo, suala hili ni zito sana kwa wanafunzi na walimu, tunawataka masheikh wetu, walimu wa vyuo wa madrasa, masuala haya wayakate mara moja, kwa sababu tunaziona hizo kesi ziko nyingi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nina ushahidi kamili katika Jimbo langu la Mtambwe, kuna wanafunzi wasiopungua watatu wamedhalilishwa kijinsi kwa masuala ya ubakaji na utelekezwaji katika suala hilo la ndoa.

Mhe. Naibu Spika, nije katika suala la mambo ya wanawake. Wanawake jamani tukitaka tusitake tunatelekezwa vibaya sana kwa masuala ya watoto. Wazazi wakiume wakishatuacha hawatutaki tena na watoto wetu, wanatutelekeza vibaya sana. Kwa sababu wewe mwanamme umeshawamiliki wake zako wawili au watatu, halafu wewe unamchukua mke wako mmoja tu unayehisiana naye kwenye masuala yako ya kindoa kuliko wale wengine

wenye watoto wale. Baadae unamchukua mmoja mwenye watoto wengi ili unataka mapenzi yako yatulie katika nyumba yako, unaishi na yule mmoja tu aliyekuwa hana watoto, wale waliokuwa wana watoto sio wanawake waliokuwa ni wazuri kwako wewe tena. Kwa hivyo, mimi nalitilia mkazo suala hili, hao wanaume waliokuwa wanatudhalilisha kijinsi kwa sisi wanawake na watoto tunawaomba watupende na sisi tuliokuwa tuna familia zao. Wasimmiliki mwanamke aliyekuwa ni mmoja tu na akawa hana mtoto, ati ni kwa kutaka kupata starehe zake za masuala ya ndoa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nieleze jengine kuhusu masuala ya kutelekezwa kwa wanawake wenye watoto. Wanaume wakishatuacha wanatuachia mzigo mkubwa na mzito wa kuwabeba watoto tuwasomeshe, tuwapeleke chuoni, tuwavishe nguo, tuwatafutie matibabu na tuwatafutie kila kitu, iwapo mwanamme yule ni mfanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hawezi kuwasaidia watoto wale na wakati keshaniacha, nikienda kwenye mashtaka na sheria za wanawake na watoto, nikienda kumshtaki, basi ananiambia siwezi kukuchumia wewe wakati si mke wangu tena huku mimi nina mzigo mzito wa wanawe wasiopungua saba mpaka nane na naishi nao, nikenda nikimshitaki kama nina haki ya kukushitaki na unieleze kwa ajili gani watoto hawa huwezi kuwamiliki na mimi ninao, ananambia wewe siwezi kukuchumia wakati si mke wangu.

Kwa hivyo, ninachokiomba mimi hapa Wizara...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, malizia.

Mhe. Hadija Omar Kibano: Naiambiwa Wizara ya Wanawake na Watoto au Mhe. Waziri, suala hili la utelekezwaji kwa watoto kwa wanawake litiliwe mkazo na watakapokwenda na mashitaka yao wanawake wapewe kipaumbele ili wafanyakazi wale kama ni wafanyakazi au ni mchumi yeyote anayefanya katika maisha yake ya kupatia kipato kidogo, naomba lisimamiwe kwa nguvu na wao wapewe haki zao za msingi zinazostahiki.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuchangia jioni hii ya leo, nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu S*ubuhana Wataala* ambae amejialia pumzi ya kuweza kusimama na leo tena, lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutuandalia hotuba hii na leo tukaweza kuichangia.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze moja kwa moja na programu ya uwezeshaji, programu hii kwa kweli imefanya kazi kubwa ya kuwaweza wananchi katika suala zima la kujikwamua kiuchumi, historia inaonyesha kwamba mara nyingi kuna kundi linakuwa linasahauliwa na hili ambalo nalipigia mimi kelele kundi la watu wenye ulemavu. Hii inaonyesha dhahiri kuwa hata katika kitabu hichi cha Mhe. Waziri, kundi hili sikuona sehemu ambalo limetajwa na limewezeshwa kiasi gani, kutokana na hilo basi labda pengine limesahaulika ingawa Wizara hii inaitwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, haina maana kuwa kundi la vijana wenye ulemavu kusahauliwa, au kundi la wanawake wenye ulemavu kusahauliwa, au kundi la wazee wenye ulemavu kusahauliwa.

Labda nimuombe Mhe. Waziri, pengine sikuangalia vizuri aje aniambie tu kwa kipindi hichi vijana wangapi wenye ulemavu waliweza kuwezeshwa, vikundi vya wanawake wenye ulemavu vingapi viliwezeshwa na kwa namna gani.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, naomba tuelewe kwamba sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuliopo hapa na ile jamii ambayo iko nje ielewe kwamba kundi hili lina hali ngumu ya kiuchumi kuliko kundi jengine lolote ambalo tunaliangalia na kuliwezesha, mara nyingi vijana wenye ulemavu wanakuwa wanakabiliwa na hali ngumu kubwa kuliko vijana wengine wowote kutokana na hali zao, ukiangalia wanawake wenye ulemavu vile vile wanakuwa na hali ngumu kuliko mwanamke ile hali ngumu tunayoitambua ya mwanamke. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri, pamoja na kuwa wamepanga kuwezeshwa hivi vikundi vya vijana, wazee na wanawake basi waangalie kwa huruma kuangalia haya makundi ambayo nimeyataja, tusiwe tena na ile hali ya kusahau sahau haya makundi, kusema kweli haya makundi yako katika hali ngumu.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo, niende katika suala zima la uzalilishaji, kuhusu suala la uzalilishaji naipongeza sana Wizara kwa jitihada zake inayochukua kuhakikisha hili suala linaondoka, lakini tu suala hili linakuwa gumu kwa sababu sisi jamii wenyewe ndio tunaofanya haya matendo, kuteswa kwa wanawake hawateswi na mtu mbali, ni sisi miongoni mwetu ndio tunaotesa wanawake, kupiga sisi wanaume ndani ya jamii ndio tunaopiga.

Halikadhalika, kubaka vile vile jamii yenyewe ndio inayoshughulika na kubaka, lakini suala la ubakaji kwa watoto wenye ulemavu au vijana wenye ulemavu sasa hivi ndio imekuwa hao wabakaji wanaona ndio dili, kwa sababu tu ya mapungufu ya sheria tuliyonayo, sheria tuliyonayo haiwezi kumtia hatiyani mtuhumiwa kutokana na ushahidi, watu wenye ulemavu wanashindwa kutoa ushahidi hasa ulemavu wa akili, kwa maana hiyo hawa wabakaji

wanakimbilia zaidi katika hao watoto au vijana wenye ulemavu wa akili kuwabaka kwa sababu tu wanajua hakuna ushahidi wowote ambao utapatikana katika kesi ile.

Kwa maana hiyo utakuta vitendo hivi vinaendelea, wanabaka na wanalawitiwa lakini tu Sheria ya Ushahidi mapungu yake ndio yanayopelekea kufanyika haya, tuna imani hiyo, lakini kwa vile sheria hii tayari imeshafanyiwa mapitio tuna imani kuwa itakapokuja hapa tutaiangalia vizuri na baadae tunaweza tukapata muafaka wake.

Lakini tu si udhalilishaji huo wa kubakwa na kulawitiwa, watu wenye ulemavu au watoto wenye ulemavu wanakabiliwa na udhalilishaji mwengine ambao huu unafanywa kutoka ndani ya familia zao, mtoto akishakuwa mwenye ulemavu basi zile huduma anazopewa yule asiye na ulemavu ni kubwa ukilinganisha na mwenye ulemavu, yaani mtu mwenye ulemavu hapati huduma kama zile, anaonekana yeye katika familia kama ni mtu mwengine, pengine kama kusoma huyu hatopelekwa skuli kwa sababu ya ulemavu wake.

Pengine kununuliwa nguo mpya huyu atanunuliwa mbili mwenye ulemavu atanunuliwa moja, ile ni aina moja ya udhalilishaji, lakini isitoshe tuna tabia ya familia kuwafungia wale vijana wenye ulemavu ndani wao wakinda pengine makondeni au katika shughuli zao. Katika hali kama ile anafungiwa ndani basi pale mbakaji ndio anapokuja au mtu yeyote ambae amekusudia kumtendea vibaya yule mwenye ulemavu ndio anapata nafasi ya kumfanyia vibaya.

Kwa hivyo, kwa hili nimuombe Mhe. Waziri katika vipindi vyao vya kuelimisha basi wajitahidi kuwaelimisha na wazazi wenye watoto wenye ulemavu kuachana na hizi tabia ambazo zinawapelekea hawa watoto wenye ulemavu kupata madhara, na kupelekea kuwa wadhururaji, lakini wakiwatunza vizuri basi wale watoto nao watakuwa vizuri na mambo mengi yale yanayowapa ya madhara yanaweza kuwaepuka.

Mhe. Naibu Spika, nije katika kifungu hichi kinachohusiana na msaada wa wazee, kama nilivyotangulia kusema; kundi la watu wenye ulemavu linakuwa linasahauliwa, lakini pengine katika msaada huu limekumbukwa, nimuombe Mhe. Waziri, atakapokuja hapa aje atueleze ni wazee wenye ulemavu wangapi ambao wameweza kupatiwa huu msaada, au kuna mikakati gani ya kuhakikisha kwa makusudi wazee wenye ulemavu nao wanapata hii huduma ya msaada.

Mhe. Naiu Spika, kutokana na hayo machache tu, naomba niunge mkono hotuba hii kwa asilimia thamanini na ishirini naweka baada ya kujibiwa. Ahsante sana (*Makofi*)

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya lala salama katika kuchangia hotuba hii ya Wizara inayohusiana na watoto. Nitangulize kutoa shukurani za dhati kwa Waziri ambae amewasilisha hotuba hii, lakini vile vile niwashukuru watendaji wake wote, nishukuru kamati ambayo imewasilisha ripoti nzuri ambayo imesomwa na Mwakilishi wetu Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), hapa niseme tu kwamba Wizara inayohusika kama wataichukua ripoti ya kamati ile na kuifanyia kazi vizuri basi mapungufu mengi yanaweza kuwekwa sawa. Hatimaye utekelezaji wa yale ambayo yamepangwa unaweza kwenda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi kutokana na suala la muda nitazungumza mambo machache tu na nina imani kwamba wenzangu wameshayachangia mengi na niwapongeze sana kwa michango yao mizuri, akiwemo Mheshimiwa Mpakabasi Mimi nianze na programu ya ukuzaji na upatikanaji wa ajira zenye staha.

Mhe. Naibu Spika, wenzetu wamekiri kwamba kuna mawakala binafsi wanaohusikana na ajira hizi kwamba hawana uelewa juu ya mambo ya mikataba na mimi nikubaliane nalo hilo, ni ukweli usiofichika kwamba suala la ajira ni suala nyeti na vijana wetu ni kweli wamepata ajira nyingi sana katika nchi hizi za Arabuni, lakini kutokana na kuzuka wimbi hili la kutolewa, mimi naweza kusema kwamba kuna uzembe kiasi fulani katika utoaji wa vibali au leseni kwa hawa mawakala binafsi. Hivi sasa kumekuwa na mawakala ambao hawa kazi yao ni kuuza ubinadamu, kwa hivyo, kuna biashara ya kuuza binadamu, niiombe sana Wizara hii iwe makini katika kutoa vibali vya mawakala hawa, kuna mawakala binafsi sasa hivi wanafanya biashara ya kuuza binadamu, vijana wetu wanaokwenda katika nchi hizi kuna malalamiko mengi, wengine wakifika tayari wananyang'anywa *passport*, wananyang'anywa simu za mikononi na pale wanakwenda kama ni soko la utumwa na baadae pale wanasambazwa katika maeneo mbali mbali wakiwa hawana mawasiliano na kwao, kuna wengine wanalazimishwa kufanyakazi za ukahaba.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri, nikuombe sana ulichunguze sana suala hili la mawakala binafsi wa masuala haya ya ajira, hivi sasa imekuja hali nyengine ya utumwa na wenzetu Wazanzibari wengi ambao wanakwenda wakija wanasikitika kutokana na mazingira ambayo wanayakuta kule.

Mhe. Naibu Spika, sasa nielekee katika suala zima la Programu ya Mikopo ya Uwezeshaji, katika kitabu hichi cha hotuba Mhe. Waziri, ameweza kuonyesha takwimu ambayo iko katika Kiambatanisho cha 67, takwimu hii inaonyesha juu ya mikopo ambayo imetolewa, wasi wasi wangu ni huu mikopo ya vikundi ni mikopo 115, lakini mikopo ya watu binafsi 222, mimi ninavyoona hii ni hatari. Mfuko huu utakapo-*base* zaidi katika watu binafsi kuliko vikundi hii ni hatari, hivi sasa ni wakati ambao tutilie mkazo zaidi kwa sababu Serikali inahamasisha vikundi itakuwaje watu binafsi wapate mikopo mingi zaidi kuliko vikundi ambavyo Serikali ndio inavihamasisha, lakini vile vile hakuna takwimu ambayo imeonyeshwa juu ya urejeshaji wa mikopo hii. Ningependa sana atakapokuja Mhe. Waziri, atupe *data* ya urejeshwaji wa mikopo hii kwa sababu kuna wajasiria mali wengi ambao wanahitaji fedha hizi ili kuweza kufanya shughuli zao za uzalishaji.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, atakapokuja ni vyema sasa atuambie kwa nini watu binafsi wameweza kupata mikopo mingi zaidi kuliko vikundivya ujasiriamali, lakini vile vile katika hili Waheshimiwa Wawakilishi, tunahusishwa vipi na vikundi ambavyo vimo ndani ya maeneo yetu, kwa sababu wakati mwengine wanaweza wakaenda vikundi au watu binafsi kutoka katika Jimbo, lakini Wawakilishi hatuna habari, yakija yakiharibika basi mnaweza mkawa viongozi sisi tukaja kuingia katika matatizo. Ningependa sana Mhe. Waziri, awe karibu na sisi Wawakilishi wa vikundi au watu binafsi ambao wanapeleka maombi ya kutaka mikopo ya uwezeshaji.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie juu ya suala la nyumba za kulelea yatima. Kwanza nishukuru Serikali kwa kuweza kutoa fursa hii ya nyumba za kulelea yatima kwa sababu tuna yatima wengi sana, wakati mwengine baadhi ya familia zinashindwa kuweza kuchukua majukumu yao katika kuwaendeleza yatima. Zanzibar ni nchi ambayo ilikuwa isiwe na nyumba za yatima kutokana na maisha yetu ambayo tuliishi, lakini kutokana na wakati huu nyumba hizi zipo.

Nataka tu Mhe. Waziri, atakapokuja aweze kutwambia nyumba hizi kwa Zanzibar au kwa Unguja ziko ngapi na kwa Pemba ziko ngapi na kuna vigezo gani vinavyotumika kuweza kutoa kibali cha kuweza kuandaa au kuweka vituo hivi vya yatima. Kwa sababu kuna malalamiko mengi kwamba kuna mayatima wanaoteswa na watu hawa na kuna watu ambao wanaweka nyumba hizi kwa ajili ya kuweza kuwafanya mayatima hawa ni migongo yao ya kuweza kupata fedha.

Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri, nyumba hizi za yatima azitazame vyema kwa sababu kuna watu wanaochukua migongo ya yatima katika kujitajirisha. Mhe. Naibu Spika, kutokana na muda na mimi nitenge muda wako nikushukuru sana na niipongeze Wizara kwa kuweza kuwasilisha hotuba yao na watendaji wote na mimi pamoja na hayo ambayo nayataka Mhe. Waziri, atuwekee wazi, lakini naiunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia ahante sana. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Naibu Spika, kidogo tu.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, tumeshamaliza siku, hayo mambo ya nini tena sasa hizi?

Mhe. Simai Mohamed Said: Kidogo tu.

Mhe. Naibu Spika: Kidogo kitu gani na tumeshamaliza muda, muda sasa hivi hauruhusu. Muda ushaisha sasa hivi, Mheshimiwa hicho kidogo kije kesho.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Naibu Spika, hicho kidogo kitakuwa hakipo kesho.

Mhe. Naibu Spika: Muda umeisha, Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru sana kwa michango yenu na natarajia kwamba kesho tukijaaliwa tunaanza moja kwa moja na Mhe. Waziri, kwa maana hiyo Mhe. Waziri, kesho atakuja hapa kufanya majumuisho na kujibu hoja za wajumbe walizochangia, kwa maana hiyo wale wote ambao walikuwa hawajapata nafasi ya kuchangia, basi wapeleke michango yao kwa maandishi.

Baada ya kusema hayo machache naahirisha kikao hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 8.50 Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 15/6/2016 Saa 3.00 Asubuhi)